ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/Jimbo la Donge
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z/Jimbo la Jang'ombe
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Uteuzi wa Rais
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake
21.Mhe. Iddi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile
41.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja
42.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
43.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani
44.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni
45.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe
46.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani
47.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe

48.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi
49.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
50.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni
51. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani
67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja

68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili – Tarehe 22 Juni,2009

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Wanyeviti): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli Wizara ya Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi). Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Maoni ya Upande wa Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 10

Ujenzi wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga jengo jipya la Baraza la Wawakilishi huko Mbweni kwa ushirikiano wa Afisi ya Baraza na Kampuni ya AL-Youseif ambalo kwa hadhi yake litakidhi haja. Ujenzi huo utajumuisha ujenzi wa nyumba ya Spika,

(a) Jengo jipya la Baraza na nyumba ya Spika inategemewa kumalizika lini.

(b) Kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wasioishi katika Mkoa wa Mjini na Magharibi hupata shida ya makaazi wanapokuwa katika shughuli za Baraza hapa Mjini, Serikali ina mpango gani juu ya kujenga hosteli kwenye eneo la karibu na jengo hilo la Baraza.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa niaba ya Serikali pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi tunazipokea pongezi za Mheshimiwa mwakilishi na tunamshukuru kwa kuziona na kuzithamini juhudi zetu. Pili kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Afisi ya Baraza la Wawakilishi iliamua kuanzisha Ujenzi wa Jengo jipya la Baraza ili kuliwezesha Baraza kufanya shughuli zake kwa nafasi na katika mazingira ya utulivu zaidi. Jambo hilo limetokana na ukweli kwamba jengo hili linalotumika sasa kwa shughuli za Baraza limeonekana kuwa halina nafasi ya kutosha kwa shughuli za Baraza za wakati huu ambazo zinazoendelea kuongezeka kadiri siku zinavyosonga mbele. Vili vile Jengo hili limechakaa sana na linakosa hadhi inayolingana na chombo chenyewe, katika wakati huu wa kukua kwa demokrasia nchini petu na ulimwenguni kwa jumla.

Aidha, jengo hili lina ukosefu wa nyenzo zinazohitajika kufanikisha shughuli za kisasa za mabunge zinazoendana na kukua kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, hasa teknolojia ya mawasiliano. Pamoja na hayo mazingira ya eneo lilipo jengo lenyewe hayatoi utulivu wa kutosha kufanyika kwa kazi za Baraza kwa ufanisi kutokana na kuzungukwa na harakati za mji. Mambo yote hayo yameifanya serikali kuwa na sababu za kutosha kuanzisha Ujenzi wa Jengo jipya ili kufanikisha shughuli za Baraza. Ujenzi huo ulioanza mwaka 2004 unaendelea katika hatua za kumalizia *(finishing)* baada ya kukamilika umbile *(structure)* na kuezekwa.

Katika hatua nyingine vile vile, Serikali kupitia Baraza la Wawakilishi ina mpango wa kujenga nyumba ya makaazi rasmi ya Mhe. Spika wa Baraza. Harakati za ujenzi huo ziko katika hatua za mwanzo. Michoro imekamilika na hivi sasa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kupitia Bodi yake ya Tenda iko kwenye mchakato wa kutafuta mkandarasi wa kujenga nyumba hiyo ya makaazi rasmi ya Mhe. Spika.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu mheshimiwa mwakilishi swali lake Nam 10 lenye vipengele a) na b) kama ifuatavyo:-

a) Tunatarajia kwamba ujenzi wa jengo jipya la Baraza huko Mbweni utamalizika haraka iwezekanavyo. Matarajio yetu ni kwamba ujenzi utakamilika mwishoni mwa mwaka huu yaani Disemba, 2009.

   Kuhusu ujenzi wa nyumba ya makaazi rasmi ya Mhe. Spika hapo Migombani unatarajiwa kuanza na kukamilika ndani ya mwaka wa fedha wa 2009/2010.

b) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mjumbe kwamba tunaelewa kuwa baadhi ya wajumbe wanaotoka nje ya mji wa Unguja hawana nyumba zao mjini na kwa kiasi fulani wanapata shida ya makaazi.

   Jambo hilo tumelifikiria na limo katika mipango yetu. Tunakusudia kujenga Hosteli ya Wajumbe wa Baraza ili wale Wajumbe ambao hawana makaazi hapa mjini waweze kufikia wanapokuja kwa ajili ya shughuli za Baraza.

   Tumekuwa tukifanya juhudi kupata msaada wa wahisani kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli hiyo tangu tulipokuwa tunatafuta ufadhili wa ujenzi wa Jengo la Baraza. Juhudi hizo ziliendelea hata baada ya kupata ufadhili wa jengo la Baraza bila ya mafanikio. Sote tunaelewa kwamba uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo. Hata hivyo, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Baraza tunafikiria uwezekano wa kuuingiza ujenzi wa Hosteli katika miradi ya maendeleo katika Bajeti ya Serikali.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika jibu mama amekiri kwamba serikali ina adhma nzuri ya kujenga jengo hilo jipya la kileo ili liende na wakati, lakini pamoja na hivyo pia kutakuwa na ujenzi wa nyumba ya Mhe. Spika, ambae kwa hivi sasa na yeye hana makaazi mazuri ya kisheria.

Je, huyu mfadhili anayejenga jengo la Mhe. Spika, ni mradi mmoja huu huu au kuna mwengine. Na kama kuna mwengine atutajie ni nani?.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, katika jibu langu nilisema jitihada inayoendelea sasa hivi ni kutafuta *contractor.*

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu a na b.

Mhe. Waziri katika jibu lake mama alisema kwamba jengo hili ambalo tunaendelea nalo na shughuli sasa hivi linaonekana kwamba halikidhi haja na pengine lina upungufu wa vitu vingi, kwa hivyo tunatarajia kupata jengo jipya karibuni.

a) Jengo hili lilikusudiwa kujengwa kabisa kama ni Baraza na kama hivyo sivyo lilikuwa katika taasisi gaini kabla ya shughuli hizi za baraza na baada ya kuhama na kuhamia jengo jipya itarudishwa katika taasisi hiyo.

b) Kwa sababu shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinahusisha visiwa vyote viwili, kuna mpango gani wa kutengeneza Afsisi za Baraza zilizoko Pemba na pengine na ukumbi kwa sababu sasa hivi hali inaonekana ni mbaya.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, jengo hili sio lilionekana halikidhi tu lakini tuliliona sote kwamba halikidhi mahitaji ya kuendesha Baraza la Wawakilishi na ndio tukapitisha uamuzi wa kujenga jengo lile.

Jengo hili halikukusudiwa kuwa jengo la Baraza la Wawakilishi hapo lilipojengwa mwanzo kwa sabahu hilo jengo la kutunga sheria kwa wakati ule halikuwepo hapa lilikuwepo kwenye *Victoria garden*, hili limegeuzwa kuwa jengo la Baraza la Wawakilishi baada ya kuona ipo haja ya kutafuta mahala pa kutafuta wawakilishi wananchi ili waweze kutoa mawazo ya wananchi.

Hili jengo ni la serikali na kwa kipindi fulani lilikuwa katika sehemu ya Mila na Utamaduni, lakini baadae ndio limegeuka limekuwa jengo la Baraza, lakini hili jengo bado la serikali kwa hivyo tukiondoka hapa sisi jengo bado linaendelea kuwa la serikali, sasa serikali ndio itaamua ilitumie vipi hapo baadae.

Mhe. Spika, uwezo wetu utakaporuhusu maana hata huo ujenzi wa Baraza la Wawakilishi la huko Mbweni linalojengwa sasa hivi uwezo wa serikali ulikuwa mdogo ndio tukatafuta mfadhili, kwa hivyo tutajitahidi kuona kwamba tunapata fedha kwa kufanyia ukaratabati wa jengo letu lilioko Pemba.

Mhe. Spika: Kabla sijamwambia Mhe. Hijja aulize swali na mimi kwenye swali hili nimefurahi sana kwa sababu tulikuwa mimi na Mhe. Waziri Kiongozi tulikuwa tunaulizana hatma ya jengo hili itakuweje sasa kumbe Mhe. Zakiya alikuwa anasikia. *(Kicheko)*

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba jengo letu litamalizika mwezi wa Disemba, 2009.

a) Je, kumaliza kwake ni pamoja na uzio.

b) Kwa kuwa pale patakuwa ni sehemu ya watu wengi mbali ya kujenga nyumba ya Spika, na hosteli kwa ajili ya Wajumbe. Je kuna mpango wowote wa kujengwa kituo cha afya.

c)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, nadhani katika mkutano wetu wa *briefing* ilielezwa kwamba uzio maana yake ni ukuta umemalizika kwa hatua ya ujenzi wa matofali na uwekaji nondo bado kupakwa rangi na kuwekwa mageti na nyenzo za kiusalama. Kwa hivyo mambo yote hayo yanakwenda sambamba katika ujenzi wa jengo hili.

Mhe. Spika, kituo cha Afya ni suala muhimu kabisa hata kama hatuna mpango, lakini itabidi lazima tufanye mpango wa kutafuta kituo cha afya karibu ili wajumbe waweze kupata huduma haraka sana, kama hapa tumeweka kwa muda pale itabidi tuweke kituo cha afya cha kudumu ili wajumbe wapate huduma.

Nam. 100

Kuanzishwa Shule za Elimu Mbadala

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Shule za Elimu Mbadala Unguja na Pemba ambapo wanafunzi wote ambao waliopata matatizo wakati wakisoma na kukatisha masomo yao hupata fursa ya kujiunga katika shule hizo ili wajiendeleze katika kuyakabili maisha ya baadaye.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kijana aliyepata matatizo na baadaye akataka kujiunga na shule hizo afuate utaratibu gani.

(b) Kwa kuwa shule hizo tayari zinatowa elimu ni wanafunzi wangapi kwa mwaka 2008/2009 walijiunga na shule hizo.

(c) Je, Mhe. Waziri ni elimu gani inayotolewa katika shule hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama vifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kuanza kwa kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Ni kweli kwamba Wizara ina utaratibu wa kutoa elimu mbadala kwa vijana waliokuwa hawakuwahi kwenda skuli na walioacha masomo njiani kwa sababu mbali mbali. Vijana hawa wanapatiwa elimu hii kupitia skuli za kawaida kwa wale walio na lengo la kuendelea na elimu ya lazima na katika vituo maalum kwa wale ambao wanashughuli zao za kimaisha na wanahitaji kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kuongeza ujuzi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kijana anaetaka kujiunga na madarasa haya anatakiwa kujiandikisha katika skuli ya msingi au Kituo cha Elimu Mbadala kiliopo karibu na anapoishi.

(b) Katika mwaka 2008/09 vijana 1190, kati yao wanaume 805 na wanawake 385, walijiunga na madarasa ya Elimu Mbadala.

(c) Wanafunzi wanaojiunga na madarasa ya Elimu Mbadala katika skuli za kawaida wanasoma masomo ya kwaida kama wanafunzi wengine ingawa kuna tofauti katika mbinu za ufundishaji. Vijana hawa wanawekwa katika darasa kwa mujibu wa uwezo wao na baada ya mwaka mmoja hupelekwa madarasa ya mbele kutokana na matokeo yao ya mitihani. Baadhi ya wanafunzi wa Elimu Mbadala wameonyesha uwezo mkubwa na kufikia kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika skuli za mchepuo.

Kwa vijana wanaojiunga na Vituo vya Elimu Mbadala, mbali ya masomo ya kawaida, hujifunza kazi za amali kama vile uchongaji, Uashi, Umeme na kazi za hoteli.

Tunatoa wito kwa vijana ambao hawakuwahi kwenda skuli na walioacha masomo njiani kujiunga na madarasa ya Elimu Mbadala yalioko katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.
Mhe. Waziri amekiri kwamba hivi sasa ziko skuli zinasomesha Elimu Mbadala hizi za kawaida. Katika kusomesha huko mwanafunzi huwa analipa ada.

a) Je, ada inayolipwa kwenye skuli za kawaida na hapa Rahaleo zinalingana.

b) Kwa kuwa amezungumza kwenye majibu yake kwamba katika mafunzo hayo wanayopewa, lakini pia yapo mafunzo ya utalii, ninavyofahamu mimi mafunzo ya utalii yana nyanja nyingi. Je, wao wanasomesha nyanja zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Wanafunzi ambao wanasoma katika madarasa ya Elimu Mbadala wanachukuliwa kama wanafunzi wengine na ada wanazotozwa zinakuwa ni zile zile za kawaida kama wanafunzi wengine.

Kuhusu nyanja za Hotali nadhani hapa wanapewa ile elimu ya msingi tu ya kuweza kujiendeleza kwa nyanja hizo za hoteli, lakini hawafundishwi kwa undani zaidi yale masomo ya hoteli ya ndani ila wanapewa elimu ya msingi tu.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa Elimu Mbadala hupewa wale ambao wamepewa elimu ya darasani kutokana na sababu mbali mbali na kwa kuwa sasa hivi nikiuliza swali hili la nyongeza katika Skuli ya Jadida Wete Pemba, kuna wanafunzi wa darasa la saba waliofukuzwa kwa sababu hawajalipa ama ada ya kawaida au fedha ya kitambulisho au fedha ya mtihani wa majaribio ambao umeshafanywa na wao hawakupata nafasi ya kufanya.

a) Je. Mhe. Spika, Wizara inatayarisha Elimu Mbadala kwa makusudi.

a) Wizara itachukua hatua gani ili wanafunzi hawa waendelee na elimu ya kawaida na wasingojee kuja kuingia kwenye elimu mbadala.

b) Kwa wale wanafunzi walioko Pemba ambao wanahitaji elimu mbadala wajiunge na skuli gani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nashukuru ile ruhusa uliyonipa ya kwenda safari nimesharudi salama na nipo tayari kwa shughuli za kikazi za Baraza.

Pili naomba kujibu swali la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

Lakini kabla sijajibu naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu waziri kwa jinsi alivyoweza kujibu maswali yote ya awali, lakini hili swali nitajibu kwa jumla. Suala la elimu mbadala ni jambo la muda tu kwa maana ya kwamba hata elimu ya watu wazima nalo ni la muda, kwa sababu tukifika hatua ina maana masuala haya yote yatakuwa yamemalizika ya elimu ya watu wazima na elimu mbadala imeisha. Kwa sababu haja yetu kila aliyekosa nafasi au fursa ya kupata elimu katika utaratibu rasmi, basi huwa tunampatia nafasi hii kwa kipindi kile ambacho alikuwa hayupo.

Kuhusu serikali kutayarisha elimu mbadala nadhani Mhe. Moh'd Ali Salim atuelewe kwamba serikali haina nia hiyo kama nilivyosema awali, lengo letu hili jambo tulimalize katika kipindi kifupi iwezekanavyo.

Kuhusu tutachukua hatua gani mimi nimekuwa nikisema hilo na naendelea kulisema, haturuhusu na hatutoendelea kuruhusu serikali hata mara moja kuwafukuza wanafunzi wote ambao kwa njia moja au nyengine wanashindwa kulipa ada kwa umasikini au kwa njia nyengine zozote, isipokuwa tumesema kamati za skuli zitumia busara na hekima kuwaita wazazi na kuwapa utaratibu maalum, kwa wale ambao hawana uwezo kabisa, basi hata kusamehe hakuna matatizo. Lakini kwa wale ambao wanahisi wanaweza kuchangia kwa utaratibu *Primary* mchango wetu ni Shs. 3,000/= kuchangia, sasa kama huwezi kutoa kwa wakati mmoja unaweza kutoa mia au mia mbili au utaratibu mwengine unaoweza kutumika pale skuli. Kwa hivyo, naomba suala hili ambalo limetumika Jadida kama ni sahihi kama alivyosema Mheshimiwa na kalifanyia utafiti, basi watoto wale warejeshwe mara moja skuli na waendelee kupata elimu yao kama kawaida.

Kuhusu Pemba watapata wapi elimu hii mbadala katika bajeti yangu ambayo nitaisoma tarehe 10,11, na 12 tukijaaliwa nitamdokeza kidogo tu ajue kwamba tayari tumeshapata pesa na tumezungumza na wenzetu wa ADB na tumetenga karibuni shilingi 253 milioni tunajenga kituo chengine cha Elimu Mbadala maeneo ya Wingwi kule Pemba ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi napenda kumuuliza Mhe. Waziri hasa katika jibu lake la sasa hivi kwa kuwa alisema elimu hii ya mbadala ni kwa muda tu.

a) Kwa nini tunajenga majengo kwa ajili ya elimu mbadala nayo ni ya muda.

b) Je, anatoa dhamana yeye kwamba hakuna tena kukimbia skuli kwa watoto ambalo ni suala zima la elimu na misingi yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Hapa asubuhi lilijibiwa jibu hapa kwambe jengo hili lilikuwa halikukusudiwa kufanywa shughuli za baraza, lilikusudiwa kufanya shughuli nyengine. Lakini kutokana na haja ilivyojitokeza tumelitumia kwa shughuli za Baraza, sasa tunajenga majengo ya muda ya elimu mbadala.

Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba kutoka mafunzo ya elimu mbadala kuna elimu ya amali na mafunzo ya ufundi, kwa hivyo majengo yetu haya tutaendelea kuyatumia kwa jambo la kudumu hilo la elimu ya amali kwa sababu ni sehemu moja ya kuwezesha vijana wetu kupata taaluma ya ufundi ili waweze kujiajiri wao na kuajiri wengine.

Nam.13

Tatizo la Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara.

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza :-

Tunaipongeza wizara kupitia Shirika la Umeme kwa kusambaza umeme hadi vijijini na kwa kufunga mita za *TUKUZA* kwa baadhi ya maeneo ya mijini. Tatizo kubwa kwa sasa kwa Shirika ambalo ni changa moto ni kukatika kwa umeme bila ya mpangilio na kusababisha baadhi ya vitu vya wateja kuungua.

(a) Je, hili tatizo la umeme kukatika mara kwa mara husababishwa na nini.

(b) Je, Mhe. Waziri kuna kitengo maalumu cha fidia kwenye Shirika hili ili kumlipa mteja hasara anayoipata.

(c) Hivi sasa Shirika la *TANESCO* linatumia Kampuni binafsi kufanya kazi za kuunga umeme. Mhe. Waziri unalionaje suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji Ujenzi Nishati na Ardhi – Alijibu :-

Mhe. Spika , kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Na. 13 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kukatika kwa umeme kunasabishwa na mambo mengi yakiwemo haya yafuatayo:-

- Kukatika kwa umeme kutoka Tanesco Tanzania Bara.
- Kuzidiwa uwezo kwa Transfoma kutokana na matumizi makubwa ya umeme kwa wakati ule. Wote tunakumbuka mwezi 28 na 29 yaumu shaka pamoja na mwezi 30 mwezi wa Ramadhani matumizi ya umeme kwa siku tatu hizo huwa yanaongezeka sana. Watu wengi kwa siku kama hizi huwa wanatumia makuka kwa mambo ambayo tunayaelewa, kwa hivyo kuna kuwa na kuzidiwa kwa transfoma kwa siku kama hizi.
- Uchakavu wa miundo mbinu kama vile nguzo, waya n.k.
- Matatizo yanayosababishwa na wanyama kama kunguru, komba , nyoka, wakati mwengine kunguru wanaporuka wakati wa kujenga wanachukua taka taka nyingi tu hata waya anaweza kuchukua akenda nao kwenye waya kuu za umeme kwa bahati mbaya pengine waya ni mrefu unagusana na mwengine sasa huleta shoti na kusababisha kukatika kwa umeme.

(b). Kitengo tunachokitumia kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Kuwalipa fidia wananchi wanaopata hasara kutokana na matatizo ya kukatika kwa umeme.

Kwa mfano kwenye mwaka 2007 Shirika la Umeme lilipa jumla ya fidia ya Shs. 4,244,750 kwa watu 42 katika maeneo yafuatayo. Michenzani jumla ya watu wanne ambao walilipwa Shs. 257,400/= kwa Mchina watu wawili ambao wamelipwa 324,900/=, Mwanakwerekwe watu kumi na tisa wamelipwa jumla ya Shs. 673,900/=, Kibweni mtu mmoja alilipwa jumla ya Shs. 202,050/= Mbweni watu tisa ambao walilipwa jumla ya Shs. 1,966,500/= Mwera watu wawili ambo wamelipwa Shs. 500,000/= Mwembemakumbi watu watano ambao wamelipwa Shs. 320,000/=

Kwa mwaka 2008 Unguja walilipwa Mwanakwerekwe Melinne walilipwa watu 19 jumla ya Shs. 400,000/= KMKM Shs. 700,000/= Jendele watu 15 wamelipwa Shs. 390,000/=

Chumbuni Mabanda ya Ng'ombe watu 10 Shs. 319,150/= Kiembesamaki kwa Kimti watu 8 Shs. 292,000/= Mtoni Sukita watu 29 Shs. 1, 386,000/= Mwembemakumbi watu 6 Shs. 425,700.

Kwa upande wa Pemba mwaka 2008. Mtu mmoja ambae amelipwa Shs. 600,000/=.

Kwa mwaka 2009. Unguja. Mfenesini watu 6 Shs. 294,000/= Chuini watu 12 Shs. 845,000/= Kiembesamaki kwa Kira watu 4 Shs. 335,000/=.

Kwa Upande wa Pemba mwaka 2009. Kwale watu 3 Shs. 315,000/= Mtemani watu 5 Shs. 1,305,000/= Jumla inakuwa ni Shs. 3,094,000/=.

Mhe. Spika, kwa hizi mwaka huu wa 2009 bado malipo hayo hayajalipwa lakini yamo katika matayarisho ya kulipa

(c). Kwa hapa Zanzibar hatuna kampuni binafsi zilizoruhusiwa kuwaungia umeme wananchi. Mhe. Spika, suala hili ni zuri kwani linapunguza urasimu, lakini linahitaji utafiti wa kina kwani linaweza likasababisha matatizo ya kiutendaji na wimbi la uungaji wa umeme kinyume na utaratibu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Amekiri kwamba kukatika kwa umeme kuna matatizo mbali mbali, lakini na mimi nakiri kwamba umeme ikiwa si wako kama wa kununua tu pia una matatizo.

Tulisikia kuna kampuni zimejitokeza kuwekeza umeme hapa kwetu kwa kutumia maji ya bahari pamoja na upepo. Je, hili ni kweli? Kama ni kweli kampuni hizo zimefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli jitihada zinafanyika na zinaendelea hadi hivi sasa kuona Zanzibar ina umeme wake mwenyewe. Sote tunajua siri ya nguo ya kuazima sitaki kuisema, kwa hivyo, jitihada hizo zipo. Miongoni mwa nchi tunazozitegemea kuja kuwekeza ni Israel, kampuni ya *SDE (IRAILE)*. Kwa bahati nzuri Mhe. Spika, ujumbe ambao ulikwenda Israel kwa ajili ya umeme wa mawimbi uliongozwa na mimi mwenyewe.

Mhe. Spika, hivi juzi tulikuwa na mazungumzo na kijana wetu ambaye kwa sasa hivi yuko Ujerumani, yeye ni msomi kutoka Rusia lakini sasa hivi anaishi Ujerumani, alikuja na anasema kila siku yeye asubuhi hufungua kwenye *internet* kujua mambo ya Zanzibar. Tumeanza kuwa na mazungumzo na tayari tumeandikiana juu ya kutumia takataka kwa ajili ya kupata umeme, lakini pia tunaendelea kufanya jitihada ya kutumia umeme wa upepo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika suala mama lililoulizwa tuliambiwa kwamba kuna Shirika la *TANESCO* linatumia kampuni hii binafsi kufanya kazi za kuunga umeme.

Je, Mhe. Naibu Waziri hivi sasa kama shirika hili limeingizwa katika ubia wa namna hiyo, likitokea tatizo lolote katika hitilafu za nyumba ya mtu nani anawajibika? Ni shirika la *ZECO* au *TANESCO* kulipa fidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, siwezi kuwasemea *TANESCO*, lakini kwa upande wa Zanzibar kwa sababu hatujaanza na utaratibu wa kampuni binafsi kuwaungia watu umeme, basi mpaka sasa hivi ni Shirika la Umeme lenyewe *ZECO* ndilo linaloshughulika na kuwaungia watu umeme. Endapo inapotokea hitilafu zozote na mtu akaunguziwa vitu vyake vikaharibika basi ni *ZECO* ndio inayolipa.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Muulizaji wa swali la msingi alianza kwa kulishukuru Shirika la Umeme na wizara kwa kusambaza umeme pamoja na kuunga mita za TUKUZA kwa baadhi ya sehemu. Mimi nakubaliana na maelezo yake kimsingi, lakini tatizo kubwa ambalo sasa hivi tunakabiliana nalo ni kwamba katika mwahala ambamo mmesambazwa umeme hasa vijijini kuna mapungufu makubwa kwamba watumiaji wa umeme ule ni kidogo kwa sababu ya uwezo mdogo kwa kuunga umeme. Kuna baadhi ya sehemu nyengine ambamo watu wana uwezo umeme ule ungehitaji pengine nguzo tatu tu, lakini hawakufikishiwa.

Je, serikali haioni kuna umuhimu wa kuwaungia wanavijiji hawa ambao uwezo wao ni mdogo na baadae ikawa na mpango wa kuwakata kidogo kidogo au kulipa kidogo kidogo, kwa sababu kufanya hivi kunaweza kuongeza utumiaji wa umeme jambo ambalo ni muhimu katika ufanisi wa shirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya maeneo umeme umefika, lakini watumiaji ni kidogo, lakini kuna baadhi ya maeneo umeme haukufika watumiaji ni wengi.

Mhe. Spika, nia ya serikali kupitia Shirika lake la Umeme kupeleka umeme kwa wananchi wote, ama wakiwa kidogo au wengi. Pia ni kweli kwamba wako wananchi uwezo wao ni mdogo wa kuunga umeme hasa tukitilia maanani sasa hivi kuunga umeme kuna gharama kubwa. Mhe. Spika, Shirika la Umeme linao utaratibu wa kuwakopesha watu kuunga umeme hasa vijijini baada yakupata watu wa kuwadhamini.

Miongoni mwa watu ambao wanawadhamini wateja hawa ambao uwezo wao ni mdogo huko vijijini ni Wawakilishi wenyewe. Kwa hivyo, tutaendelea na utaratibu huo hasa pale wawakilishi wao wenyewe watapojikubalisha kuwadhamini wapiga kura wao kwamba waungiwe umeme kwa mkopo na walipe kidogo kidogo kusudi mteja huyu akishindwa kulipa moja kwa moja basi Mwakilishi au Mbunge ambaye amebeba hiyo dhamana taratibu za kufanya tunazijua.

Mhe. Spika: Lilikuwa ni swali la mwisho la nyongeza. Najua Mhe. Ame Mati Wadi kwa sababu alipokuwa Nairobi aliona kuna maswali mengi ndani ya Bunge yanaulizwa pale, Kanuni inasema mwisho maswali matatu.

Nam. 30

Vifaa vya Uchunguzi wa Maradhi ya Watoto,
Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza niwapongeze Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa kuwa swali nililituma kabla ya uzinduzi wa tarehe 11 June, 2009 ambapo Mhe. Rais amezindua rasmi baadhi ya vifaa vingi vilivyoletwa wizarani huko vikiwemo *CT Scan* ambacho ni kifaa cha kwa kwanza kama kile kwa Afrika, naomba swali langu hili lijibiwe kwa niaba ya wananchi wale ambao hawakuviona na wengine hawakusikia ili wafahamu. Ahsante Mhe. Spika.

Mara nyingi watoto walio chini ya miaka 10 husumbuliwa na magonjwa mbali mbali yakiwemo Neumonia, Safura, Figo, Uziwi, Polio na mengineyo. Kwa kuwa baadhi ya matatizo yao huhitaji uchunguzi ambao hapa Zanzibar hushindikana kutokana na ukosefu wa vifaa.

(a) Je, Mhe. Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vipimo vya uchunguzi wa maradhi mbali mbali yanayowakabili watoto, vinapatikana hapa Zanzibar.

(b) Je, Mhe. Waziri kwa kuzingatia kwamba watoto hawa ambazo wazee wao ni wakulima na wakwezi, ambapo ni wazee masikini wasio na uwezo wa kuwapeleka watoto wao nje ya nchi, Je, Wizara inatoa msaada gani kwa watoto hao wagonjwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu**:-**

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 30 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe . Spika , ni kweli kwamba mara nyingi watoto waliochini ya miaka 10 husumbuliwa na magonjwa mbali mbali yakiwemo Nimonia, Safura, Figo, Uziwi, Polio na kadhalika. Hali hii inatokana na miili yao kutokua na kinga kuliko ile ya watu wazima.

Mhe. Spika, vipimo vya kufanyia uchunguzi wa maradhi yote hayo vinapatikana katika Hospitali zote za Unguja na Pemba, Hata hivyo, katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa maradhi mbali mbali siyo kwa watoto tu bali hata watu wazima, Serikali yetu ya Mapinduzi kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tayari imeshafunga vifaa mbali mbali katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuwapunguzia wananchi shida na gharama za kuwapeleka nje ya nchi yetu kwa kufanyiwa uchunguzi wa maradhi yao. Miongozi mwa vifaa hivyo ni:-

- *CT Scan*
- X-*ray* mpya (*Fluoroscope*)
- Machine ya Echo
- *Ultrasound* ya macho
- Mashine ya kufanyia operesheni ya macho.
- Mashine ya kupimia *pressure* ya jicho na kadhalika.

Aidha, Kitengo cha sikio, pua na koo (*ENT*) kimepatiwa mashine mbali mbali za kufanyia uchunguzi na matibabu ya maradhi hayo.

Mhe. Spika, sambamba na uwekaji wa mashine hizo, kitengo cha matibabu ya masikio, pua na koo kimeandaa mradi wa afya maskuli kwa madhumuni ya kuondosha au kupunguza ulemavu unaoweza kutibika kama vile uziwi na upofu, jumla ya skuli 48 Unguja na Pemba zimejumuishwa. Kwa mwaka huu 2008/2009 mradi huu umeshawachunguza wanafunzi 58,957, kati yao wanafunzi 2,147 wamekutikana na matatizo yafuatayo:-

-- Kutokuona vizuri.
-- Kutoka usaha sikioni.

-- Maradhi ya ngozi.
-- Maradhi ya Kichocho na Meno
-- Ulemavu.

Mhe. Spika, mradi huo mpaka sasa umeshatoa miwani 108,vipaza sauti vya masikioni vya kutibu uziwi (*hearing aid*) 33 na kuwafanyia upasuaji wanafunzi 11. Mbali na hayo wanafunzi 462 waliokuwa na matatizo ya kutoka usaha masikioni sasa wameacha kutoka usaha baada ya kupatiwa matibabu na ushauri nasaha.

Mhe, Spika, katika mwaka 2009/2010 mradi umekusudia kuziingiza skuli nyengine 48 mpaka pale Skuli zote za msingi Unguja na Pemba zitakapomalizika.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri aliyoeleza juu ya upatikanaji wa vifaa hivi. Katika upatikanaji wa vifaa vilivyoelezwa hapa vikiwemo *CT Scan* je, anategemea kipindi gani kutumika kifaa hiki kwa wagonjwa wetu tuliokuwanao. Vile vile vifaa hivi vina masharti gani ya kutumia vifaa hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, vifaa vyote hivi nilivyovitaja katika jibu mama tayari hivi sasa vimeshaanza kutumika na vinafanya kazi. Vile vile kuhusu masharti mpaka sasa hakuna masharti yoyote yanayomhusu mgonjwa, sharti liliopo ni kwamba daktari akihisi mgonjwa ana tatizo la kutaka kupimwa kupitia vipimo vyetu hivi, basi lazima daktari amwandikie, hayo ndio masharti yetu. Mtu hawezi kukurupuka tu kwenda moja kwa moja, lakini masharti mengine hakuna Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Katika swali la msingi kuna watoto ambao ni wagonjwa na inabidi kusafirishwa nje kwa ajili ya matibabu. Je, ni utaratibu upi unaotumika kwa ajili ya watoto hao walio chini ya umri wa mika 10 ambapo inabidi mtoto huyo kusafiri kwake mpaka asafiri na mama yake kwa ajili ya kuhitaji usaidizi wa mama yake.

Mhe. Spika, kwa sababu jana nilimkuta mtu kaambiwa anatakiwa kwenda India na atafute nauli ya kwendea serikali imsaidie nauli ya kurudia. Je, kufanya hivi serikali haioni kwamba ni kumbebesha mtu mzigo ambao hauwezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, utaratibu unaotumika ni ule ule wa kuhudumiwa mgonjwa aliyekuwa chini ya miaka kumi pamoja na mama yake, lakini kama Mheshimiwa anasema yuko mama

aliyemkuta analalamika, basi aje afisini tutaona cha kufanya, lakini kwa kweli utaratibu anakwenda mama na mtoto.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ilitangazwa afya bila ya malipo, lakini kwa kuwa hivi sasa tunaingia karne nyengine kuna utaratibu wa kuchangia na kwa kuwa *CT Scan* ili iendelee inahitajika kuchangia. Hivyo mgonjwa atahitajika achangie kiasi gani ili apate tiba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa *CT Scan* kiwango kinachohitajika kuchangia ni shilingi laki moja, lakini hata hivyo, kama kuna tatizo lolote kama tunavyosema kuwa mgonjwa hatoachwa kutibiwa, hatoachwa kupimwa wala kuhudumiwa kwa kuwa hana pesa hizo, tunao utaratibu wetu kwa wale watu ambao hawana uwezo.

Nam. 9

Kukamatwa kwa Meli ya Kigeni

Mhe. Ali Abdalla Ali – Alijibu**:-**

Mnamo mwezi wa Machi, 2009 katika maeneo ya Bahari Kuu ya Tanzania ilikamatwa meli ya uvuvi ya Kigeni iliyokuwa ikivua samaki bila ya kibali. Wahusika wa suala hilo wasiopunguwa kumi walipandishwa Mahakamani na kushitakiwa, na Mahakama iliamuru samaki wote waliovuliwa wauzwe ili wasiharibike.

(a) Je, Mhe. Waziri meli ngapi za kigeni kwa mwaka 2008-9 zilikamatwa zikivua kinyume cha Sheria.

(b) Kunauvumi kuwa, meli hiyo iliyokamatwa na samaki kuuzwa ilikua ikivua katika maeneo ya Bahari ya Zanzibar, Je, Mhe. Waziri suala hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itachukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nam 9 lenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu maswali yake naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Meli iliyokamatwa tarehe 08 Machi, 2009 ilikuwa na jumla ya wafanyakazi (Raia wa Kigeni 37). Baada ya meli hiyo kukamatwa, kesi ilipelekwa katika Mahakama ya Hakimu Mkaazi Kisutu ambapo baadae ilihamishiwa Mahakama Kuu, hivyo bado Mahakama Kuu haijafikia uamuzi wa mwisho na kutoa hukumu yoyote kwa raia hao waliokamatwa na kwa samaki waliomo katika meli hiyo. Aidha, napenda kwa mara nyengine kusisitiza kuwa eneo la ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

a) Katika mwaka 2008-2009 jumla ya Meli 69 za kigeni zilikata leseni kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuvua katika maeneo ya Bahari Kuu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kweli kuwa meli ya uvuvi ijulikanayo kwa jina la Tawaariq ilikamatwa kama taarifa yangu ya ufafanuzi ilivyoeleza.

b) Eneo la Bahari Kuu ni sehemu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria nambari 3 ya mwaka 1989. Hivyo suala hili linashughulikiwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

c) Kama Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania itashinda kesi ilioko Mahakamani, Zanzibar itafaidika kutokana na mgawano wa mapato kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nakubaliana kwamba Bahari Kuu ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwa kuwa na sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahusika moja kwa moja na lolote linalotokea katika mambo haya.

Je, katika kukamatwa hawa wavuvi haramu katika eneo hili na kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano ambao tumeunganishwa katika Bahari Kuu, Zanzibar imeshirikishwa vipi ili kujua kinachoendelea na kupata haki yetu tusije tukaikosa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu mama kwamba suala hili la meli iliyokamatwa bado lipo Mahakamani, lakini pale kesi itakapomalizika kama nilivyosema Zanzibar nayo itafaidika kutokana na mgao wowote utaojitokeza pindipo kesi hii tukishinda. Katika suala hili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalijua kupitia Idara ya Uvuvi, kila linalofanyika kule Mahakamani kuna Maafisa wetu wanafuatilia kwa pamoja. Kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Zanzibar na Tanganyika kwa hivyo tuko sote.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa meli hii ilikamatwa na tani nyingi za samaki na kwa kuwa samaki hawa wameshauzwa na fedha imeshapatikana mkononi.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata fedha zake kiasi gani kutokana na samaki hawa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza walitaka kuuzwa hawa samaki, lakini ikaonekana mauzo hayo ni kinyume na utaratibu wa kisheria. Kwa hivyo, mauzaji hayo yalizuwiwa na mpaka leo bado samaki hawa hawajauzwa na kesi kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba iko Mahakama Kuu inangojea uamuzi. Ahsante sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mahakama ilizuia kuuzwa samaki hawa ambao tayari uamuzi ulikwishatolewa kuuzwa. Iwapo Mahakama itaamuru samaki hawa sasa wauzwe je, Mhe. Waziri anatuhakikishia kwamba baadhi ya mauzo haya yatafanyika katika soko hili la Darajani pengine hata Mkoani na Chake-Chake au sisi tutafaidika katika fedha tu, lakini *nutrition* itakwenda Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, suala la kuuza samaki Mahakama ikiamua yaani kesi yetu tukishinda nafikiri haitokatazwa kuuziwa mtu yeyote watauziwa wafanyabiashara wowote hata awe anatoka Chonga na sehemu nyengine yoyote ya Kisiwa hiki.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe leo tulikubaliana baada ya hoja kuungwa mkono tangu tarehe 17 Juni, 2009 kwamba tuanze mjadala leo. Kwa sababu hiyo na kwa maana hiyo namkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeiviti kutoa hotuba yake.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena katika shughuli ya kawaida ya kila mwaka ya kujadili Bajeti ya Serikali katika hali ya afya njema.

Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuniruhusu kuchangia bajeti hii nikiwa mtu wa kwanza, kwa niaba ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha unaoendelea Baraza la Wawakilishi limeondokewa na wajumbe wawili. Kwanza Marehemu Mheshimiwa Daud Hassan Daud aliyefariki siku ya Ijumaa ya tarehe 19 Disemba 2008 na baadae Marehemu Mheshimiwa Soud Yussuf Mgeni aliyefariki siku ya Ijumaa ya tarehe 22 Mei, 2009.

Waheshimiwa hawa walikuwa wenzetu na tulishirikiana nao kikamilifu katika Baraza na kazi za kijamii. Hivyo, kuondoka kwao kumeacha majonzi kwetu sisi tuliobaki. Hata hivyo, hatuna la kufanya kwa kuwa hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu na imetokea kwa matakwa yake. Kilichobaki na sisi tuliobaki tujue kwamba mtu yeyote atafikwa na majaaliwa hayo wakati wowote. Kwa hivyo, tujiandae kwa kufanya mambo mema na zaidi tuwaombee marehemu hao Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amin.

Mhe. Spika, vile vile naomba uniruhusu kutoa pole kwa wananchi wote wa Zanzibar waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na tukio la kuungua na kuzama kwa Boti ya Amana Pemba huko Tanga na kuzama kwa Meli ya MV Fatih iliyomilikiwa na Kampuni ya Sea Gull, hapo Bandari ya Malindi, Unguja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira wafiwa pamoja na wale waliopoteza mali zao kutokana na kadhia hii kubwa.

Mhe. Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kwa juhudi kubwa iliyochukua ya kuhakikisha Meli ya MV Fatih inanyanyuliwa haraka iwezekanavyo ili kuokoa maiti na mali zilizokuwa zimefunikwa ndani ya meli hiyo. Pia natoa pongezi zangu za dhati kwa Shirika la Bandari - Zanzibar, Vikosi vyote vya Ulinzi vikiwemo vya SMZ na vile vya SMT, Wafanyakazi wa MV. Ndovu pamoja na wananchi kwa kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo gumu la uokozi.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowapongeza Waandishi wa Vyombo mbali mbali vya Habari kwa kutupatia taarifa kwa hatua mbali mbali zilizokuwa zikifikiwa za uokozi.

Mhe. Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Asha Moh'd Hilal kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni kwa tiketi ya CCM. Ni matumaini yetu kuwa ataziendeleza juhudi zilizoachwa na Marehemu Daud Hassan Daud.

Mhe. Spika, vile vile napenda niwatambue na kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Wenyeviti kwa mashirikiano yao mazuri wakati wa kupitia Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omar Kheri	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	-	Mjumbe
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mjumbe
5. Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej	-	Mjumbe
6. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe Mualikwa wa Heshima
7. Ndg. Mdungi Makame Mdungi	-	Katibu
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa kwa dhati ya moyo wangu kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti na kwa niaba ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wa pande zote mbili (CCM na CUF) kwa sababu maalum naomba nimshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa heshima na busara zake za kuiongoza nchi yetu ya Zanzibar kwa kuheshimu Utawala wa Katiba na Sheria. Mhe. Spika, sio dhambi nikitamka kuwa, Mhe. Dr. Amani Abeid Karume anathamini kazi zinazofanywa na Baraza la Wawakilishi, ikiwa ni pamoja na michango adhimu inayotolewa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, kwa msingi huo tunao wajibu wa kumpongeza sana Dr. Amani Abeid Karume na ninayofuraha ya kusema kifua mbele kwamba, Dr. Karume anatujali na kututhamini sisi na wananchi wenzetu majimboni na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu kutoa shukurani za dhati kwa Kaimu Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ambae pia ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Zanzibar, Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano makubwa waliyotupa wakati wa kuupitia Mpango wa Maendeleo na Bajeti hii tunayoijadili kwenye Kamati ya Wenyeviti. Vile vile, naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa kuleta mbele ya Baraza hili hotuba ambayo inaeleweka vyema, inayobeba matumaini ya kuongeza maisha bora ya wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, matumaini hayo yanatokana na mipango madhubuti iliyomo kwenye bajeti hiyo pamoja na hatua mbali mbali ambazo serikali inakusudia kuzichukua katika mwaka ujao wa fedha zinazolenga kuleta hali nzuri ya maisha kwa wananchi, chini ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA).

UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2008/2009

Mhe. Spika, kamati yangu inaipongeza serikali kwa mafanikio iliyopata katika mwaka wa fedha unaomalizika, kwa kuzipatia taasisi zake mgao mzuri wa fedha za matumizi ya kazi za maendeleo kiasilimia ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo utoaji wa vifungu vya fedha za matumizi ya Taasisi za Serikali ulikuwa mdogo sana katika Bajeti ya Maendeleo. Pamoja na mafanikio hayo, kamati hii inaishauri serikali kuzidisha mkakati wa kukusanya na kukabidhi mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali vya mapato ili bajeti iweze kutekelezeka. Kamati yangu imegundua kuwa kuna vianzio vingi vya mapato ambavyo havijatiliwa mkazo kama vile kushajihisha wananchi kusajili ndoa zao na sio kubaki na karatasi tu inayotolewa na shekhe siku ya ndoa. Vile vile wananchi washajihishwe kuvisajili vifo, majengo, kupunguza bei za makontena yanayoingia Zanzibar ili kuwashajihisha wafanyabiashara kuitumia bandari yetu kikamilifu.

BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amewasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 yenye kauli mbiu Bajeti ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Kuimarisha Kilimo na Utalii. Bajeti hii imelenga kufanikisha malengo ya (MKUZA) pamoja na kukabiliana na misukosuko iliyoshamiri hivi sasa duniani, kama vile matatizo ya kiuchumi yanayotokana na kuyumba kwa masoko ya fedha, upungufu wa chakula duniani, mfumko wa bei, na majanga ya kimaumbile na mengi mengineyo yanayoendelea kutishia au kudumaza uchumi wa nchi nyingi zilizoendelea pamoja na nchi zinazoendelea. Katika kukabiliana na misukosuko hiyo serikali inatarajia kuweka mkazo mkubwa katika shughuli za kilimo na hasa uzalishaji wa mazao ya chakula, kuendeleza ushirikiano na Benki Kuu ya Tanzania katika kudhibiti mzunguko wa fedha pamoja na kuendelea kuimarisha shughuli za bandari, kupitia Mpango wa Maendeleo na Bajeti hii tunayoijadili leo hii.

Mhe. Spika, kasi ya ukuaji kwa sekta ya kilimo imeongezeka kwa asilimia 5.7 kwa mwaka 2008 kutoka ukuaji pungufu wa asilimia 0.4 mwaka 2007. Ukuaji huo kwa mwaka 2008 umechangiwa zaidi na ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa asilimia 6.5, hasa mazao ya biashara kama hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi ilivyobainisha kwenye ukurasa wa 10. Hii ni ishara njema na kamati yangu inaipongeza serikali kwa kuweka sekta hii kuwa ni miongoni mwa sekta kiongozi katika kuchangia ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa, kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Tunayo sababu ya kuamini hivyo kwa kuwa tunayo ardhi nzuri kwa uzalishaji, ingawa si kubwa sana, na tunayo mazao ambayo bado thamani yake kibiashara inaendelea kudumu. Kosa tunalolifanya ni kuacha kuyaendeleza mazao hayo katika kiwango kinachostahiki. Hivi sasa

kuna wimbi kubwa la uangamizaji wa mikarafuu na minazi kwa sababu za kibiashara, ujenzi wa nyumba za makaazi na hata matumizi ya nishati ya kuni.

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imeona kuwa kuna umuhimu katika kuimarisha sekta ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa lengo la kuongeza uzalishaji kwa ajili ya masoko ya ndani na nje. Hali hii itadhibiti mfumko wa bei kutokana na kuwa utegemezi wa uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida kutoka nje kupungua. Kamati yangu inaishauri serikali ichukue juhudi zaidi ili kuimarisha uwekezaji katika kilimo ili kuihuisha sekta ya uzalishaji na kuuweka katika mazingira mazuri uchumi wetu na kuleta maendeleo endelevu kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali inatarajia kutumia asilimia 33 ya bajeti katika kugharamia miundombinu ikiwemo barabara. Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi inaishauri serikali kusimamia na kutekeleza mpango wake wa kuzijenga barabara zote zielekeazo kwenye maeneo ya mahoteli ya utalii na zile zinazoelekea mashambani na vijijini, kwa lengo la kukuza uchumi. Aidha, kamati inashauri kuwekwa mkazo mkubwa katika kuimarisha mkakati wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya miji na vijiji kama vile *Manta Resort Hotel* na kwengineko.

Mhe. Spika, sekta ya benki nayo lazima ichukue nafasi yake kwa kusaidia utoaji wa mitaji kwa wakulima kwa njia ya mikopo, kama inavyofanya kwa wafanyakazi na wafanyabiashara. Hata hivyo, kamati yangu inatoa tahadhari kwamba ni lazima iwepo mipango imara itakayosaidia kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumika kwa uzalishaji na sio kuifanyia shughuli nyengine, ili kufikiwa lengo lililokusudiwa.

Mhe. Spika, sambamba na hayo kamati yangu inaishauri serikali kuimarisha sekta ya viwanda ili sekta ya uzalishaji ipate uhai zaidi. Sekta hii haina budi kupewa kipaumbele na kuwekewa mikakati ya kuikuza, badala ya kuiacha ikue wenyewe, jambo ambalo litachukua muda mrefu sana. Sera zetu za kiuchumi ni lazima ziweke mazingira mazuri ili kuvutia uwekezaji katika viwanda. Pamoja na kuweka vivutio maalum vya kisera. Vile vile, tunaweza kuwashawishi wafanyabiashara wetu wakubwa wawekeze katika viwanda. Katika eneo hili ni vyema wafanyabiashara wa Zanzibar wabadilike; wawekeze katika viwanda ili wazalishe na kusafirisha bidhaa nje badala ya kuagiza nje na kuuza ndani pekee.

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri amebainisha mipango mbali mbali ya serikali katika kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ikiwemo kuanzisha kodi ya ardhi ujenzi unaombatana na mahoteli ya kitalii. Kamati yangu inaunga mkono mpango huo, hata hivyo, inaona kuwa, eneo la

kodi ya pango la ardhi ni eneo muhimu sana hivi sasa kulifanyia marekebisho kwa kiwango cha utozaji kodi. Hivyo, mfano eneo la hekta moja hivi sasa hukodishwa kwa US$ 5,000 kwa mwaka, bei hiyo ni ndogo mno ukilinganisha na thamani ya ardhi hivi sasa. Mhe. Spika, kwa hesabu ya US$ 5,000 kwa kila hekta kwa mwaka ukigawa kwenye hoteli yenye vyumba 50 unapata US$ 100 kwa mwaka na US$ 100 ukigawa kwa siku 30 unapata US$ 3.3 kwa siku, kiwango hiki ni kidogo mno.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo kamati yangu inashauri lisimamiwe vizuri ni mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji. Katika nchi nyingi duniani mapato haya hayapokelewi na kukusanywa na Maafisa wa Uhamiaji *(Immigration Officers)* bali hupokelewa na Taasisi ya Ukusanyaji Kodi, kwa hapa kwetu ni Bodi ya Mapato Zanzibar *(Zanzibar Revenue Board, - ZRB).* Afisa Uhamiaji kazi yao ni kutoa kibali stahiki kinachomruhusu mgeni kuingia au kuishi nchini. Hivyo, si vibaya serikali ikafanya marekebisho haraka iwezekanavyo, ili kodi ya pango la ardhi nayo pamoja na kodi hiyo ya vibali vya uhamiaji ikachangia sana kutunisha Mfuko Mkuu wa Hazina na hatimae Idara ya Hazina itimize wajibu wake wa kugawa kasma za matumizi kama tunavyozipitisha ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Waziri inaonesha kukua kwa uchumi wetu kwa kuongezeka Pato la Taifa kufikia Tsh. 747,950,000/- sawa na asilimia 5.4 kwa mwaka 2008 ikilinganishwa na Tsh. 586,388,000/- kwa mwaka 2007 kwa bei za mwaka husika.

Aidha, pato la mtu binafsi limeongezeka kwa wastani wa asilimia 23.8 kutoka Tsh. 516,000/- ambazo ni sawa na dola za Kimarekani 414 mwaka 2007 na kufikia Tsh. 639,000/- sawa na dola za Kimarekani 534 mwaka 2008. Habari hizi zinaweza kuwa na maana katika hesabu za kiuchumi tu, lakini katika hali halisi ya maisha, dola moja ya Kimarekani ni ndogo sana kwa siku.

Kamati hii inaiomba Serikali izidi kuchukua juhudi ili kubadilisha hali hiyo. Bila shaka usimamizi mzuri wa mpango aliouwasilisha Mheshimiwa Waziri utasaidia sana kuleta mabadiliko, na hali bora zaidi ya maisha kwa wananchi.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuwaletea wananchi maendeleo serikali inatarajia kutumia jumla ya Tsh. 239,913 milioni kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo. Bajeti ya kazi za kawaida imepangiwa jumla ya Tsh. 172,692,000/-. Kiwango hiki kinatia moyo ukilinganisha na fedha zilizotolewa mwaka wa fedha 2008/2009. Hata hivyo, bado juhudi zinahitajika ili kufanya uwezekano wa kuwa na bajeti yenye matumizi makubwa zaidi katika kazi za maendeleo kuliko matumizi ya kawaida.

Hapa kamati yangu haina maana kwamba Bajeti ya Kazi za Kawaida ipunguzwe kufidia Bajeti ya Maendeleo, bali iwekwe mikakati ya kukuza uchumi itakayowezesha kufikia malengo hayo kama nilivyoeleza hapo awali. Pamoja na maelezo hayo, kamati yangu inaishauri serikali kuhakikisha kuwa miradi na programu zinazotekelezwa zinatunzwa vizuri ili kuzienzi nguvu za washirika wa maendeleo na nguvu za walipa kodi na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, serikali chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi inasimamia Mpango wa Matumizi Bora ya Fedha za Umma. Mpango huo unalenga kuweka nidhamu katika matumizi ya fedha za serikali, ikiwemo matumizi ya fedha kulingana na bajeti. Kamati inasisitiza kwamba zoezi hilo lisimamiwe vyema na litekelezwe katika ngazi zote za serikali. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inatakiwa iwe mfano wa jambo hilo.

Mhe. Spika, maelezo yangu haya yana sababu ya msingi. Kamati yangu ilipopitia matumizi ya Bajeti Kuu ya Serikali imegundua kuwa fedha za kukabiliana na maafa hazitolewi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na badala yake zinatolewa kwenye vifungu vya Idara ya Kukabiliana na Maafa, kwa kuwa fungu la maafa halijatengwa kama Sheria Nam. 2 ya mwaka 2003 inavyoelekeza.

Kamati hairidhishwi na utaratibu huu na inaishauri serikali itenge fungu maalum la fedha kwa ajili ya shughuli za maafa kama sheria inavyoelekeza, badala ya utaratibu wa sasa wa kuitaka Idara ya Kukabiliana na Maafa itumie fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli nyengine za idara, jambo ambalo linaweza kusababisha idara hii kushindwa kutekeleza majukumu yake mengine ipasavyo.

Mhe. Spika, kamati yangu inaipongeza sana serikali kwa uamuzi wake wa kuyapeleka mafungu ya Afisi Kuu Pemba moja kwa moja, badala ya kupitia Makao Makuu ya Wizara – Unguja. Kamati inaiomba serikali kutekeleza hili kwa moyo mmoja, ili kuondosha usumbufu kwa watendaji, lakini pia utazidisha ufanisi kiutendaji kule Pemba.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa mara nyingi kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kinakuwa na kasoro ya kimahesabu. Jambo hili hupelekea Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupewa karatasi za marekebisho mikononi *(loose paper).*

Hivyo, hupelekea usumbufu wakati wa kujadili na kupitia vifungu; lakini pia linaashiria kutokuwa makini kwa watendaji wanaoshughulikia masuala haya pamoja na kuisababishia serikali kupoteza fedha nyingi kwa jambo ambalo ufanisi wake haukuridhisha. Ili kuondosha tatizo hili kwa miaka ijayo, kamati yangu inaishauri Wizara ya Fedha na Uchumi kufanya maandalizi ya bajeti mapema ili kuiwezesha idara inayohusika kusawazisha matatizo ya maandishi na mahesabu katika kitabu hicho kabla ya kufikishwa mbele ya kamati na wakati huo huo kunusuru matumizi ya Fedha za Umma yanayotokana na kazi ya kusahihisha kitabu hicho.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri serikali inatarajia kuimarisha huduma za elimu na mkazo zaidi ukiwa katika kujenga uwezo wa kitaasisi na watumishi. Kamati yangu inalipongeza suala hili. Hata hivyo, Kamati inaishauri serikali itoe nafasi za masomo zaidi kwa walimu wa sayansi ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi. Aidha, kamati inaishauri serikali iweke mkakati maalum wa kuwa na mkataba kwa kuwataka wafanyakazi wanaodhaminiwa na serikali wanaporudi masomoni wafanye kazi angalau miaka mitatu kabla ya kuruhusiwa kuhama kutoka Taasisi za Serikali na kwenda Taasisi za Binafsi au nyenginezo, ili kupunguza tatizo la upungufu wa wataalam hasa walimu.

Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar inaipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kuwalipa wastaafu mafao yao kwa asilimia kubwa na kuahidi kulipa deni lililobaki la miezi miwili mara tu taratibu za uhakiki wa malipo zitakapokamilika. Kamati hii inaishauri serikali kukamilisha taratibu hizo haraka iwezekanavyo ili kuondosha usumbufu kwa wastaafu hao. Aidha, kamati inaishauri serikali kutowarudisha kazini kwa ajira ya mkataba *(contract)* wafanyakazi wanaostaafu pasipo na haja ya dharura, ili kutoa nafasi za ajira kwa vijana wanaomaliza masomo ambao wapo wengi sana hivi sasa.

Mhe. Spika, kamati yangu inaishauri serikali kutokuwashirikisha Makatibu Wakuu waliostaafu kwenye vikao vya Makatibu Wakuu pasipo na sababu za msingi kwa kuwa yale mambo yanayoamuliwa humo hawatoyafanyia kazi wao kama wastaafu. Pia, inawafanya makatibu waliopo madarakani kutokuwa na uhuru wa kutoa michango yao ipasavyo. Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti imebaini kuwa marekebisho ya maslahi ya watendaji na wafanyakazi wa serikali yamefanywa bila ya kuwepo kwa sera madhubuti ya utumishi. Kamati ya Wenyeviti imeona ni vyema utaratibu wa kuandaa sera ungekamilika kwanza halafu ndipo mambo ya maslahi yakarekebishwa kwa nchi nzima na sio vyenginevyo. Mhe. Spika, mfumo ninaozungumzia ni ule wa *payment consolidation salary* ambao umefanywa bila ya kuzingatia kuwepo kwa sera madhubuti.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake ameeleza mpango wa serikali wa kuwaongezea mishahara wafanyakazi wake kutoka Tsh. 80,000/- kufikia Tsh. 100,000/- kwa mwezi. Hii ni hatua nzuri katika kuwapunguzia mzigo na ugumu wa maisha wafanyakazi, lakini kiwango hiki bado hakikidhi mahitaji halisi ya maisha. Tunaipongeza serikali kwa hatua hiyo. Hata hivyo, kamati yangu inaishauri serikali kudhibiti mfumko wa bei ijapokuwa tupo katika biashara huria, lakini serikali ina uwezo wa kudhibiti hili kama inavyoonekana hivi sasa kwamba bei ya bidhaa muhimu za vyakula zimeshuka na kuleta unafuu kwa wananchi. Jambo hili ni zuri na inatupasa kuipongeza serikali na wafanyabiashara wa Zanzibar.

Mhe. Spika, utamaduni ulioanzishwa na serikali wa kukaa pamoja na wafanyabiashara ni mzuri mno na utaisaidia sana Zanzibar kuondokana na dhana ya kuonana maadui kati ya serikali kupitia Taasisi za Kodi na Wafanyabiashara. Hivyo, ni vyema jambo hili likaendelezwa kwa maslahi ya nchi yetu.

MSAADA WA KIBAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 52 Mhe. Waziri ameeleza kuwa katika mwaka ujao Serikali ya Zanzibar itafaidika kupata asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kutokana na mikopo *(GBS)* tokea kuanza Tanzania kufaidika na mikopo hiyo kati ya mwaka 2003/2004. Kamati ya Wenyeviti imefarajika sana kwa tamko hili. Hata hivyo, kamati yangu inaona kiwango hicho ni kidogo sana. Hivyo, inaishauri serikali kuhakikisha kuwa kima hicho kinaongezwa. Kwa msingi huo, kamati yangu inashauri kasi ya kupitia mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, inahitajika kuwekwa wazi na kuletwa hapa Barazani ili Wawakilishi wa Wananchi nao watoe maoni yao kuhusu kiwango cha mgao wa 4.5.

CHANGAMOTO KWENYE BAJETI YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, wapo watu wengi wenye dhana ya kwamba Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010 ni bajeti tegemezi kwa kiasi kikubwa kwa namna moja au nyengine. Dhana hiyo nakubaliana nayo, lakini hebu tujiulize ni nchi gani duniani iliyoendelea ambayo haikupitia katika mchakato wa kutokuwa na bajeti tegemezi?

Mhe. Spika, katika sekta ya uchumi wataalamu waliobobea katika mambo ya uchumi wana neno la kigeni wanalolitumia nalo ni *comparative advantage*. Sasa hapo nadhani tunaweza tukapata jibu kwamba ni bora tuwe na bajeti ambayo sio tegemezi, lakini haileti majibu katika kuleta maendeleo ya kweli

kwa wananchi au ni vyema tuwe na bajeti tegemezi ambayo italeta majibu ya mafanikio ya kuleta maendeleo na kukuza uchumi wetu?

Mhe. Spika, kwa msingi huo, bajeti hii ya mwaka 2009/2010 kama kauli mbiu yake inavyosema kuwa Bajeti ya Miundombinu kwa Kuimarisha Kilimo na Utalii. Kauli mbiu hii ni majibu tosha ya kufuata barabara ile ya dhana ya kupunguza umasikini tufikapo mwaka 2020. Kwa msingi huo ni dhahiri kwamba mwaka 2020 hakuna miundombinu itakayokuwa haijakamilika na kama hivyo ndivyo ni dhahiri kwamba kwa kuwa uchumi wetu ni mchanga ni lazima tuaminiwe ili tukopesheke na pia tujisaidie ili tusaidiwe.

Mhe. Spika, nasema haya tukiamini kuwa aliyemaskini kama Zanzibar ndie anayestahiki pekee kukopa au kusaidiwa na aliyetajiri kama walivyo matajiri duniani hawastahiki kukopa wala kusaidiwa. Naomba tubadilike kwa hili. Katika misukosuko ya uchumi iliyoikumba dunia hivi sasa tumepata kusoma au kusikia makala mbali mbali zinazoonesha kwamba taifa moja kubwa duniani linadaiwa kiasi trilioni moja na taifa jengine. Hivyo, dhana ya kuwa na bajeti tegemezi ni mfumo na utaratibu tu wa kufikia malengo uliyokusudia kuyafikia kwa maslahi ya nchi yako.

Mwisho, katika hotuba yangu nimehimiza sana Taasisi za Serikali kusimamia mapato yatokana na vianzio mbali mbali vilivyopo kisheria, lakini wananchi tulio wengi hatuwajibiki katika kuisaidia serikali kwenye sekta hii ya ukusanyaji wa mapato.

Hivyo, kuanzia sasa kila mmoja wetu na kila mwananchi awajibike katika hili. Tuwe na utamaduni wa kudai risiti za kila bidhaa tunayoinunua. Tujiulize tuliomo humu ndani ni wangapi tunadai risiti tunaponunua kilo ya mchele? Tunaweza kuona kilo ya mchele kodi yake ni ndogo, yaani hiyo ndogo ndiyo inayokosesha mapato makubwa serikali. Tusipodai risiti tunapoteza mapato ya serikali na athari yake ni kuinyima serikali uwezo wa kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi wake *(Makofi)*.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha Maoni ya Kamati, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu, ambapo kwa mara ya kwanza nitasema maneno machache kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vile vile ninaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Washirika wa Maendeleo waliochangia kufanikisha maendeleo yaliopatikana katika muda wote wa uongozi wangu hasa kutoka mwaka 2005 hadi leo.

Jimbo la Tumbatu washiriki wenyewe ni Norway waliosaidia Mradi wa Umeme, Marekeni, Japan na Iran waliosaidia Mradi wa Maji, Sweden, *ADB*, *UNDP* waliosaidia Miradi ya Elimu, Ufaransa kwa kusaidia Mradi wa *Maternity Ward* Kisiwani Tumbatu na wengine wote ambao kutokana na muda mdogo sitoweza kuwataja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, siku kama ya leo mwaka jana nilisimama na kuikumbusha serikali juu ya mambo mbali mbali ambayo ilikuwa imeyaahidi kwa wananchi wa Jimbo la Tumbatu. Leo hii ninayofuraha ya kusema kwamba ninaishukuru sana serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwa yale yote ambayo serikali imeyakamilisha na inaendelea kuyakamilisha *(Makofi)*.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii kuikumbusha tena serikali kwamba katika bajeti ya mwaka jana, serikali ilitenga jumla ya shilingi 250 milioni kwa ajili ya ujenzi wa barabara Pale Kiongele hadi Mkwajuni. Kwa sababu ya ratiba ya ukamilishaji wa barabara ya Mshelishelini Pwani Mchangani, ujenzi wa barabara ya Pale Kiongele hadi Mkwajuni haukufanyika.

Imani yangu kuwa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuwa mwaka huu wa fedha barabara hii itajengwa na hasa kwa vile barabara ya Mshelishelini Pwani Mchangani itakuwa imekamilika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba uniruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini, pia nikushukuru wewe kwa mara ya pili kwa kuniruhusu kutumia muda mrefu kiasi, katika kuwasilisha maoni ya Kamati yangu pamoja na ya Jimbo langu.

Mhe. Spika, napenda kutamka tena kwa niaba ya Kamati yangu na Jimbo langu, ninaiunga mkono Bajeti hii Kuu ya Serikali ya mwaka wa fedha 2009/2010 kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana *(Makofi)*.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha): Mhe. Spika, nakupongeza kwa kunipa nafasi hii na pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kwa namana alivyowasilisha hotuba yake juzi *(Makofi)*.

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima unaotuwezesha kujadili matatizo yetu. Ninamuomba azielekeze nia zetu, ili yatayojadiliwa yawezeshe kuiondoa nchi yetu kutokana na umaskini, unyonge

na maradhi ili Zanzibar ipige hatua ya kweli katika ustawi wa uchumi utao imarisha ajira, kipato, biashara, ukuaji wa mitaji na raslimali na hatimae ujenzi wa miundo mbinu bila ya kutegemea ufadhili na ombaomba unaopunguza heshima na uhuru wetu.

Naomba uniruhusu niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu kwao.

Mhe. Spika, mwaka jana katika kikao kama hichi, tulikuwa nao wenzetu Marehemu Daud Hassan Daud na Marehemu Soud Yusuf Mgeni, tuwaombee maghfira na Mwenyezi Mungu aziweke roho zao peponi Amin. Aidha na mimi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti naomba niwape pole wananchi mbali mbali wa Zanzibar walioondokewa na jamaa zao katika matukio tofauti, lakini hasa katika Ajali ya Kuzama kwa Marekebu ya M.V. Amana iliyouwa watu wasiojulikana na pia ajali ya meli M.V Fatih iliyozama chini ya miguu ya Mamlaka ya Utawala na kuua idadi ya watu inayobishaniwa.

Ajali hizi na nyengine zilizotokea kabla inadhihirisha kuwepo ufa mkubwa katika Sera na Uongozi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafiri, Kambi ya Upinzani inahimiza hatua za kuwajibika kwa wanaohusika.

Mhe. Spika, hii ni bajeti ya tisa katika awamu hii ya sita, iliyofuatiliwa na bajeti tano za awamu ya tano, zote zikiongozwa na CCM. Sisi wajumbe wa Baraza lako tumezoelea kusikia misamiati mingi iliyotutumainisha kwamba safari ya kuelekea nchi ya ahadi kiuchumi iko karibu, tuliwahi kusikia:

- *Rolling Plan and Forward Budget,*
- Dira 2020 na Mkuza
- Klasta *Programme* na miradi
- *B. O. T, World Bank and IMF*
- Mabilioni ya J. K. na A. K

Pamoja na misamiati yote hio na mengine mingi hali za wananchi wetu zinaendelea kuwa ngumu na ukali wa maisha unashamiri, kiasi ya kwamba asilimia kubwa ya Wazanzibar wamekuwa wahitaji au omba omba, ili waweze kumudu gharama za msingi za maisha kwa siku chakula, mavazi na pakulala. Kama hawaombi hapa ndani wanaomba kwa jamaa zao walioko nje.

MKUZA

Mhe. Spika, serikali ilitangaza mpango wa MKUZA, ili isaidie kuondoa umaskini wa kipato na kwamba pamoja na malengo mengine MKUZA, uliazimia mambo yafuatayo:-

1 Kuinua kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa na kufikia asilimia 8 – 10 mwaka 2010.

2 Kupunguza kasi ya mfunuko wa bei na kufikia chini ya 8% ifikapo mwaka 2010.

Katika kufanya tathmini ya bajeti hii, ni vyema tukubali kwamba MKUZA umefeli, umaskini wa kipato umeotai na kiwango cha ukuaji wa pato la Taifa ni 5.4% badala ya 10% na mfunuko wa bei unakaribia 24% badala ya 8%.

Mhe. Spika, katika usimamizi wa MKUZA, Kamati za Wataalamu wa Klasta husika ni muhimu sana, hawa husaidia kutathmini utekelezaji na kufanya tathmini ya matumizi *(Public Expenditive Review)*. Kwa maoni yangu kamati hizi hazishirikishwi au zina wataalamu wasio na uwezo, wakati MKUZA II unamalizika kwa kufeli, ni lini wataalamu wa Klasta hizo wamepewa mafunzo ya kufanya tathmini (PR) *(Makofi)*.

Malengo ya Milenia

Mhe. Spika, katika bajeti kama hii ni vyema wananchi wakapatiwa uchambuzi wa kina wa mikakati ya utekelezaji wa malengo yote ya milenia na sio maneno ya jumla jumla tu, katika uchambuzi huo ni vyema wananchi wakaeleweshwa tumefikia wapi, tumebaki wapi na vigezo vinavyotumika katika malengo yote 8.

Kwa mfano, katika lengo la mwanzo kabisa la kuondokana na umaskini na njaa, tungeambiwa kidata ni Wazanzibari asilimia ngapi wanaohusika na lengo hili, wako wapi, kibajeti wameandaliwaje, wanatathminiwaje, na kwa vigezo vipi, na lini lengo hili litafikiwa. Haitoshi serikali kujisifu kwa malengo ya Millenia, lakini kila mwaka habari za Wazanzibari kula mizizi na chochoni zinasikika *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika bajeti zilizotangulia serikali ilikuwa na azma ya kuona kwamba bajeti ya kawaida inakidhiwa na makusanyo ya ndani. Je, tumefikia wapi, kwani katika bajeti hii mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa 159.69 bilioni, huku matumizi ya kawaida yakikadiriwa 172.69 bilioni.

Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana ukurasa 28 para 54, Washirika wa maendeleo walichangia 35.33% ya makadirio ya mwaka kwa kipindi cha miezi tisa, na tuchukulie hadi mwisho wa mwaka watatupatia 40% ya makadirio, maana yake ni kwamba 40% ya 173.752 bilioni ni sawa na 69.5 bilioni kwa mwaka jana.

Sasa ikiwa mwaka jana tulipata 69.5 bilioni ya wahisani badala ya 173.75 bilioni. Je, kigezo gani alichokitumia waziri kueka makadirio ya 199.18 bilioni kutoka mchango wa Wahisani mwaka huu?

Je, kwa swali la hapo juu, mwananchi akiwa na hisia kwamba bajeti hii ina sura ya kutotekelezeka atakuwa amekosea?

Mhe. Spika, serikali imeitangaza bajeti ya mwaka huu kuwa ya kuendeleza miundo mbinu, kwa kuimarisha Kilimo na Utalii. Lakini kiuhalisia maneno yake hayaendani sambamba na Mgao wa Bajeti ya Serikali katika Sekta husika. Wizara ya Miundo mbinu imetengewa 4.49%, Wizara ya Utalii imetengewa 1.49% na Wizara ya Kilimo imetengewa 3.94%. Sasa mafanikio hayo yatapatikanaje, angalia kiambatanisho No. 1 *(Makofi)*.
Kila mwaka Mawaziri wanaosoma bajeti hutupa matumaini kwamba uchumi umekuwa kwa asilimia hii na hile, maendeleo yamekuwa kwa njia hii na hile, pato la mtu binafsi limefurika kwa kiwango hichi na kile, uekezaji raslimali umekuwa kwa bilioni hizi na zile. Lakini mbona takwimu hizo hazileti tafsiri ya kweli katika masuala yafuatayo:-

- Uwezo wa wananchi wetu kutumia na kujikimu, kueka akiba, kulipa kodi na kuekeza raslimali.
- Uwezo wa nchi yetu kukuza ajira, kupunguza urari wa biashara na kutotegemea ufadhili uliokithiri.

Mhe. Spika, naishauri serikali iziorodheshe raslimali zetu na fursa zetu na tutumie vipaji vyetu kuziendeleza kwa maslahi yetu, kwa mtazamo wangu uduni wa uchumi wa Zanzibar unachangiwa na mambo mawili:

(a) Udhaifu wa Sera zinazofuatwa na SMZ na usimamizi duni wa sera hizo.
(b) Mfumo mbaya wa Muungano.

A) UDHAIFU WA SERA NA USIMAMIZI WAKE

Mhe. Spika, katika kusadikisha udhaifu wa Sera katika uchumi wetu na katika maelezo yangu nitajaribu kupitia ahadi za Kibajeti za Mawaziri wetu wa Fedha waliotangulia na waliopo na kuangalia utekelezaji wa ahadi zao pamoja na sera zao.

(i) Ujasiri wa Kuitetea Zanzibar

Mhe. Spika, kwa kuona kwamba kiuchumi Zanzibar inaangamia ndani ya mfumo wa Muungano, viongozi wa wamejaribu kujipapatua katika

makucha hayo, lakini ujasiri umekuwa dhaifu na haukuzaa matunda, kwa mfano na naomba kunukuu:

- "SMT na SMZ zilikuwa na mazungumzo magumu kupitia upya maeneo ya Muungano na kufikia muafaka katika maeneo kadhaa kama vile mfumo wa kifedha, mamlaka ya utozaji kodi na utumishi katika vyombo vya Muungano (Mhe. Amina Salum Ali, Bajeti ya 1996).

- Kuimarisha majadiliano na SMT ili Haki ya Zanziba kwenye mapato ya Muungano ipatikane kikamilifu. (Mhe. Suleiman Othman Nyanga, Bajeti ya 2002)."

Mhe. Spika, nakusudia kueleza kwamba kwa kutumia nukuu za hapo juu na hali ilivyo hivi sasa ni aibu ndani ya miaka 14 Mawaziri wa Serikali 2 za Chama kimoja kujadiliana bila ya kupata ufumbuzi wa maana, iko wapi *Joint Financial Commission*? Kambi ya Upinzani ina wasi wasi kuwepo woga katika mijalada hii kwa upande wetu *(Makofi)*.

(ii) Ajira

Ajira katika nchi huinua kipato, huongeza matumizi, hukuza biashara, huongeza ulipwaji wa kodi na huinua uchumi. Serikali imekuwa ikitupa matumaini ya ajira, lakini hazionekani, na serikali badala ya ku-*review* ahadi na sera zake inabakia mlalamikaji, sasa nani alete ufumbuzi, kwa mfano na naomba kunukuu:

- "Kuongeza Ajira ambapo angalau kwa kila Kaya ya watu watano nafasi moja ya kudumu. Hii maana yake kutengeneza nafasi mpya za kazi zipatazo laki moja (Mhe. Amina Salum Ali, Bajeti ya 1996).

- Kuna ongezeko la vijana wanaomaliza masomo wapatao 15,000 kila mwaka, nafasi za ajira zinazoundwa kila mwaka sio zaidi ya 500. Hii ina maana yake ni kuongezeka kwa wastani wa watu 14,500 wasiokuwa na kazi kila mwaka. Suala la Ajira italishughulikia kwa nguvu zote katika kipindi cha miaka mitano ijayo (Mhe. Suleiman Othman Nyanga, Bajeti ya 2001).

- Licha ya kazi nzuri ya ukuaji wa uchumi ni vizuri kukiri kuwa bado tunakabiliwa na Changamoto kubwa ya kuwapatia wananchi wetu nafasi za kazi. Idadi ya vijana wetu wanaoingia katika soko la Ajira kila mwaka ni kubwa kuliko

uwezo wa uchumi wetu kutengeneza nafasi za Ajira kwa Ajili hio (Dk. Mwinyihaji Makame, Bajeti ya 2005)."

Mhe. Spika, hao ndio watu ambao nchi hii imewapa jukumu la kusimamia Sera itayotoa Ajira. Bahati mbaya wameshindwa kusimamia kuona kwamba Wazanzibari wanapata ajira, kwa ushauri wangu ujenzi wa viwanda vya samaki kwenye angalau kila wilaya pamoja na uvuvi wa bahari kuu ungeleta ajira kubwa, tukajifunze japo hapo Mwanza, viwanda vya minofu ya samaki wa ziwa si wa bahari, vilivyotoa ajira za viwanda na wavuvi.

(iii) Taasisi za Fedha

Mhe. Spika, kuwepo kwa taasisi za kifedha zilizoimara katika nchi zina umuhimu mkubwa katika uekezaji wa raslimali na katika kukuza Ajira kwa wananchi. Vitega uchumi vichache vilivyoekezwa na wageni hapa Zanzibar, mingi ya mitaji yake ni mikopo kutoka Sekta za Fedha za nchi zao.

Mhe. Spika, hapana shaka Wajumbe watakubaliana nami kwamba Sera iliopo ya Taasisi za Fedha inahitaji mapitio. Kambi ya Upinzani inashauri utaratibu uandaliwe na Serikali, ili Mabenki yatoe mikopo kwa Wakulima na Wavuvi wetu na sio wafanyakazi wa Serikali tu.

(v) (a) Kilimo

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi iliyo na ardhi yenye rutuba na mvua ya kutosha kila mwaka. Wazanzibar sio tu tunaagiza mchele lakini hata karoti, mabilingani na nyanya, utadhani Zanzibar ni visiwa vya Jangwa. Zanzibar ilishaanza kupiga hatua ya usafirishaji wa matunda kama embe, takwimu zinataja kwamba usafirishaji wa embe umeshuka kutokana tani 250 mwaka 1993 hadi tani 0 hivi sasa, ukiuliza serikali? Jibu ni ubabaishaji tu.

Sekta ya kilimo inajikongonya katika ukuaji wake, ambao hauwezi kuwaondoa wananchi kutoka katika umaskilini uliokithiri, ambapo idadi ya watu inaongezeka kwa wastani wa asilimia 3.1 kwa mwaka, na mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa, umeshuka kutoka wastani wa asilimia 58 katika miaka ya 60 hadi kufikia wastani wa asilimia 27.3 mwaka 2007.

Kutokana na hali hiyo bado serikali haijazinduka katika kutanabahi kwa kuongeza Bajeti ya Kilimo angalau kufikia asilimia 10, ambayo ndio agizo la Azimio la Maputo, mwaka huu Bajeti ya Wizara ya Kilimo na taasisi zake ni chini ya 4% wakati Bajeti ya Wizara Nchi Tawala za Mikoa na Vikosi vyake ni karibu 10%. Je, sera hizi zitatukwamua? Angalia kiambatanisho No. 1

Mhe. Spika, serikali haina budi kuweka mazingira mazuri ya soko la Mazao, Mikopo kwa wakulima, Uekezaji katika Sekta ya Kilimo, Kilimo cha

Umwagiliaji/Uvunaji Maji ya Mvua na vivutio kwa wafanyakazi ya Sekta ya Kilimo na Uimarishaji wa kweli wa utafiti na kupiga vita wadudu waharibifu wa mazao na matunda.

Kambi ya Upinzani inashauri kwa mwaka huu kutenga Sh. Bilioni 10 katika bajeti ya maendeleo kwa shughuli ya uvunaji maji ya mvua na umwagiliaji, sh. Bilioni 2 ziwe kwa Wilaya ya Micheweni na wilaya zilizobakia zipate sh. Bilioni moja moja isipokuwa Wilaya ya Mjini.

(b) Karafuu

Mhe. Spika, karafuu na Zanzibar ni watoto pacha katika historia na Ustawi, na Uchumi wa Zanzibar ulijengeka kwa uuzaji wa karafuu nje. Sera mbaya zinazofuatwa na serikali imeangusha uzalishaji wa karafuu kutoka tani 24,000 kwa mwaka katika miaka ya 1960 hadi tani baina ya tani 2000 na 3000 miaka hii.

Serikali haina budi kuelewa kwamba zaidi ya 70% ya mikarafuu iliopo ni mikongwe sana na haina budi kueka sera itayosababisha ustawishaji wa mikarafuu mipya. Suala la ubinafsishaji wa zao la karafuu lipatiwe ufumbuzi, katika hili mawaziri wamekuwa wakitoa ahadi nyingi, lakini bado utekelezaji wake hauonekani, kwa mfano na ninanukuu:

- "Aidha serikali itafanyia marakebisho utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa karafuu, wajibu wa *ZSTC* utaainishwa upya na hatua kwa hatua wadau wengine watapata fursa ya ununuzi wa karafuu kwa utaratibu maalum (Mhe. Suleiman Othman. Nyanga Bajeti ya 2003)

- Mapendekezo yanalenga katika kutoa fursa kwa Sekta Binafsi chini ya usimanizi wa Wizara ya Kilimo, kusaidia kutoa huduma kwa mkulima, kusambaza miche ya kutosha, utafiti, kuvuna karafuu na kuuza nje karafuu chini ya Leseni itayotolewa na *ZSTC* (Dk. Mwinyihaji Makame, Bajeti ya 2006)."

Mhe. Spika, tokea ahadi hizo nilizozinukuu zilipoahidiwa hapa Barazani muda mrefu umepita, mikarafuu inaendelea kufa, na baya zaidi wakulima wanazidi kuelemewa na utarabitibu mbovu wa ununuzi uliohodhiwa na *ZSTC*. Shirika hili linakopa benki pesa ya ununuzi wa karafuu, fedha ya Benki ina riba, inayobebwa na Mkulima.

Hayo yakifanyika *ZSTC* inadai serikali kiasi ya 4 bilioni. Kwa tafsiri nyengine serikali ndio inayomfukarisha mkulima wa karafuu, kwa riba na kwa kuuzwa nje katikati ya msimu kwa bei poa.

Wakati Zanzibar ikilitelekeza zao la karafuu, umuhimu wake duniani unashamiri. Ni miaka michache tu iliyopita watafiti wa Chuo Kikuu cha *UAE University* katika Falme za Kiarabu wamegundua kwamba karafuu zina uwezo wa kutibu saratani (kensa). Kiambatanisho No.4 ukurasa wa mwisho kuna tiba nyingi za karafuu Mhe. Spika, uziangalia kwa makini *(Makofi)*.

(c) Ukusanyaji Mapato

Mhe. Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa katika suala hili, nguvu imeonekana kukamua wale walio taabani mfano kwenye maduka na Taxi/magari. Lakini kumeonekana mwanya wa upotevu wa fedha nyingi kwenye kodi za Sekta ya Utalii na kwenye uingizaji wa bidhaa bandarini, ambako misamaha ya kodi ya Taasisi na '*underdeclaration'* kwenye bidhaa zinazoingia ni suala linalohitaji kuangaliwa sana, kabla halijatukosesha mapato ya mabilioni ya shilingi. Taasisi za *ZRB* na *TRA* Zanzibar ziwe makini.

Udhaifu mwengine wa ukusanyaji wa mapato ni kutoa malengo ya Jumla kwa Taasisi za Ukusanyaji, badala ya kuweka malengo kwenye vyanzo vyenyewe vya Mapato. Kwa mfano, Haielezwi Malengo ya Mapato kutoka Bandari au Zanzibar *Airport*, Hoteli za Kitalii au Kodi za Mafuta na kadhalika. Suala hili ni muhimu sana kwani tutaweza kuelewa mwenendo wa mapato kutoka kila chanzo na hivyo kupata kipimo cha kupanda, kushuka au ubadhirifu.

(d) Mwani

Mhe. Spika, zao jengine ambalo serikali ina wajibu wa kulifanyia kazi kitaalamu, kimafunzo, kisoko na kibei ni mwani, ili kuondoa umaskini wa kinamana wetu.

Serikali haina budi kusaka fursa za uekezaji wa Viwanda Vidogo vya Usarifu wa Mwani, ili kuona kwamba tija zaidi inapatikana.

(e) Biashara

Jambo jengine linaloitambulisha Zanzibar kihistoria ni suala la Biashara. Zanzibar ulikuwa Mlango Mkuu wa Bidhaa za Afrika Mashariki na Kati na bado penye sera mzuri, mikakati na usimamizi madhubiti, Zanzibar inayo fursa ya kuwa Dubai ya Afrika. Panahitajika umakini na kuondoa woga katika kufikia huko, sio kuuliza kwa wengine, tufanye au mwasemaje? au tusibiri vikao vya kero za Muungano. Lazima serikali ibadilike, iwaenzi wafanyabiashara wetu, iwashirikishe, iwatetee, iwalinde, iwasaidie *(Makofi)*.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa na matatizo mengi na serikali haijachukua hatua madhubuti za kuwasaidia, matokeo yake ni kuongezeka urari wa biashara kila mwaka baina ya Zanzibar na nchi na nje. Katika suala hii serikali ya awamu ya tano ilijaribu kidogo, kwa mfano na nanukuu:-

> ➢ "Hivi sasa biashara kwa jumla imepungua kutokana na matatizo wanayopata wafanyabiashara wetu wanapouza bidhaa zao Tanzania Bara. Pamoja na matatizo hayo serikali inaangalia motisha ya pamoja kuwapa wafanyabiashara, ili wafanye biashara na sio tu na Tanzania Bara bali wa hata na nchi za jirani. Vile vile itashughulikia suala la Wafanyabiashara, ili kuondoa usumbufu wanaopata katika Bandari za Tanzania Bara (Mhe. Amina Salum Ali, Bajeti ya 1996)."

Mhe. Spika, juhudi hizo zilizochukuliwa enzi zile zilisaidia kidogo, ndio maana wafanyabiashara sio wabara tu hata wa nchi za jirani walijazana katika mitaa ya Zanzibar kwenye Migahawa, kwenye Mahoteli ya kulala wageni, na kusababisha "*Economic Multiplying Effect*" kwa wenye *Taxi*, Daladala, Mikokoteni, Wauza Chips, Makuli na wengineo, wako wapi leo? Hawaji tena Zanzibar sasa wanaishia Dar es salaam.

Haya ni matokeo ya sera zinazoyumba, Kambi ya Upinzani inashauri tutanabahi, nchi inaangamia, haitoshi wala haisaidii viongozi wa serikali kukosa uamuzi, kwa mfano na ninanukuu:

Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba kweli tuna matatizo na *TRA* na wafanyabiashara wetu, kila tukijitahidi serikali kuwatetea bado *TRA* inawabughudhi hasa Dar es Salaam. Tumefanya mazungumzo mengi hata katika Vikao vya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu kujaribu kutafuta suluhisho. Tunajaribu, tunakwenda tunakubaliana mezani na wakuu wao wanakiri, lakini wale watendaji tumegundua kuwa ndio wakorofi.

Sasa tunakuja na mkakati mpya alivyosema kwamba tubadilishe sera, basi sera yenyewe sasa tunataka kushauri kwamba wale watendaji wakorofi tuwachukulie hatua zinazofaa. Kwa sababu imekuwa zaidi ni utashi wa watu kuliko sera yenyewe ya serikali, hawaambiwi.

Kwani vima vya kodi ni hivyo hivyo na shirika ni hilo hilo kwa nini huku wawe hivi na kule wawe vyengine. Kwa hivyo tumegundua ni ukorofi wa baadhi ya watu tu."(Dk. Mwinyihaji Makame majibu ya swali No. 58 tarehe 31st March 2009)" *(Makofi).*

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi, viongozi wasituangushe, tatizo sio waliochini, nadhani ni hao munaojadiliana nao.

(f) Ukusanyaji Takwimu

Mhe. Spika, usahihi wa Ukusanyaji wa Takwimu mbali mbali katika nchi ni jambo muhimu sana, kwani ni katika matumizi yake ndio nchi hupata viwango sahihi vya viashiria vya uchumi wake, mimi natilia shaka usahihi wa mfumo wa Ukusanyaji Takwimu kupitia makubu ya Masheha, Masokoni, maskulini, madukani na kwengineko.

Ni kweli kulifanyika Utafiti wa Matumizi ya Kaya, lakini utafiti huo hautoshi, kuna pia tafiti za sekta isio rasmi, nguvu kazi, Sensa ya Kilimo, Viwanda na nyenginezo, ambazo hutakiwa kufanyika angalau kila baada ya miaka mitano, ili kutoa taswira halisi.

Mhe. Spika, ndio maana huwa tunaambiwa uchumi unakua, huku wananchi wakilia njaa kwenye uchumi unaokuwa. Suala hili liliwahi kumstaajabisha, mchumi mmoja aliposema naomba kunukuuu:

> ➢ "Katika hali ya kawaida, matarajio ya ukuaji wa uchumi wa 4.8% yangetazamiwa kuambatana na ukuaji wa ajira, uwekezaji rasilimali, na ongezeko la wastani wa mapato ya wananchi nchini. Kinyume chake kiwango cha ukuaji wa ajira, uwekezaji rasilimali haikuongezeka pamoja na ukuaji wa uchumi kwa ujumla, hali hio sio ya kawaida (Mhe. Amina Salum Ali, Bajeti ya 1998)."

Mhe. Spika, hali hio iliyomchanganya mchumi ni la ukuaji wa uchumi wa 4.8%. Je, leo waziri nasema mwaka 2008 uchumi umekuwa kwa 5.4%, mchumi huko aliko akisikia atasemaje? Lakujiuliza Je ni takwimu sio sahihi, ni mapishi ya *data* au ni kujifurahisha?

(g) Utalii

Mhe. Spika, SMZ imetangaza kwamba Utalii ndio Sekta Kiongozi. Watalii wanaoingia Zanzibar ni wengi kwa mwaka, kungelikuwa na usimamizi mzuri, kodi hio ya Utalii na kwenye mahoteli yenye nyota tano kungekuwa hakuna sababu ya Zanzibar kuomba. Lakini bahati mbaya hata takwimu sahihi hazitolewi vizuri, angalia kiambatanisho Na.3 mfano wa wenzetu Bara walivyowazi na makini.

Mhe. Spika, wenzetu wa Malaysia wanasimamia vizuri utalii na kwa kweli sio tu wanachangamkia ukusanyaji wa kodi mbali mbali, lakini wanahakikisha wananchi wao wanafaidika na fursa za kiuchumi za kitalii.

Vile vile wamekuwa wakizielekeza bajeti zao kusaidia na kuwakopesha wafugaji, wakulima pamoja na wahudumiaji wao waweze kuzalisha ndani na kukimu matumizi ya Mahoteli na watalii wanaoingia. Kwetu utalii unawanufaisha wakulima na wafugaji wa nje ya Zanzibar.

Kwa kweli kwetu mambo yameachwa holela bila ya udhibiti hadi karibu nusu ya Mji mkongwe umegeuzwa kuwa eneo la uuzaji wa masanamu ya kuchonga nakuchora, halafu wananchi waseme baraka imepotea! itabakia wapi? Lazima utalii wetu usimamiwe, tusipotanabahi tunaelekea pabaya *(Makofi)*.
Mhe. Spika, kufuatia kudorora kwa uchumi duniani, Sekta ya Utalii katika nchi nyengine imeanza kuathirika. Je, serikali imefanya tathmini ya hali hiyo na kuelewa ni kwa kiasi gani tunaweza kuathirika? Pengo la taathira hio litazibwa vipi, na kwa kiasi gani au *risk plan* yetu ni vipi?

Muundo wa Utumishi wa Serikali na Maslahi ya Wafanyakazi
Hali ya Utumishi Serikalini ni jambo linahitaji mageuzi makubwa. Kuna haja kwa serikali kufanya tathmini ya watumishi na utumishi. Kuna wafanyakazi wengi ambao hawana tija serikalini; mfano Uajiri kwenye kikosi cha Valantia na JKU ni mzigo mkubwa bure unaogharimu bajeti ya shilingi 6.16 bilioni mwaka huu.

Kambi ya Upinzani inashauri kufutwa Vikosi vya JKU na Valantia na Kuviimarisha vikosi vya KMKM, Zimamoto na mafunzo kwa vifaa, kielimu na kimaslahi. Kutokana na hali ya mfumuko wa bei ulivyo serikali inashauriwa ipandishe mishahara hadi laki moja na nusu kwa kima cha chini kwa mwezi. Kwa upande wa wastaafu wa kima cha chini kulipwa angalau theluthi moja ya kima cha chini cha mshahara. Ninaishauri serikali sasa kutoa muongozo unaohitajika ili malipo ya wafanyakazi yatolewe kwa kutumia kiashiria cha *Retail price Index (RPI),* ili wafanya kazi wanacholipwa kiweze kukimu hali zao za maisha. *(Makofi)*.

Walemavu
Kwa mujibu wa kumbukumbu nilizozipata kwenye Umoja wa Walemavu Zanzibar kuna Walemavu wa aina mbali mbali wafikao 5,000 ambao watu wazima ni karibu 3,000 na watoto ni kama 2,000, hawa wote wanakabiliwa na makali mazito ya maisha. Kambi ya Upinzani inashauri kuanzishwa ruzuku ya thuluthi (1/3) ya kima cha chini cha Mshahara kwa kila Mlemavu mtu mzima na (1/6) ya kima cha chini cha Mshahara kwa Mlemavu mtoto kwa ajili ya fedha ya matibabu na masomo.

Pemba na Umasikini

Mhe. Spika, Kisiwa cha Pemba kina umaskini mkubwa hata baada ya miaka mingi ya uzalishaji wa karafuu nyingi ambazo hazikuacha athari ya maendeleo ya kiuchumi kwa watu wake. Pamoja na Pemba kujaaliwa ardhi nzuri ya kilimo na jitihada ya watu kujituma kwenye kilimo, bado bajeti ya Kilimo kwao ni haba, miradi ya umwagiliaji maji haijapewa kipaumbele Pemba na miradi ya kilimo inapelekwa kwa kuziba ziba midomo tu, mfano – wilaya kati Unguja yenye wakaazi 62,500 imeekewa bajeti ya *PADEP* kwenye shehia 26 dhidi ya wilaya ya Wete yenye wakaazi 102,500 ilioekewa Bajeti ya *PADEP* kwenye shehia 13 tu, na huku wilaya ya Micheweni inayoongoza kwa umaskini kwenye wilaya ya Zanzibar ikifanyiwa dhihaka kwenye Bajeti ya *PADEP* kwenye shehia zake.

Mhe. Spika, tunaambiwa kwamba ujenzi wa miundo mbinu kama vile barabara ni kichocheo cha uchumi, kambi ya upinzani imekuwa ikiilalamikia serikali kwa namna inavyokinyima kisiwa cha Pemba bajaeti ya Ujenzi wa Barabara kiasi kwamba tangu awamu hii iingie madarakani imejenga zaidi ya 200km za barabara hapa Unguja ambapo Pemba imejenga kiasa ya 60 km tu, ndani yake mukiwa na 30km zilizojengwa na Prismo barabara ya Mkoani –Chake.

Mhe. Spika, katika hali ya kukithiri kwa umaskini Pemba, wananchi wanashindwa kulipwa kodi kwa sababu mfumo wa kimaisha ni wa kujikimu, na kwamba uwezo wa matumizi kwao ni mdogo sana labda kwa waajiriwa wachache kwenye taasisi za serikali. Katika kipindi cha miaka hii mine 2006 - 2009, serikali imetenga karibu sh 69.585 biln tu kama ni bajeti ya kawaida kwa wizara kisiwani pemba. hii ni sawa na 16% ya Bajeti yote ya kawaida ya Serikali kwa miaka hii.

Mhe. Spika, kwa sababu ya umaskini uliokithiri, makushanyo ya kodi kwa *ZRB* kwa Pemba nzima kwa mwaka 2008 yalikuwa 4% ya makusanyo ya *ZRB* kwa Zanzibar, huku Pemba ikiwa na wakaazi karibu 40% ya Wazanzibar. Je serikali basi haikerwi na hali hii?

Mhe. Spika, kambi ya Upinzani inataka serikali kupitia wachumi wake kufikiria aina ya utaratibu wa kuamsha uchumi *(STIMULUS PLAN)* kwa kisiwa cha Pemba ili kuongeza mapato, kuinua utumiaji na hivyo kuwawezesha wananchi wawe walipa kodi katika uchumi wa nchi yao.

Mhe. Spika, jambo jengine linaloiumiza Pemba ni ukosefu wa walimu wa kutosha na pia ukosefu wa Taasisi za Elimu ya juu, na pia huduma duni za Afya, vijana wanaojitayarisha kwa mitihani hufuata Tuition Unguja na Dar es salaam, aidha wagonjwa wengi kila wiki hulazimika kujisafirisha kufuata matibabu nje ya Pemba. Safari hizo zote za elimu na matibabu huwagharimu

sana wananchi kwa kutumia kipato ambacho tayari kwao ni mtihani, serikali unapoiuliza jibu lake rahisi ni kwamba Wapemba hawataki kufanya kazi kwao

Inawezekana uzalendo umewashinda, na Sipeke yao, kuna watu wameuacha uwaziri hapa na ndugu zao walikuwa madaktari wazalendo – wamehajiri wamekimbilia "taa inakong'a"

Mhe. Spika, Mikoa ya Lindi na Mtwara ilikuwa na umaskini kama ulioko Pemba na Wafanyakazi wengi hawakutaka kufanya kazi huko, utawala wa Mwalim Nyerere ulipanga vivutio maalum vya kifedha vilivyowafanya hata wachaga achilia mbali wamakonde kuridhika kufanya kazi Mtwara, SMZ, inashindwa na nini kufuatanyayo za Baba wa Taifa kwa wafanyakazi wataalamu kufanya kazi Pemba.

Demokrasia

Mhe. Spika, utawala wa kidemokrasia una nafasi kubwa katika kujenga imani *(confidence)* ya wananchi, wafanyabiashara na Waekezaji na katika ukuaji wa Uchumi, Serikali lazima ichukue hatua madhubuti za kuona kwamba uendeshaji wa nchi unafuata misingi ya utawala bora, na haitoshi kutaja dhana ya utawala bora na umoja wa kitaifa, lakini vitendo vikawa ni kinyume chake, kwa mfano na naomba ninukuu.

- Naomba pia nitumie fursa hii kuwaeleza wajumbe wa bara lake tukufu na wananchi kwamba zoezi linaloendelea hivi sasa la Utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi havihusiani kabisa na masuala ya uchaguzi, vitambulisho vya ukaazi ni jambo linalofanywa na nchi nyingi duniani. (Dr. M. H. Makame Bajeti ya June 2005 pg 14 para 18)

- Ni miezi kumi na tano imebakia kabla ya uchaguzi Mkuu (wa 2005) Ningependa kuitumia fursa hii kutoa nasaha kwa vyama vya Siasa, viongozi wa vyama, makundi ya kijamii, na viongozi wa dini zote na wananchi kwa jumla kwamba Taifa lililostarabika, taifa la Kidemokrasia ni lile ambalo linaendesha taratibu zake za kuwapata viongozi kwa njia ya haki, amani na utulivu. (Mhe. S. Oth. Nyanga Bajeti ya Juni 2004 pg 51 par 130)

Mhe. Spika, maneno niliyo nukuu yana kipimo kwa wananchi, ama yake ya Dk. Mwinyi mie nimeyatafsiri yanapingana na uamuzi wa Serikali hii juu ya kitambulisho na Uandikishaji katika Chaguzi, na maneno ya Mhe. Nyanga yanajikanganya, yeye ndie mwenye dhamana ya utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, lakini Wazanzibari wengi wananyimwa, Jee kunyimwa huko ndio kutembea kwenye nasaha zake?

Hili ni jambo zito, na kwa maoni yangu suala hili linaweza kuwa la kimkakati kwa zile zinazojiita kamati za ushindi wa uchaguzi wa 2010. kambi ya upinzani inasikitishwa na njama hii, hivi hadi lini chaguzi zetu zitakuwa za mbinu na ghiliba tu?

Mfumo wa Muungano na Taathira ya Uchumi Wetu

Sisi katika Kambi ya Upinzani ni waumini wa dhati wa Muungano, lakini uwe Muungano wenye HAKI SAWA KWA WOTE, sio Muungano wa Mkoloni na Mtawaliwa.

Mhe. Spika, Muungano kama ulivyo umeiathiri Zanzibar katika Njanja zifuatazo:-

1) Zanzibar imepoteza Udhibiti wa Sera ya Fedha *(monetary Policy)*, sera muhimu katika udhibiti wa Uchumi *(economic regulation).* Mara nyingi Benki kuu ambayo eti ni mali ya SMT na nimshauri tu wa SMZ inapopanga maamuzi ya Udhibiti wa fedha hutumia Viashiria vya Tanzania bara, ikiiwacha Z'bar mbebaji wa taathira zake (mfano hai, kupanda na kushuka kwa thamani ya shillingi ya Tanzania).

   Ninashauri SMZ kujifunza kwa nchi zinazotumia Sarafu moja, mfano EU na Sarafu ya Euro ni vipi katika nchi hizo wanavyodhibiti sera ya Fedha ya sarafu moja bila kuathiri udhibiti wa uchumi wa nchi husika. Hilo ni somo muhimu kwetu tusikokotwe tu.

   Zanzibar imekosa udhibiti mpana wa Sera ya Kodi, au ina udhibiti dhaifu wa uwanja wa kodi *(weak fiscal base).* Katika udhaifu huu Zanzibar inaathirika katika nyanja zifuatazo.

a) **Usawazishaji wa Kodi *(Tariff harmonization)***

Dhana hii imepotoshwa na kuifanya SMZ iamini na ikubali kuwa usawazishaji huo lazima uwe wa viwango sawa. Wenzetu wengine huwa wanasawazisha kodi kwenye taratibu tu *(tax procedures)* sio viwango, na ikibidi na viwango vya kodi vifanyiwe *'hormonization'*, suala la fidia kuwa nchi itayoathirika kiuchumi ni jambo linalojadiliwa kabla. Haiwezekani kwa viongozi wa nchi kukubali kusawazishwa kodi kwa mfumo wa viwango vimoja bila ya kuelewa aina ya fidia nchi yao itayopata. Hata hapa Afrika Mashariki uamuzi wa viwango vimoja vya kodi vya Forodha viliambatana na Nchi za Tanzania na Uganda kutaka fidia ya muda wa miaka mitano ili iweze kujijenga kiuchumi – huu ni

mfano hai. Kambi ya upinzani inaishauri SMZ kufanya mapitio ya suala hii, na kutathmini faida na hasara za uamuzi huu kiuchumi.

b) Malipo ya kodi (Payee) ya Wafanyakazi wa Muungano

Hapa ni eneo jengine ambalo uwanja wa kodi kwa Zanzibar umefinywa na Ndugu zetu. Kinadharia hii ni kodi inayokatwa kwenye mshahara wa mfanyakazi kuchangia huduma za jamii mfanyakazi anazopata katika nchi anayoishi. Wafanyakazi wote wa taasisi za Muungano wanaofanya kazi Zanzibar kodi hii haiingii kwenye hazina ya SMZ, na badala yake hadaa imefanywa ili malipo hayo yaingie hazina Bara, inakisiwa kiasi ya Sh. 7 bilioni kwa mwaka tunazikosa. Hili linahitaji ufumbuzi.

c) Malipo ya Corpotate Taxe

Kuna taasisi nyingi zinazofanya kazi hapa Zanzibar ambazo kodi zao za mashirika hazilipwi, na ambazo kama kodi ya mapato *(Payee)* nazo magube yamefanywa kodi hii zilipwe bara. Inakisiwa karibu sh 2 bilioni kwa mwaka huwa zinakosekana hapa Zanzibar.

d)* Malipo ya Kodi ya kuendeleza Ujuzi *(Skill development levy)

Hii ni kodi inayokatwa kwenye mshahara wa mfanyakazi kwa ajili ya kuendeleza ujuzi kwa mujibu wa sheria tulizozitunga. Wafanyakazi wote wa taasisi za Muungano, kodi hii haipatikani, inakisiwa sh. Bilioni 2 kwa mwaka inakosekana kuingia kwenye hazina ya SMZ.

e) Mapato yasiyo ya kodi ya Taasisi

Wizara na Taasisi nyingi za SMZ na SMT huwa zinautaratibu wa kukusanya mapato ya sio ya kodi *(NonTaxed Revenue).* Utatatibu wa Retention umepangwa kwa Taasisi hio kutumia baadhi ya fedha hizo kwa uendeshaji. Kwa taasisi za SMZ fedha zinazobakia baada ya kuchukua retention yao, huzipeleka hzina ya SMZ kwa uendeshaji wa Serikali, suala lililopo kwa Taasisi za SMT kama vile Uhamiaji, *Tanzania Civil Aviation Authority, Tanzania Communication Regulatory Authority* na nyengine ambazo fedha hizo zinakusanywa hapa Zanzibar baada ya kutoa fedha wanazozihitaji kwa uendeshaji, baka ya fedha hizo zinaingia hazina ipi, inakisiwa karibu sh Bilioni 8 tunazikosa kwa mwaka. Hapa panahitaji ufumbuzi

f) Asilimia 4.5 faida ya BOT na gawio la misaada ya kibajeti

Wanzanzibari wanaamini kwamba katika uanzishwaji wa Benki kuu, nchi hii ina mchango wake wa 11.2% kupitia *E. A. C. B.* Hivyo uhusiano wetu wa kifedha na Tanganyika ni kupitia mtaji wetu wa 11.2% katika uanzishwaji wa *BOT*, na si vyenginevyo, kwa mantiki hii, ugawaji wa Faida ya *BOT* na mikopo/misaada ya kibajeti lazima ujengeke kwenye msingi wa 11.2%.

Tanzania bara ina mikoa 20 na mtu akikubali dhana kwamba Zanzibar ni sawa na mkoa wa 21 wa Tanganyika, maana yake ni kwamba asilimia 100/mikoa 21 = 4.7% kwa kila mkoa Maana yake ni kwamba kila mkoa utapata gawio la *BOT* na misaada ya kibajeti ya 4.7%.

Jee, kigezo cha Zanzibar kuwa mkoa ndicho wenzetu wanachokitumia? Na hata hio 4.7% wamekiona kikubwa ndio wakaamua kutupa 4.5% labda ni kwa sababu ya uhaba wa watu milioni moja tulionao ukilinganisha na mikoa mengine ya bara.

SMZ kuendelea kukubali mgao wa 4.5% ni kuwadhalilisha Wazanzibar, Kambi ya upinzani inatambua 11.2% kuwa ndio gawio halali kwa faida ya *BOT* na misaada na mikopo ya kibajeti na kwa matarajio ya misaada/mikopo ya kibajeti kwa mwaka huu inayokadiriwa kufika 1600 Bilion, 11.2% x 1600 bilioni = 179 Bilioni hiyo ndio haki yetu stahiki.

Mhe. Spika, kuna wengine wanaweza kustaajabia fungu hilo, naomba nieleze kua wakati bajeti yote ya SMZ ni 412.6 Bilion, Bajeti ya Wizara ya Miundo Mbinu ya bara ni 570.53 bilioni, kati ya hizo, zaidi ya 230 bilioni ni fedha za nje, au bajeti ya Wizara ya Afya bara ni 260.6 bilioni, kati ya hizo, zaidi ya 247 bilioni ni fedha za Nje. Zanzibar lazima ipate fungu lake stahili ya fedha za Nje,au irudishiwe *soverenity* yake ili iweze kufaidika na fursa zake.

g) Mapato ya Uvuvi wa bahari kuu

Mhe. Spika, **"Chanzo hichi kinaweza kikaingizia serikali karibu nusu ya Mapato yake".**

(Mh. S. Oth. Nyanga, bajeti ya June 2004 pg. 38 para 101) bahati mbaya SMT imechukua chanzo hichi muhimu cha mapato ya Zanzibar na SMZ imekubali kutoa raslimali hii muhimu, sijui ni kwa kulipa fadhila gani, na **pip**i tuliyopewa kumung'unya eti ni Makao Maku ya Mamlaka itayoanzishwa yatakuwa Zanzibar. Hii haitasaidia, kwa desturi ya wenzetu

wao ndio wataojazana kwenye nafasi nyeti na za maamuzi na sisi hatutajua kinachoingia wala kinachotoka; mfano, Meli zilizokimbizwa zikiiba samaki wetu zinasemekana kukamatwa kwenye Bahari kuu eneo la Zanzibar, na meli iliyoshikwa haikuletwa Zanzibar ilipelekwa Bara, kesi na minada ya samaki inafanyika huko jee tumeshirikishwaje?

h) Ongezeko la idadi ya watu

Ongezeko la idadi ya watu katika nchi ina athari kubwa kiuchumi, idadi ya watu katika nchi huongezeka ama kwa kuzaliwa au kuhamia.

Kwa utaratibu mbovu wa uhamiaji wa wasio wa Zanzibari katika visiwa hivi, haiwezekani kudhibiti idadi ya watu, na hivyo ukuaji wa uchumi wetu ni ndoto. Kuna visiwa vilivyoungana na nchi nyengine au vilivyo sehemu ya nchi nyengine mfano Honkong na China, lakini taratibu za uhamiaji zimeekwa ili kulinda uchumi wa visiwa. Hapa kwetu nadhani ni kwa maslahi ya KURA, ndio wasio Wazanzibari wanaachiwa kuhamia bila ya hesabu maalum, bila ya kujua shughuli gani ya kiuchumi wanafanya. Ninacho kusudia kusema ni kwamba Zanzibar kama visiwa haiwezekanani kujenga uchumi wake kwa kuacha mlango wazi watu wajiingilie watakavyo kama shamba la bibi.

i) Raslimali ya Gesi na Mafuta

Hii ni raslimali ambayo nayo inanyemelewa, napongeza msimamo wa Baraza lako uliotolewa katika kika cha April mwaka huu kuhusiana na suala hili, ila nasikitika kwa mambo mawili:

1 Baadhi yetu wameanza kuyumba kuhusiana na agizo lililotolewa na Baraza hili kuhusiana na suala la Mafuta, eti kuna baadhi yetu wanasema litapelekwa kwenye kikao cha kero ya Muungano, kambi ya Upinzani inasema Agizo la Baraza lako litekelezwe haraka, na Serikali ijue inawajibika kwa chombo hichi.

2 Baadhi ya wanasiasa wanajaribu kuwalaghai Wazanzibari kwamba eti hata hayo mafuta hapana, sawa na iwe hivyo, suala la kujiuliza hiyo hadaa ya kuyafanya kuwa ni ya Muungano ni ya nini kama hayapo, na jee huyo Mshauri Elekezi aliajiriwa kuja elekeza mgao wa mafuta ya Chikichi au ya halizeti, na ile leseni Kampuni ya Canada iliyopewa na SMT bila SMZ kushirikishwa ilikuwa inahusu mafuta ya samaki au vipi, Kambi ya upinzani inaihimiza SMZ

kuchangamkia neema hii ili kuondokana na umaskini wa Wazanzibari.

Mbadala wa bajeti ya serikali

Mhe. Spika, Katika hali tulionayo ya vianzio vya mapato ndani ya Muungano, na katika hali ya matumizi katika nchi yetu, ninawasilisha mbadala wa mapato na matumizi ambayo nimeita **bajeti ya kuibua vyanzo vya mapato na kuzinyanyua hali za wananchi** kama ifuatavyo:

S/N	CHANZO CHA MAPATO	KIMA KINACHOTEGEMEWA	MAELEZO
1	Mapato ya Kodi ZRB	90,000 (85.773)	Ziada ya 4.77bil. itoke katika kudhibiti misamaha ya kuekeza, kodi ya Ardhi, na kutilia mkazo kodi ya Sekta ya Utalii.
2	Mapato ya Kodi TRA	80,000 (63,159)	17 Biloni, udhibiti wa Ukwepaji ushuru wa Forodha, Misamaha ya ushuru na under declaration. VAT ya baadhi ya Mashirika (Bandari)
3	Vyanzo visivyo vya Kodi (SMZ)	15,000 (10.763)	Ziada ni Leseni za bahari kuu
4	In come tax (Payee) wafanyaka zi SMT – Zanzibar	7,000 (0)	
5	Corporate tax Taasisi za SMT – Zanzibar	2,000 (0)	
6	Vyanzo	8,000 (0)	

	visivyo vya kodi (SMT)		
7	Kodi ya kuendeleza Ujuzi wafanyakazi – SMT	2,000 (0)	
8	Leseni ya utafutaji/mafuta	4,000 (0)	
9	Mgao wa faida wa Benki ya Posta	1,000 (0)	Zanzibar n shareholder wa Benki ya Posta
10	11.2% mgao wa BOT	1,200 (500)	4.5 % ya mwaka 2009 = 500 milion,11.2% yake ni 1,200 mil.
	Jumla ya makusanyo ya ndani	**210.2**	
11	11.2% Mgao (wa Misaada) ya Kibajeti (Badget support)	179,000 (50 bilion)	IMF kuipa Tanzania 340 Bilion World bank kuipa Tanzania USD 970 = 1261 Bil. **(1261 + 340) x 11.2% = 179.00 Bilion**
	Jumla ndogo	**389,200**	
12	Washirika wa maendeleo	199,188 40% =79,672.2	Mwaka jana tulipata kama 40% ya lengo
	Jumla kuu	**468,872.2**	

MATUMIZI

S/N	FUNGU LA MATUMIZI	KIMA KITACHOTOLEWA	MAELEZO
1	Mishahara 73,765 - 5.355 (mishahara ya JKU/Volantia) = 68,418 x 1.35	92353.5	Kima cha chini laki moja na nusu (viwango vyengine vya juu viongezeke kwa asilmia stahiki
2.	Matumizi mengine ya wizara 38,942 – 1,346 (OC za JKU/Volantia)	37,596	
3	Mishahara ya Taasisi 9,094 x 1.35	12276.9	
4	Matumizi mengine ya Taasisi	12,073	
5	Mfuko mkuu wa serikali		
	a) Penchen 5.50 x 100%	11,000	Kima cha chini cha Pencheni kiwe 1/3 ya kima cha chini cha mshahara na viwango vyengine viongezeke kwa asilmia stahiki
	b) Kiinua mgongo	6,000	
	c) Malipo ya Riba	2,350	
	d) Malipo ya Deni	15,794(12,794)	Bilioni 3 zaidi za ZSTC zilipwe
	e) Malipo ya wastaafu BLW	3,800	
	f) Gharama za Uchaguzi	2,500	
	g) Matumizi mengine	6,258	
	h) Ruzuku kwa walemavu watu wazima 3000@ 50,000 kwa mwezi x	1,800 (0)	Kupunguza makali ya maisha walemavu

	12		
	i) Ruzuku kwa Walemavu watoto 2000@ 25,000 kwa mwezi x 12	- 0,600 (0)	Fedha ya Dawa walemavu watoto
	Mfuko mkuu wa serikali	50,102	
	Matumizi ya Kawaida	**204,404.4**	**Ni madogo kuliko makusanyo ya ndani**
	Matumizi ya maendeleo, fedha za Ndani	170,240.8	Imeeongezwa 10 bil, za maji ya mvua/umwagiliaji
	Jumla	**374,645.2**	
	Mfuko wa HAZINA	14,584.8	Akiba ya Taifa (hivi sasa hatuambiwi tuna Akiba kiasi gani)
	Matumizi ya Maendeleo fedha za Nje	199,188 40% =79,672.2	Mwaka jana tulipata kama 40% ya mategemeo
	Jumla kuu	**468,872.2**	

Mhe. Spika, nilicho jaribu kuonesha ni kwamba tukiondoa woga na tukijiamini katika kudai haki za Wazanzibar na tukachangamkia vyanzo vya mapato, hakuna sababu ya nchi hii kudumaa hivi,la msingi tudai kilichochetu, raslimali zetu tusizitoe sadaka, na tusikubali kugombanishwa, na nawashauri viongozi wasiukubali kuekewa "*Ceiling*" ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kambi ya Upinzani inasononeshwa na hali za wananchi wetu, nyuso za wananchi wetu zimejikunja kwa unyonge, na wengi wao huamka asubuhi hawajui chai itakuwa nini achilia mbali kijio – hio ni hali ya ufakiri mkubwa, Serikali ilioko madakani ndio masuul wa hali hio kwa kutandika sera madhbuti na usimamizi wake.

Mhe. Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kama kuna yoyote aliyehisi nimemgusa naomba anivumilie, sikukusudia kudhihaki ila ni katika kuoneshana njia. Ninamshukuru sana Mhe. Abubakar, Kiongozi wa Upinzani kwa miongozo anayonipa, na kwa imani aliyonipa na kunichagua nimsaidie katika masuala haya ya uchumi na fedha katika kambi ya upinzani ya baraza lako.

Ninawashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza, na nawaomba waichangie bajeti hii kwa kuonesha njia. Nakushukuru Mhe. Spika. Naomba kuwasilisha

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi ya mwaka 2009/2010.

Pia nikupongeze wewe Mhe. Spika, kwa kuniona kwamba baada ya hotuba ya Mhe. Waziri, Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Waziri kivuli na mimi kupata nafasi hii kama mchangiaji wa mwanzo, bahati nzuri niseme tu kwamba mimi katika wajumbe na Makamo wa wenyeviti kwanza natoa fursa hii kwa kuwa mengi nimeyapitia, hizi changamoto ambazo zinatolewa katika pande zote mbili zitasaidia kuiweka vizuri bajeti yetu ili kuleta manufaa kwa wananchi wetu.

Kwanza naipongeza serikali kwa kuzingatia kwamba hali ya mwananchi wetu wa kima cha chini ni ngumu na pia hali ya maisha imepanda, kiasi kwamba pana haja kwa kila serikali ikipata nguvu iongeze mshahara, naipongeza kwa kutoka shilingi thamanini elfu hadi laki moja na matarajio yangu huko mbele tunakokwendea itakuwa hivyo hivyo, kila ukipatikana uwezo tuongeze posho kwa ajili ya wafanyakazi wetu.

Lakini Mhe. Spika, kidogo nina masikitiko au nina mawazo namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa ongezeko la mshahara ni changamoto kwa wafanya biashara kufanya wanavyotaka, naiomba serikali kwa dhati kabisa kwa kuwa kodi haikuongezeka kwa chakula cha aina yoyote wala kitu chochote katika nchi yetu, basi udhibiti wa changamoto ya wafanyabiashara kuongeza bei kiholela uzuiwe. Serikali ifanye kila uwezo wake kuhakikisha kwamba wafanya biashara wanafanya kazi zao kihalali ili kunusuru jamii yetu hii iliyopata nyongeza hii na wananchi wetu wa kawaida wasiathirike kwa nyongeza hii.

Mhe. Spika, ongezeko lolote lile lina faida yake kwa anayeongezewa, lakini lina athari nyengine kwa yule muongezewa na waliokuwa hawakupata nyongeza ile kwa wananchi wote kwa jumla, namuomba sana Mhe. Waziri, serikali nia yake njema kwa wananchi wake hasa kwa wafanyabiashara ambao wengine hawana uzalendo katika nchi yetu watatumia mwanya huu kuleta hatari kwa kuongeza mambo yao kama wanavyotaka wao ili kuwakomoa wananchi, namwomba sana Mhe. Waziri hili liangaliwe.

Jengine ningetegemea kwamba baada ya kuongezwa nyongeza hii ya mshahara basi na wale wenzetu ambao ni wastaafu nao watizamwe kwa jicho la huruma ili waangaliwe kutokana na hali halisi ya maisha kama tulivyosema mwanzo,

kwamba hali ya maisha imepanda basi na wao pia inawagusa. Namwomba Mhe. Waziri atafute njia yoyote kwa uwezo wake aliokuwa nao na taratibu zake hili likaangaliwa.

Mhe. Spika, nchi yoyote duniani inaendeshwa kwa kodi na mambo mbali mbali ya biashara, mimi niseme tu kwamba ukusanyaji wa mapato ndio roho ya nchi na naamini kama tutakuwa udhibiti katika nyanja hii, basi ukweli utapatikana na mafao mengi yatapatikana ili kuisaidia serikali yetu, kwa hivyo namwomba Mhe. Waziri wenzetu wakusanyaji wa mapato waendelee kufanya kazi zao kwa ufasaha na katika kila sekta iliyohusika.

Hapa kuna maneno mengi ambayo yanazungumzwa kwamba wakusanyaji wa mapato wanakwenda baadhi ya sehemu wakifika kuna mchezo wa hapa na pale huwa unatokea na mapato halali yakakosekana na kuletwa kinyume na utaratibu, namwomba Mhe. Waziri hata kama watalishwa kiapo hawa kuinusuru serikali yetu na nchi yetu, basi wafanyiwe taratibu hizo, lakini mapato yapatikane bila ya kupitia mlango wa nyuma. Mhe. Spika, tunaamini kwamba tuna mambo mengi katika nchi yetu tuna mahoteli na mambo mengi mazuri ya kuanzia vianzio vyetu vya mapato, kama mkakati utakuwa wa halali na utakuwa unafanywa kidhati kabisa, basi naamini mapato ya nchi yataongezeka na itakuwa faraja kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kilimo ni uti wa mgongo na tunazingatia kwamba Zanzibar ni sehemu moja ambayo ijitegemee kujiimarisha katika kilimo, lakini tuamini kwamba ardhi ya Zanzibar ni ndogo kabisa, kwa hivyo mimi wazo langu na ushauri wangu kwa serikali kwamba lazima tuongeze nyenzo za kilimo tuhakikishe wananchi wetu wanapata nyenzo za kufanyia kazi ili kilimo chao kiwe rahisi na uzalishaji uwe mwingi. Kilimo cha kijembe kongoroka kimepitwa na wakati na tukitaka tusitake ili kuongeza tija kwa mkulima, basi nyenzo lazima ziwepo za kutosha pamoja na mbolea ya kutosha ili ongezeko la mazao ya mpunga yawe kwa wingi kabisa.

Lakini pia tuna bahati kwamba sisi katika nchi yetu tuna kilimo kizuri cha mwani na kilimo hiki kimeelekezwa katika sehemu mbali mbali za vijiji vyetu. Wananchi wetu kadhaa, wengi tu hasa kinamama hicho ni kilimo chao kikubwa na kinawapa msukumo wa kujisogezea au kujipunguzia umasikini katika kuzalisha mwani huo na kupata soko zuri ili wauze mali yao na fedha za kutumia wao na jamii yao.

Ningemwomba Mhe. Waziri pamoja na juhudi ya serikali na wafanya biashara hawa wa mwani, bado narudia kauli yangu kwamba bado serikali ifanye kila uwezo na hali yake iliyokuwa nayo kusaidia kutafuta masoko ya kuongeza tija kwa zao hili, bado zao hili liko chini na lina uzito mkubwa zaidi kwa wananchi

wetu. Kwa hivyo ningelimwomba Mhe. Waziri hili aliangalie na tuwe wabunifu kidogo kwa kutafuta masoko mbali mbali ili kuongeza tija kwa mkulima.

Mhe. Spika, bahati nzuri Zanzibar tumezunguukwa na bahari, yaani visiwa vyetu vya Unguja na Pemba hiyo bahari kuu ya Tanzania iko Zanzibar. Bahati nzuri nyenzo za uvuvi au vyombo vya uvuvi imara hatuna kwa hivyo wakati umefika sasa hivi Mhe. Spika, ili kuongeza mapato katika nchi yetu, kuongeza ajira kwa wananchi wetu vyombo vitafutwe katika sehemu mbali mbali na hata ikiombwa misaada si vibaya ili wananchi wetu wapate kuvua katika bahari kuu ambayo itawaletea maendeleo na fedha nyingi katika kuendeleza maisha yao.

Lakini isitoshe baada ya uvuvi tu unakwenda kuvua na kuuza samaki katika mitaa ndio imekwisha, lakini umefika wakati wa kujengwa viwanda vya samaki mara nyingi huwa natoa rai hii kwamba Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vimezungukwa na bahari ni sehemu moja wapo ya rasilimali nzuri tuliyokuwanayo, lakini rasilimali ile hatupati kuitunza na kuifanyia biashara za kutosha kusafirisha nje tunashindwa.

Mhe. Spika, nakumbuka miaka ya nyuma Shirika la Uvuvi walikuwa na mtambo mzuri sana wa kuhifadhi samaki ambapo Serikali ya Ujerumani ilitoa boti ikajenga kiwanda Malindi pale kizuri, ilikuwa mwananchi yeyote wa Zanzibar hawatoki pale, lakini kwa bahati mbaya mradi ule umekufa na tukaambiwa kuna mwekezaji mwengine kapita, lakini hatujui kinachoendelea.

Mimi ningemuomba Mhe. Waziri masuala kama haya yakatafutiwa ufumbuzi ili tuhakikishe kwamba viwanda vile vinatoa ajira kwa wananchi wetu wengi tukizingatia kwamba boti za uvuvi pamoja na kiwanda chenyewe ni sehemu moja wapo ya changamoto la waajiri wetu vijana ambao wametuzunguka katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, utalii ni sehemu moja wapo ya kukuza uchumi wetu katika nchi, lakini sasa hivi kutokana na mtikisiko wa fedha duniani au hali ya uchumi tuna mashaka. Kama taarifa hii ilivyosemwa katika bajeti kwamba watalii wengi watatukimbia kuja katika sehemu zetu. Ombi langu namwomba Mhe. Waziri serikali ijitahidi kutoa kila fani kwa watalii kutembea katika sehemu mbali mbali ili kuitangaza Zanzibar na kuhakikisha kuwa kama kuna kasoro ndogo ndogo zinaondoka ili watalii waje kwa wingi kunusuru uchumi wetu.

Mhe. Spika, tumeshuhudia kwamba vijana wetu wengi wamepata ajira katika sehemu mbali mbali na vijana hao wanaanza kwenye kilimo kwa kupeleka mazao mbali mbali, dada zetu wasusi wa nywele, wapakaji hina na mambo mengine, lakini na vijana wengi wanaotumia viboti ambavyo vipo Malindi na

sehemu nyengine wanapata ajira kubwa sana. Namwomba Mhe. Waziri suala la utalii ni suala muhimu na pia ni changamoto ya uchumi wetu lipewe kipaumbele katika kulishughulikia ili kulinusuru na harakati za mtikisiko wa fedha duniani.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu biashara. Biashara ni sehemu muhimu katika nchi na sio kutoa nje tu kuingiza ndani, lakini na sisi tuwe na tija ya kutoa hapa kusafirisha nje. Kwa hivyo, bado naishauri serikali tuongeze bidii na tuhakikishe kwamba wataalamu wetu sehemu za kilimo na sehemu nyenginezo zinawapa wananchi wetu mafunzo mazuri hasa vijijini kuelimisha wakulima wetu wafanye nini ili waongeze tija yao.

Mhe. Spika, tuna watu wengi ambao ni washauri wazuri wa kilimo, lakini bado kuna manung'uniko ya hapa na pale tunaambiwa kwamba wengi wanabakia maofisini kuliko kutembelea katika maeneo. Mimi nakubaliana na ushauri wa baadhi wa wenzangu kwamba bado serikali ina kila namna kutafuta yale maeneo ya kuanza vitalu vya majaribio, vitalu hivyo vikiwekwa wananchi wetu ni rahisi kwenda kusoma pale na kujua kwamba ukitumia mbolea hii unapata zao hili namna hii haraka. Kwa hivyo, wakati umefika wataalamu wetu watoke katika maofisi na waingie katika maeneo, lakini kubwa linalowashinda nakubaliana na hayo kwamba vitendea kazi hawana. Namwomba Mhe. Waziri wataalamu wetu wa kilimo wapewe nyezo yaani vipando vya kuwawezesha kufika katika maeneo mbali mbali ya kilimo ili kuharakisha kazi za kuleta manufaa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, zao la karafuu nalo ni muhimu na sasa hivi umefika wakati kwamba mikarafuu mingi imekwisha hata ule uzalishani hauna nguvu. Kwa hivyo, sitegemei kama kuna dawa kama vile ilivyokuwa ikifanywa zamani kuwa mti huu unatiwa dawa fulani sijui, lakini dawa yake kata mti panda mti, sisemi kuwa miti ile ikatwe, lakini kwa ile iliyokuwa inaonekana imekwisha basi ni vyema ikaongezwa mikarafuu mingine ili kuleta faida kwa miaka ijayo huko mbele.

Mhe. Spika, Wazanzibari sisi bado ni masikini na tunaamini bajeti yetu inategemea wahisani. Kwa kuwa tumeambiwa katika bajeti hii kwa asilimia kama arubaini na kitu hivi tutategemea wahisani, namwomba Mhe. Waziri bajeti hii iliyoelezwa kwamba tutatumia bilioni mia nne kumi na mbili na kuendelea, lazima tuhakikishe kwamba wahisani waliotuahidi tufanye kila njia, tumalize namna zote, lakini tuhakikishe kwamba fedha hizi zinapatikana ili kunusuru bajeti yetu.

Kama fedha hizi walizoziahidi wahisani zitapatikana naamini Mhe. Spika, bajeti yetu itakwenda sambamba na matarajio ya serikali juu ya kutekeleza ahadi zake ambazo imejiwekea katika bajeti. Kwa hivyo, namwomba Mhe. Waziri tusichoke kulitafutia suala hili la wahisani wetu kulifuatilia kwa hali ya juu.

Mhe. Spika, katika Baraza lililopita nyuma huko nakumbuka tulipitisha mswada unaohusiana na majengo au kodi ya majengo. Mhe. Spika, kwa bahati bajeti hii imeingiza kodi hii ya majengo, ningetoa ushauri kwa Mhe. Waziri kwamba kodi hii sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaifahamu inamlenga nani na kitu gani, lakini wananchi wengi mitaani wameshituka na kusema tunaanza kodi ya majengo itakuwaje, hawaelewi, namwomba Mhe. Waziri akisimama kuja kutoa majumuisho awaeleze wananchi na kuwaelimisha na kujua lengo la kodi hii kwamba inamlenga nani na kwa maana gani. Kwa sababu imeelezwa kwa ufupi katika kitabu hiki, lakini haikueleza kwa urefu madhumuni yake.

Mimi naamini madhumuni yake ni mazuri kama yatasimamiwa na wale watu wetu wanyonge wasiwe na wasi wasi, mimi sitaki kutoa kauli, lakini Mhe. Waziri atakuja kutoa kauli nzuri kwa manufaa ya wananchi wetu. Kwa hivyo, bado tuendelee nayo taarifa hii na kodi hii isimamiwe vizuri itasaidia bajeti yetu kuiweka vizuri katika mapato yake.

Mhe. Spika, nakubaliana kwamba nchi yoyote bila ya miundombinu haina maendeleo, nchi ikiwa na miundombinu basi maendeleo yake yanakua haraka na tutaona tu kwamba mambo mengi yatajitokeza katika maeneo yale. Kwa mfano, barabara mimi nakiri kwamba ni jambo la mwanzo katika nchi linalosaidia katika huduma ya jamii. Pia umeme, maji, halkadhalika katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba pia tunategemea bandari na uwanja wa ndege. Mimi niishukuru sana bajeti hii kwamba hayo yote yameonekana. Kwa hivyo niseme kwamba, changamoro bado iendelee kuhakikisha kiwanja cha ndege cha Zanzibar kinafanyiwa matengenezo mazuri ili kuongeza tija kwa wageni wetu wanaokuja hapa na mapato yanayoongezeka yatasaidia kuendesha nchi yetu.

Mhe. Spika, pia bandari zetu, Bandari ya Malindi ni bandari muhimu sana na niishukuru serikali au wizara kupitia bodi yake ya shirika hili kwamba mkakati wao sasa hivi wanasema madhali bandari imejengwa kazi ziende kirahisi, wametafuta vifaa vya kisasa na juhudi zinakwenda vizuri na bado mategemeo ya bandari yapo ili kuongeza nyezo nyengine ili ufanisi uendelee zaidi.

Mimi naweza kukiri kwamba katika harakati za kazi za bandari yaani upakuzi wa mizigo, basi Zanzibar inaweza kuwa nambari moja kuliko Tanzania Bara

kwa. Hii inadhihirisha kwamba sasa hivi ikiingia meli haitochukua siku mbili, siku ya kwanza kama kuna makontena 400, 700, 800 yatateremshwa meli iondoke ikafanya kazi zake nyengine. Kwa hivyo, hiyo ni faraja kwa upande wetu na kuitangaza bandari yetu kwamba inafanya kazi vizuri na wenye mizigo yao kupitishia hapa ili kuwa na urahisi. Kwa hivyo, naomba serikali ijitahidi kuongeza fedha zaidi baada ya shirika kuomba wakati mwengine ili kuongeza ufanisi wa kazi zake.

Mhe. Spika, tumeshuhudia katika dunia sasa hivi kuna maradhi ya miripuko. Sasa hivi maradhi ambayo yanaleta hofu kubwa katika dunia ni hii *swine flu*. Maradhi haya ni hatari, tuseme mafua ya nguruwe kwa Kiswahili kwa sababu wananchi watakuwa hawafahamu baadhi yao. Mhe. Spika, naomba serikali iangalie sana, haya mapato yetu yote tunategemea kutumia kwa bandari yetu na viwanja vyetu vya ndege. Kwa bahati mbaya hivi sasa katika nchi nne za Afrika zimetangazwa zina mripuko wa maradhi haya Mwenyezi Mungu atunusuru yasiingie kwetu.

Mhe. Spika, ombi langu kwa serikali tujitahidi kujihami, kujihami kwa serikali sio dawa tu, lakini kwa vifaa. Kwa sababu maradhi yoyote ya mripuko yana vifaa vyake ambavyo katika televisheni tunaona, wale wafanyakazi wanajitayarisha vipi na mavazi yao ili kujinusuru na athari ya kuguswa na mtu aliyepatwa na maradhi yale.

Mhe. Spika, tunaamini sasa hivi katika nchi zote duniani na Shirika la Afya Duniani limefanya semina juu ya kuelekeza mambo mbali mbali na kanuni mbali mbali kuwekwa, moja wapo kuhakikisha kwamba katika viwanja vyetu vya ndege na bandari zetu panajengwa vituo vya afya vya dharura. Ningemuomba Mhe. Waziri hili halimo katika bajeti, lakini wahisani wapo na kwa kuwa maradhi haya yanagusa dunia nzima serikali ifanye bidii ya kuomba vituo vya dharura katika maeneo yetu ya bandari na viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, kwa sababu wagonjwa wanaotoka nje anaweza kutokea katika ndege fulani Mwenyezi Mungu atunusuru, lakini akifika pale hatakiwi kuchanganyishwa na wagonjwa wengine katika hospitali zetu, mtu anatengwa katika sehemu hiyo na vifaa vinakuwepo pale vya *checking* ili kunusuru jamii yetu isije ikaambukizwa na maradhi hayo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili suala ni muhimu na sasa hivi Shirika la Afya Duniani limo katika harakati za kuelimisha jamii juu ya tahadhari ya maradhi haya ya miripuko.

Mhe. Spika, si vibaya wafanyakazi wetu ikiwa madaktari au wauguzi wakapatiwa taaluma, mafunzo mbali mbali juu ya kujikinga na kuhami maradhi haya pindi yakitokea, lakini tunamuomba Mwenyezi Mungu yasitokee katika maeneo yetu haya yote.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitalizungumza ni mikakati ya elimu. Elimu ni sehemu moja ya changamoto inayowapa wananchi wetu taarifa mbali mbali, pamoja na juhudi ya serikali bado kuna haja ya kuwaelimisha wananchi wetu kupitia vyombo vya habari hasa ukusanyaji wa mapato waelimishwe wananchi wajue utaratibu gani na kila kitu kwa manufaa ya wananchi wetu na wajue kwamba mlipa kodi humrudia mwenyewe kutokana na manufaa ya ile kodi anayoilipa kutokana na mambo mbali mbali ya utendaji katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, niseme baada ya hayo machache na kwa kuwa mimi ni mmoja katika wenyeviti nikiwa makamo mwenyekiti wa wenyeviti, niseme kwamba hotuba hii naiunga mkono na nawaomba wenzangu wote waichangie vizuri tumuelimishe, tumpe maelekezo Mhe. Waziri na watendaji wake juu ya kufanikisha mapato ya nchi yetu. Penye maelekezo aelekezwe na penye matatizo afahamishwe ili yaje manusura juu ya mambo hayo ya mtikisiko wa fedha usituguse katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema naikubali hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, napenda nikushukuru kwa asubuhi ya leo kunipa nafasi na mimi nizungumzie hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Fedha na Uchumi, kuhusiana na hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, mchango wangu mkubwa utatokana na maoni ya wananchi wangu kwa asilimia 75, na asilimia 25 ndio utakuwa wangu mimi.

Kwanza nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Koani nitoe rambirambi kwa serikali yetu na kwa jamaa wa watu ambao walipata maafa katika kuzama kwa Meli ya MV Fatih hapo Bandarini Malindi. Tunawapa pole na tunawaomba wawe na subira na hii ni moja katika mtihani wa Mwenyezi Mungu na *Inshaallah* atawafariji. Hilo ni la kwanza.

Mhe. Spika, katika hotuba hii ambayo nilikuwa nikichukua maoni takriban kwa wiki mbili kabla ya kusomwa na baada ya kusomwa nimemaliza jana katika Shehia ya Ubago na Kidimni. Yaliyojitokeza nikama ifuatavyo:-

Mambo muhimu ya kilio cha wananchi kwa jimbo langu la Koani ambalo mara nyingi huwa nayatoa hapa bado hayajaoneshwa wazi wazi katika hotuba ya Mhe. Waziri katika vitabu vyake vyote vitatu, vya maendeleo, mwelekeo wa hali ya uchumi na maendeleo kwa mwaka 2007/2008 na huu wa 2009 pamoja

na hotuba yake. Sasa hapo kidogo tumevunjika moyo na maeneo yenyewe kuhusu mambo ya barabara.

Tumezungumza hapa masuala ya miundombinu, utalii, kilimo ndio bajeti hii, lakini Mhe. Waziri bajeti hii haikutaja kuwa itatujengea barabara yetu ya Koani – Jumbi ambayo miaka mitatu nyuma tuliambiwa itakuwemo kwenye *millennium* na baadae mradi huu umekufa, lakini waziri kwa wakati huo alisema ataitia kwenye bajeti zetu za serikali tutajenga sisi wenyewe.

Mhe. Spika, pia kilio cha siku nyingi cha barabara ya Unguja Ukuu – Uzi, wananchi wanapata tabu haimo kwenye bajeti hii.

Vile vile barabara yetu ya Jendele – Unguja Ukuu, lakini pia kwa faida ya wananchi wote barabara ya Mfenesini – Bumbwini humu haimo. Hii ilikuwa inakwenda sambamba na barabara yetu ya Koani – Jumbi ambayo ya jirani yangu. Sasa bajeti hii mimi bado nitakuwa na mashaka kuiunga mkono kwa sababu inatuvunja moyo, inatuvunja moyo kwa matakwa Mhe. Waziri ambayo ameyasema ya kuinua hali ya uchumi kwa nchi hii na wananchi.
Mhe. Spika, barabara niliyoitaja ya Koani – Jumbi ina faida mbili, kwanza faida ya kiuchumi kwa sababu imepita katika maeneo ya ardhi yenye rutuba ya uzalishaji wa matunda pamoja na kilimo cha chakula, kuna mabonde ya mpunga ya mtwango, Pongwe matunda mazuri ya shokishoki, nanasi Ubago, Karafuu pamoja na nazi.

Kwa sehemu ya pili barabara hii ndiko alikozaliwa kiongozi wetu wa nchi alikotoka mzee wake, Mzee Abeid Amani Karume na kumbukumbu ipo. Sasa Mhe. Waziri hata haya mambo mawili hatuyajali na mwaka huu wa 19 niko katika Baraza hili nasikitika sana, lakini nitaendelea kusema bado nina mwaka mmoja wa ishirini na Mwenyezi Mungu anijaalie wanichague tena nitaendelea kudai haki ya barabara hii ya Koani hadi Jumbi itengenezwe. Kwa sababu huko ndiko sehemu aliyotoka muasisi wetu, inakuwaje sasa barabara yenye uchumi na pia imeweka heshima ya nchi yetu ambako muasisi wa taifa hili ametoka.

Vile vile kwani nani hajui kama huyu Rais wetu mama yake anatokea Bumbwini, licha ya mambo ya uchumi, sasa kuweka heshima barabara ya sehemu ambayo mzee wa rais wetu ametokea hatuoni aibu?

Mbali ya hivyo kwa mambo hayo yaliyoelezwa ya utalii Mangapwani kuna beach nzuri. Mhe. Spika, kuna majabali hata Agakhan amejenga maeneo ya kumbukumbu na vivutio vya kiutalii na hii kwa miaka mingi haimo na ilitiwa kwenye mpango na sisi tumezungumza miundombinu au miradi ambayo hatukuweza kupata wahisani, basi sisi wenyewe tutajipiga kifua. Mhe. Waziri hakutaja humu, kataja kwa lugha nyepesi kwamba tutaendelea kutengeneza

barabara hakutaja wapi, ametufunga, lakini hakutaja wapi ili tusipate kumkamata.

Mhe. Spika, kama katika kitabu chake katenga barabara kidogo, lakini hakuzitaja sasa kama atazitaja kama alivyotaja humu kwenye kitabu nitajenga barabara anitajie barabara ya Koani – Jumbi, barabara ya Mfenesini – Bumbwini, Jendele- Unguja Ukuu, basi mimi nitaunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii, kinyume cha hapo mimi kwenye hotuba hii, lakini hata kwenye hotuba za sekta maalum za hiyo barabara utanivumilia Mhe. Spika, nitakuwa mgumu mno kuikubali hotuba hii.

Mhe. Spika, kwa hivyo cha muhimu anieleze Mhe. Waziri kwa nini kwenye bajeti hii barabara hizo hazikutajwa na kama kazitaja ametaja kama fumbo, ataponiwekea wazi basi mimi sina mashaka na hayo.

Mhe. Spika, pia kwenye kitabu cha mwelekeo kwenye ukurasa wa 27 na 28 amesema kwenye utunzaji wa barabara yatafanywa matengenezo madogo madogo. Wapi? Ndio niliposema hii ni kama fumbo. Je, Kwahani – Kwamtipura, Mpendae – Jang'ombe au wapi. Kwa sababu mwaka huu tumeona Wilaya ya Mjini tu ndiko alikoelekea, basi atwambie anaendelea kule kule tuweze kulia vile vile, wapi atafanya matengenezo madogo madogo haya ya barabara atusaidie. Hayo ameeleza kwenye kitabu cha mwelekeo katika ukurasa wa 27 na 28.

Mwaka jana tulikuwa na kilio cha huduma ya afya hasa katika Wilaya ya Kati, tulipendelea kuwa na hospitali yetu ya wilaya au hospitali kubwa na tukapewa matumaini, tukapewa taarifa kuwa katika ziara za Makamo wa Rais Dr. Ali Moh'd Shein katika Falme za Kiarabu kuwa kumetokea uhisani wa kujengwa hospitali hiyo.

Mhe. Spika, mimi na Mhe. Mkuu wa Mkoa tulihangaika kutafuta eneo tumeshapima eneo la Binguni pale, hatimiliki tayari tumeshakabidhi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, lakini Mhe. Waziri sijui kama hawajawasiliana naona humu tupu, kama hakuna basi kile kiwanja tuwaachie wananchi wapige matuta wapande viazi kisikae bure. Bado huduma kwa Wilaya ya Kati baada ya vituo vyetu vidogo hata hiyo sekta wanayosema daraja la pili au la tatu hapana Wilaya ya Kati. Daraja la pili tunaambiwa kile kituo chetu cha Mwera, nyumba ile mchezo wa Dr. Ayoub umefanywa hapo hapo, sehemu ya kufungia vidonda hapana, bado hatuna kituo cha afya chenye hadhi.

Sisi tulitegemea hospitali ambayo tuliambiwa itajengwa pale Binguni ambayo eneo Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Mazingira keshatupa ametupa

matumaini. Sasa Mhe. Waziri hiki ni kilio cha wananchi wa Jimbo la Koani ambapo ikijengwa hospitali hiyo sisi sote watu wa Wilaya ya Kati tutafaidika.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo wananchi wamezungumza juu ya hisia zao za upandishwaji wa mishahara ambalo linakwenda sambamba na upunguzaji wa kodi ya *VAT* kutoka asilimia 20 hadi 18. Maoni yao yanakwenda sambamba hapa, hivyo kupunguzwa huku kwa asilimia mbili hii kutamsaidiaje mwananchi wa kawaida wakati hii inao wadau wawili yaani wafanyakazi na wakulima. Tukikumbuka kuwa asilimia ya wafanyakazi ni ndogo sana kuliko hii ya wakulima, lakini wafanyakazi wakilia kilio kidogo waongezewe mshahara sasa hawa wao watafaidika vipi nakupandishwa mshahara.

Mhe. Spika, maoni yao juu ya hili la kupandishwa mshahara hayawasaidii, njia nzuri itayowasaidia wafanyakazi na wakulima wa kawaida ni kupunguzwa zaidi hii kodi ya *VAT* kwenye vitu muhimu. Mchele ukiuzwa kilo shilingi mia tano atanunua mkulima na mfanyakazi, hiyo itakuwa ni suluhu watu wote wamefaidika, lakini unampandishia mshahara mfanyakazi bado mzigo huu wote unamuangukia mkulima ambao ni watu wengi katika nchi hii.

Mhe. Spika, naiomba serikali hasa Mhe. Waziri basi maoni haya ayafikirie, kwa sababu kila ukipandisha mshahara kwa wafanyakazi, basi wafanyabiashara wanapandisha bei za vyakula na vitu muhimu. Sasa kwa kiwango fulani utaona serikali imeshapandisha huko lakini je, huu umma mkubwa unaufanya nini, lakini njia waliyotoa watu wangu nafikiri ni sahihi, utakapopunguza kodi kwenye vitu muhimu ambavyo watu wote wanatumia hawa wafanyakazi na wao nafikiri hiyo itakuwa ndio njia sahihi na mimi naunga mkono naishauri serikali juu ya hili.

Lakini pia niungane na Waziri Kivuli juu ya mafao ya wastaafu. Mhe. Spika, kwa kweli bado serikali haijawatendea haki wastaafu wetu, fedha wanazozipata kidogo wakati wametumikia nchi hii kwa muda mrefu na bado wanastahiki kuishi katika nchi hii ili waweze kumudu maisha kama watu wengine. Serikali inamstaafisha mtu kwa sababu ameshachoka hamudu kufanya kazi. Usitegemee mtu yule sasa hivi akamate jembe alime zaidi ya kupalilia nyumba yake anayoishi, sasa ili aweze kuishi basi serikali imuwezeshe. Mhe. Spika, tunakusudia hiki kiinua mgongo kinachotolewa na serikali nacho kipandishwe ili kiweze kumkidhi tufanye kazi. Mhe. Spika, imezungumzwa hapa huwa wanaongezewa shilingi tano hazisaidii kitu.

Mhe. Spika, katika njia za kuinua hali za wananchi bajeti hii siku zote inakwenda kwa *ceiling*, wizara inayohusika huambiwa fanya bajeti yako ya vitu unavyovitaka. Lakini Mhe. Spika, katika mtazamo wangu wa shughuli za kawaida kwenye kamati kuna maeneo mawili yanaumia sana kwa maisha tu, la

kwanza ni eneo la hospitali. Mhe. Spika, nazungumza kwenye bajeti hii sitaki kuizungumza kwenye sekta kwa sababu nitakuwa nawaonea. Mhe. Spika, fungu la vyakula linakuwa dogo mno.

Siku moja nilikwenda hospitali kiasi saa 6.00, basi akaja *orderly* akawaambia leo chakula hakuna mjitegemee hivyo muwaagizie jamaa zenu kutoka nyumbani. Mhe. Spika, hii ni hatari kwa sababu wanajua ni kawaida pale mtu aliyelazwa anapata dawa na chakula, hiyo saa 6.00 mtu atapata wapi chakula nae kalazwa pale yupo miguu juu, anamsubiri anayekuja saa 7.00 anamwambia hata akimaliza kupika saa 10.00, mgonjwa anapewa madawa pale yanamlevya kwa sababu ya njaa si atakufa.

Mhe. Spika, hapa nakusudia fungu la vyakula lisifanyiwe masihara kwa wagonjwa wanaolazwa hospitali. Wagonjwa wanapewa chakula mara mbili si sahihi tunawadhili. Mhe. Spika, mimi nimewahi kufanya kazi hospitali na pia nilikuwa nashughulikia chakula. Kwa uchache walikuwa wanapewa chakula mara tano. Alfajiri wananawishwa uso wanapewa uji wa pilipili, kabla ya kupewa dawa saa 1.30 wanapewa chai, saa 4.00 wanapewa kikombe cha maziwa na yai, saa 7.00 mchana wanapewa chakula chengine kizito, saa 10.00 wanapewa chai kwa biskuti na jioni wanapewa mkate kwa supu ya tungule au nyama. Hivi ndivyo walivyokuwa wakipewa na mgonjwa anaondoka pale akiwa amepona kwa sababu dawa bila ya chakula haziwezi kumponesha mtu.

Mhe. Spika, samahani kwa kumtaja jina Dr. Mwinyihaji Makame aliwahi kuja miaka minne kachukua kozi akafanya kazi miaka miwili kabla ya kwenda Wizara ya Kilimo anajua hivyo. Sasa sijui kwa nini fungu la vyakula analibinya na hali anajua mimi nastaajabu sana.

Jamani jambo hili tusilipuuze, mgonjwa kulazwa hospitali akanyimwa chakula badala ya kumtibu tunamuua. Wengine wana jamaa kenda kampelekea bakuli la supu lakini wengine hawana hasa sisi tunaotoka vijijini. Mtu atatoka Kae Kuu huko kachukua uji hata akifika huku umeshapoa itakuwa togwa hilo. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunakusudia kuwa bajeti hii kwenye suala zima la vyakula kwa wagonjwa katika hospitali litupiwe macho na lisifanyiwe masihara.

Mhe. Spika, suala la pili ni wanafunzi walioko Chuo cha Mafunzo. Waheshimiwa tumekwenda pale tumefanyiwa bajeti anatwambia Kamishna wa Mafunzo kwa makisio pesa ninazopata mimi ni shilingi 500/- tu ambazo wewe unampa mjukuu wako anapokwenda skuli. Binadamu kamili unaweza kufanyishwa kazi nzito, kama anapewa landa inakuwa landa, kama kuni wanachanja. Wastani wa pesa ambazo anatumia kwa chakula ni shilingi 500/-.

Mhe. Spika, eneo hili nasema lisifanyiwe masihara, maana kila mtu anaumwa hapa na kule vile vile sote ni malaika kila mmoja ana kosa na lazima apelekwe kule kwa ajili ya kurekebisha tabia. Sasa unakwenda kule siku nyengine anasema ni mlo mmoja tu au miwili baba kama wewe Mhe. Spika, si unauliwa badala ya kurekebishwa tabia. Hiyo nia ya kurekebisha tabia itakuwa? Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri na eneo hili wasilifanyie masihara na pia pesa zao watoe kwa wakati.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye mambo ya kiuchumi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anatwambia tuimarishe miundo mbinu katika mambo ya kilimo. Lipo tatizo kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na wawakilishi muda wote wanazungumza, tatizo hili la kuhakikisha kuwa mpunga ndio unaopewa kipaumbele, hivyo sisi sote tunakula wali tu kila siku? Hapa tuna kasoro kwenye mipango yetu.

Tutachukua muda kuweza kuhakikisha kwamba tunaumudu mchele sisi wenyewe bila ya kuagizia. Lakini tuanze mambo madogo madogo ambayo tutaweza kukidhi mia juu ya mia hasa mahitaji ya mboga mboga, angalau tuweze kulima kabeji, mchicha bila ya kuagizia. Mahoteli yapo ndio sekta itakayoisaidia.
Pamezungumzwa habari ya ajira wananchi wetu kuwezeshwa kufanya vitalu, konde au mashamba ya mboga mboga. Sekta hii ya kilimo itasaidia sana kuongeza ajira na pato la nchi yetu. Lakini sisi kazi yetu ukija sijui mpunga wa kumwagilia. Tuanze mambo madogo madogo na haya yanakwenda taratibu.

Mhe. Spika, katika huu mpango aliozungumza Mhe. Waziri wa kuimarisha kilimo, nafikiri tuelekee kwanza kwenye ukulima wa mboga mboga, vitunguu maji vinaota Unguja na Pemba kwa ardhi yetu, mbatata, karoti, matango haya sisi tunayataka kwa afya yetu lakini pia kuweza kukidhi mahitaji ya mahoteli yetu.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ardhi tuliyonayo nyengine kuna ukulima wa maweni. Imezungumzwa kuwa Kamati ya Utafiti wa Kilimo imekwenda. Lakini nafikiri kuwa watu wasiohusika waliotiwa mle hawakuweza kufanya utafiti kuweza kuitumia ardhi tuliyonayo Zanzibar. Ardhi nyengine tuliyonayo ya coral wamefanya wa kutosha ili tuweze kutoa chakula. Vyakula vya mizizi vinakuja katika mawe pamoja na nafaka kama mtama, mahindi na vyenginevyo.

Sasa kwa kiasi gain tumeweka malengo ya kuhakikisha tani ngapi tutoe za mtama, hatuzungumzi tunazungumza tutalima eka ngapi. Tuseme tani ndio kitakuwa kipimo kwetu sisi wanasiasa kuweza kuishauri serikali. Ukanda wa Mtende, Uroa na Pongwe ni ukanda wa mawe, tani ngapi tumejipangia

kuzalisha mtama na tutauwekea miundo mbinu gani ili wananchi waweze kuzalisha. Tumeyashughulikia mabonde haya haya ya Chechele, Kibokwa, Mtwango lakini asilimia kubwa ya ardhi hatujaitumia na wananchi wapo. Wenzetu wana ardhi mbaya kuliko ile lakini wanazalisha ngano na kila kitu, kwa nini sisi tushindwe.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje kutueleza ni kiasi gani ardhi ya coral tutaweza kuitumia na ni eneo kubwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Pemba ni kuanzia Kiwani, Makaani, Vitongoji mpaka unafika Micheweni. Tutaweza kuifanyia kazi ardhi hii kubwa iweze kuleta tija kwa chakula. Kwa sababu hata hayo mataifa yametwambia sasa hivi hatukusaidieni, tutakusaidieni njia za kuweza kuzalisha chakula ili muweze kushiba kwanza.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu uvujaji wa mapato. Yamezungumzwa mengi lakini kuna eneo la ada na viza pamoja na uingiaji kazi ambazo zinafanywa na Idara ya Uhamiaji. Eneo hili Mhe. Spika, tangu kuambiwa fedha hizi zinazopatikana nusu zibakie Zanzibar na nyengine wapewe Idara ya Uhamiaji hapa Zanzibar hazina mshughulikiaji. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa sababu kile ni chombo cha Muungano wameachia wanangojea watu wazikusanye ziletwe. Serikali ya Muungano wa Tanzania wameona kwa sababu fedha hizi sasa wanachukua Idara ya Uhamiaji Zanzibar na zinakwenda Zanzibar hawashughuliki. Mhe. Spika, Idara ya Utalii inapokea pesa nyingi sana watalii wanaokuja wote wanalipa, hawa wazungu wote wanaofanya kazi hapa tunawapa vibali vya kukaa hapa nchini wanalipa pesa zinavuja. Mhe. Spika, naomba mwanya huu uzibwe

Mhe. Spika, jengine ni serikali zetu za mitaa, masheha na wilaya katika suala zima la uuzwaji wa maeneo. Kuna asilimia iingie kwenye serikali za mitaa haziendi, sheha ana mkoba wake anakwambia hizi nimepewa kwa Mkuu wa Wilaya wala hana risiti. Mhe. Spika, maeneo kuanzia Pongwe na Kiwengwa eka kwa maeka wamemilikishwa watu tena kwa kuuziwa, kwanza wanatoa pesa za *advance* ambazo zingekuwa zinastahiki asilimia kumi ziingie kwenye serikali za mitaa lakini zinaingia mifukoni mwa watu hawa, madiwani, masheha na ofisi zao za wilaya.

Mhe. Spika, kwa heshima naiomba kamati yako inayohusiana na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi basi kazi ya mwanzo tukianza basi waende waone maeneo haya yaliyokodishwa mangapi, fedha zilizotolewa ni ngapi ambazo ziliingia nchini. Waone na waje kutwambia kwenye Baraza lakini eneo hilo linatuhumiwa linavujisha fedha nyingi haziendi zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi.

Mhe. Spika, la mwisho niwaombe wananchi tufanye kazi kwa bidii kwenye kazi za kilimo. Lakini tuna tatizo kwenye mipango yetu yote nimesahau naomba nirudie kwenye shughuli za kilimo tuna janga moja la maradhi.

Mhe. Spika, Waziri kivuli alizungumza tulikuwa tukiuza embe tangu tani kadhaa mpaka tumefika ziro. Mhe. Spika, machungwa yana wadudu mabungu, matofaa yana mafunza, embe zina mafunza. Hivyo nani atakwenda kununua embe yenye mafunza, mtu wenyewe mzungu au mwarabu kutoka nje sisi wenyewe hatuli. Kweli lakini si yeye tu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atwambie katika mpango huu wa kuimarisha kilimo upande wa utibabu wa mimea kwa sababu ndio wenye matatizo. Mhe. Spika, mimi mwenyewe ni mkulima mwaka huu nimekula hasara eka zaidi ya sita sikupata muhogo mote umeoza umepata madudu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili la utibabu wa mimea pamoja na maradhi ya matunda lisaidiwe. La si hivyo, hayo matunda au hicho kilimo ambacho tunawaambia wananchi walime hayatasaidia kitu. Mhe. Spika, nashukuru ardhi hii tuliyojaaliwa lakini mazao yote yana maradhi.Upande wa pembejeo zilizoletwa ni hafifu hazikutosha mwaka huu hasa dawa za magugu. Sasa katika huu mpango wa kuimarisha kilimo kama bajeti ilivyozungumza basi ihakikishe zinakuwepo dawa za kutosha serikalini. Wafanyabiashara binafsi sasa hivi ndio wanaowakomoa wakulima kwa sababu wameshaona ndio tunakokwenda wanatukomoa kuhusu bei za dawa na mbolea pamoja na dawa za mifugo ambayo miradi ya *PADEP* na mengineyo imeletwa na serikali hii kuwasaidia wananchi. Mhe. Spika, ili kuheshimu kauli yako basi kwa heshima na taadhima nikushukuru ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na tukawa wazima tukaweza kupata fursa kuzungumza machache kuhusiana na bajeti ya mwaka 2009/2010 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuunga mkono maelezo yote yaliyotolewa na Waziri kivuli na kuitaka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iangalie upya mtazamo kwa maslahi ya kuwanufaisha wananchi wa visiwa hivi viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwanza mimi mara nyingi nikianza katika michango ya bajeti ikiwa tutaangalia *hansard* basi huwa kuna kauli naitoa na naomba Mhe. Waziri akatazame tena bajeti za miaka mitatu, minne, mitano iliyopita kwamba keki iliyotayarishwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni ndogo sana na watu walioalikwa. Nasikia hapa mjini kuna utaratibu wa kutoa kadi kwa sababu kile kilichotayarishwa kina idadi maalum ya watu wa kuwapa. Sisi watu wa shamba

huwa tunapiga upatu tu pale atakayekuja tena akija na mwanawe wote watakula.

Sasa kwa sababu hii bajeti inatoka mjini basi ingefaa kila mtu akapewa kadi ili nay eye akapata. Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika, tukigawanya hizo asilimia hakuna wizara hata moja itakayopewa asilimia mia hicho kilichopewa ikatekeleza mambo yake yalivyo kawaida. Kwa hivyo, inaonesha kwamba bajeti inayotayarishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni ndogo sana ukilinganisha na hali halisi. Hii inatokana na udhaifu wa serikali yenyewe katika kubembeleza vianzio vya mapato. Vianzio vya mapato vipo vya aina mbili na vyengine vinajificha.

Mhe. Spika, aina ya kwanza ambayo sasa hivi ndio iliyotiliwa mkazo sana ni mapato yatokanayo na kodi ya moja kwa moja. Kwa sababu kutokana na bajeti hii iliyotajwa inaripotiwa kwamba hata ilipofika mwezi wa Juni matarajio ya ukusanyaji wa kodi yalifikia asilimia 99 katika kila pande, inaonesha kwamba serikali imefikia kikomo cha kuwakamua wananchi wake na haiwezi tena kwenda kuwabana kwa sababu watatoka damu sasa. Kwa hivyo, ikiwa ukusanyaji wa kodi umefikia asilimia 99 ulipofika mwezi wa Juni inaonesha kwamba serikali sasa itafute njia nyengine za kutafuta mapato.

Mhe. Spika, moja imetajwa na Mhe. Waziri kivuli kwamba ni kurudia sera na matatizo yaliyomo katika Muungano na kuona ni kiasi gani Zanzibar inajikwamua kupata mapato ambayo ndani ya ulimwengu wangeliyapata au ndani ya Tanzania ingeyapata.

Lakini la pili ni suala zima la kutafuta nishati mbadala. Kwa sababu ukiweza kupata nishati mbadala unaweza ku-*save* yale matumizi ya kulipia nishati. Sasa uki-*save* matumizi unayolipia nishati moja kwa moja umeongeza mtaji fulani katika bajeti yako. Sasa tukifanya mchezo wataalam wengi wamekuja na leo nashukuru kidogo Mhe. Naibu Waziri alitaja taja hapa lakini mwakani akija atataja vile vile alikuja akaondoka kila siku hakuna kinachokuwa na wenzetu wanaendelea kupata nishati mbadala.

Lakini suala jengine Mhe. Spika, lingeweza kuokoa sehemu ya fedha ni sherehe. Wakati ambao Mapinduzi ya mwaka 1964 yalifanyika kuwakomboa wakulima na wafanyakazi watoto wetu wanagaragara chini hawana kiti cha kukalia tofauti na waheshimiwa wanaozunguka kwenye viti vyao. Mtoto wa mkulima na mfanyakazi anagaragara chini katika sakafu au katika vumbi.

Kuna tetesi kwamba serikali ilitumia zaidi ya shilingi bilioni 3 katika Sherehe za Mapinduzi kule Pemba. Mhe. Spika, nasikitika ikiwa hiyo ni kweli namuomba Mhe. Waziri aangalie tena matumizi ya fedha katika sherehe. Bora

tungelielekeza wakapata samani watoto wetu halafu tukashereheka kwamba tumewapatia samani, kuliko kuwaalika watu wakapiga wali siku tatu walipoondoka wengine wameshajaza mifuko yao.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu mwelekeo wa bajeti hii kuna mfumko wa bei ambao umefikia asilimia 20.6 kwa mujibu bajeti hii ikichangiwa zaidi na mfumko wa bei katika bidhaa ya mchele. Tokea mwaka jana serikali ilishauriwa kwa nguvu kabisa kwamba iweke akiba yake ya nafaka *(strategic grain reserve).*

Kipindi cha mwezi mmoja tu uliopita tulipata mtikisiko mdogo hivi wa bei ya mchele, badala ya ku-*stabilize* kidogo ukapanda juu halafu ukarudi tena. Lakini serikali haijatwambia katika bajeti hii kwamba angalau ina mpango gani wa kuweka akiba ya chakula wakati nchi zote duniani ikiwemo na Tanzania Bara zina mpango huo wa kuweka akiba ya chakula kwa sababu ya kuzuia mitikisiko inayotokezea katika ulimwengu kwa ukosefu wa bidhaa hii.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba Zanzibar inaonekana ni mfuataji tu katika maamuzi ya kodi. Kwa sababu wakati bajeti ya Tanzania iliposomwa ndio ikatajwa kwamba VAT imeteremshwa kutoka asilimia 20 mpaka 18. Nilifikiria kwamba Zanzibar ingesema sisi tutafika asilimia 16 lakini imetoa *photocopy* ile ile tu. Kwa hivyo, hakuna jipya hapa tunatarajia labda kutakuwa na hatua nyengine za kuwapunguzia makali wananchi sio hii, kwa sababu hii imeshasemwa.

Mhe. Spika, moja katika madhumuni makubwa ya kufanywa bajeti na kuwapa matumaini wananchi ni jinsi gani bajeti ile inavyoweza kuongeza ajira. Hatukusikia katika kurasa hizi zilizotolewa hapa kwamba kuna mkakati fulani wa kuongeza ajira za vijana wetu. Kwa hivyo, nadhani bajeti hii bado haijawa na mwelekeo wa kuwapa matumaini wananchi. Kwa sababu maelezo mengi yametolewa kijumla jumla kwa hivyo bajeti haikuwa na takwimu za kutosha za kui-*support* katika maelezo yake.

Pia inalingana sawa sawa na malalamiko yaliyopo kwamba bado Zanzibar haijawa na utamaduni wa kutumia takwimu katika kutekeleza mipango yake ya kimaendeleo na kibajeti. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri aje hapa atueleze kuwa kitengo chake ambacho bahati nzuri kipo chini ya wizara yake kimeteleza kidogo au vipi. Lakini katika bajeti hii takwimu kwa kweli imekosekana kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 19 katika kitabu cha bajeti kilichosomwa kuna neno linaloitwa changamoto na changamoto moja imeandika ongezeko la kasi la idadi ya watu. Lakini mimi nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri, hata Mhe. Waziri

kivuli alisema hili kwamba ongezeko la watu lipo kwa upande wa wanavyozaa watu *(birth rate)*, lakini ongezeko la watu vile vile lipo katika Idara ya Uhamiaji namna watu wanavyohamia.

Hapa kisiwa cha Unguja *demographic picture* yake inabadilika sana kwa sababu ya mambo mawili. Tusingependa itokezee hivyo. Ndugu zangu na jamaa zangu kutoka Pemba kwa sababu serikali imeshindwa kutononesha maendeleo halisi Pemba wanawajibika kuhama kuja kutafuta ajira. Tunapiga kelele sisi angalau hivi vyuo.

Mhe. Spika, Vyuo vyote vya Elimu ya Juu hata kile ambacho sisi ndio wazalishaji wakubwa wa ndizi na mihogo, basi chuo kinawekwa Kizimbani na wala sio Kizimbani ya Wete Pemba kwa Mhe. Said Ali Mbarouk, yaani Kizimbani ya Unguja.

Kwa hivyo, kuna utaratibu gani ambao nchi haigawi ? Kwa mfano juzi hapa tumeona Chuo Kikuu kimepelekwa Dodoma na Arusha pamoja na Morogoro pia kiko. Sasa hivi visiwa vyetu viwili tu tunashindwa hata na chuo kimoja na kusema kwamba chuo hiki tunakipeleka Pemba na wao wakaonje hizi ajira.

Kutokana na hali hii tunategemea nini? Kwa hivyo, ni lazima atakuja kutafuta ajira na wala hawaji kama ni Kisiwa cha Unguja, yaani anakuja kwamba ni Makao Makuu na kila kitu kimewekwa hapa ndio suala analokujia *(Makofi)*.

Mhe. Spika, hata kile Chuo cha Kilimo badala ya kuwekwa kule Konde ambako mvua haziondoki na tena kuna Msitu wa Ngezi na kinawekwa hapo Kizimbani Unguja.

Vile vile juzi mashahidi wapo tulikuwa kwenye kazi za kamati. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji ilipofika wakati wa Bajeti ya Biashara niliwaambia kwamba hamjatuambia kuhusu utaratibu wa viwanda. Basi nitastaajabu kuona Kiwanda cha Usindikaji wa Embe kikawekwa Matemwe na wala kisiwekwe Ole na wenyewe walikuwepo. Mhe. Spika, sisemi uongo na wala simsengenyi mtu isipokuwa ninachokisema ndicho kile ambacho nilikisema kwenye kamati na hilo la kwanza *(Kicheko/Makofi)*.

Lakini *demographic picture* ya pili ni uhamiaji wa watu kutoka Tanzania Bara. Tanzania Bara si watu wa Tanganyika tu, kwa sababu kuna wahamiaji kutoka Burundi, Rwanda, Congo na kwengineko wote wanakuja, lakini sisi tunakaa na kusema ongezeko la watu.

Mhe. Spika, nitastaajabu sana Mzanzibar akapigwa sindano, ili asizae sana lakini ukawaachia watu waingie, kwa lengo la kufaidi matunda ya Zanzibar na

wale wa hapa wasizae sana Kwa hivyo, ninawashauri wazae sana sasa, ili na sisi tupingane na tupate *population* kubwa na wala masuala ya majira watu wasitumie, kwa sababu huu ni utaratibu mbaya. Kwa mfano, kungelikuwa na njia ya kwamba sisi ni kisiwa tuna-*control measures* na wala mtu duniani hakatazwi pa kwenda yoyote yule, ndio maana watu wana *Visa* pamoja na *Passport*, lakini hata *control measures*. *(Makofi)*.

Suala la ongezeko la watu tulitizame pande zote. Kwa upande wa ndugu zetu wa Pemba waekeeni maendeleo turudi na tukajenge kisiwa chetu. Na watu kutoka Tanzania Bara viwekwe vikwazo vya vitambulisho vya kuweza kudhibiti hali hii *(Makofi)*.

Mhe. Spika, niunganishe hapa kabisa kuhusu suala la hivi Vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi vinavyotoka hapa ni haki ya Mzanzibari, kwa nini watu wengi hawapati haki hii na wanaishi hapa na lengo ni kuzuia kwamba huyu siye na yule ndiye. Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu suala la mishahara. Mhe. Spika, Zanzibar viwango vyake vya mishahara ni vidogo sana na mimi nilifanya hesabu ya haraka, basi mtu apate chakula angalau mara mbili kwa siku lazima awe na shilingi 10,000/-, tena shilingi 10,000/- hiyo pamoja na *asprin* au *panadol* kwa sababu mara moja huyu ama yule kaumwa.
Kwa hivyo, shilingi 10,000/- kwa muda wa mwezi mmoja mfanyakazi anahitaji alipwe angalau mshahara wa chini shilingi 300,000/-. Lakini unapompangia shilingi 100,000/- tena kwa mkupuo mpaka kwanza wende ukatie udhu ndiye uje umlipe. Kwa kweli suala hili halitatufikisha mbali, kwa sababu watu wetu ni masikini, mishahara midogo na wala hii shilingi 100,000/- haitoshi.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli) nadhani alianzia tu pale kwamba iwe shilingi 150,000/-, lakini nina amini angeweza kuendelea. Kutokana na hali hii serikali ingepaswa ifikirie tena je hizi fedha tunazowapa wananchi kwa kazi walizofanya ? Mimi mwenyewe binafsi ikiwa napokea mshahara serikalini wakati ninapomwita fundi yeyote, basi yeye atanitoza fedha kwa kazi atakayoifanya na wala sio kwa fedha nilizonazo mimi.

Kwani yeye atatizama kazi ile ataifanya siku ngapi na chejio chake siku ngapi, kwa mfano akitaka kunitengezea kitanda, kunikata nywele, kunishonea nguo, yeye atanitoza kwa mujibu wa kazi anayoifanya. Lakini serikali tu ndio iwape wananchi ujira wao kwa mujibu wa fedha walizonazo na wala sio kwa kazi wanayoifanya au mahitaji. Kwa hivyo, hapa kuna kasoro kubwa sana, basi ni vyema ifikirie tena.

Mhe. Spika, na tujitizame sisi wakati tunapostaafu kweli mtu alipwe shilingi 15,000/- kwa mwezi hata nauli ya kwenda na kurudi, kwa kule kwetu Pemba tuna utamaduni wa kununua halua. Kwa hivyo, ukifika mjini na baada ya

kupewa fedha na kwenda kununua halua basi ndio zawadi tosha ya mshahara wako wa mwezi mzima. Wajukuu wako, yaani wajukuu wangu serikali imenipa vikanda viwili vya halua ndio nimewachukulia, iliyobaki mnipe nyinyi, ninadhani hatuko radhi hivyo.

Kutokana na hali hiyo, serikali ifikirie kama walivyosema wenzangu kwamba ifikirie tena njia ya kuwalipa wastaafu pato zaidi, angalau aweze kujikimu kwa siku kumi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika bajeti hii kuna sherehe imepita na ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, atupe ufafanuzi kuhusiana na suala hili. Kwa mujibu wa ilivyoripotiwa kwenye ukurasa wa 29 na kuendelea ni kwamba Miradi ya Maendeleo ilipofika Machi 2009 wafadhili walikuwa wameshalipa asilimia 35.33.

Sasa ukiwavuta wafike asilimia 40 au 50 mpaka mwezi wa Juni, kwa sababu serikali ilijipangia kutoa kidogo sana asilimia 10 tu ya mchango na kufanya asilimia 60 ndio fedha zilizopatikana. Kwa hivyo, mbona hawajatuambia ni miradi gani iliyokwama kwa sababu wafadhili hawakutoa fedha ipi iliyokamilika kutokana na fedha za wafadhili na ikiwa haikuripotiwa hivyo ina maana hii miradi hakupangwa vizuri. Kwa sababu hawa wafadhili wametoa asilimia si zaidi ya 50 na miradi imekamilika. Kwa hivyo kulikuwa na udanganyifu ndani yake. Kutokana na hali hiyo namuomba Mhe. Waziri aje atueleze ni lipi sahihi hapa, yaani miradi imekamilika au haijakamilika kutokana na kwamba wafadhili hawakutoa fedha kikamilifu, kikwazo gani kilichowapata wafadhili wasitoe. Mhe. Spika, ikiwa kuna kikwazo kwa nini tuliwapangia wafadhili watoe fedha nyingi zaidi ya kile tulichowapangia mwaka jana.

Inawezekana na ninaishukuru serikali hapa kwamba imeongeza mchango wao kutoka shilingi bilioni 19 mwaka jana hadi kufikia 40 bilioni na kufikiria wafadhali hawatoi sana. Lakini kwa nini wale wafadhili wakawapandishia kutoa shilingi bilioni 172 mwaka jana hadi shilingi bilioni 199 watoe mwaka huu. Wakati mwaka uliopita wametoa asilimia si zaidi ya 50 ya michango waliopanga. Kwa hiyo, hapo namuomba Mhe. Waziri aje atufahamishe kidogo kuhusu suala zima la wafadhili kuhusiana na michango yao.

Vile vile kuna suala la mtikisiko wa fedha duniani pamoja na hali ya uchumi na kila nchi inatangaza hali ya kujiokoa na wala hapa hatujaisikia na kiasi gani kilichotengwa na kitatoka wapi bado hatujakisikia, Zanzibar imejitayarisha vipi na itaokoa katika hali gani ? *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika bajeti hii kama nilivyosema kwenye takwimu, vitu vinavyoingia hapa vinakuja kupitia njia mbili, ama kutoka nje ya Zanzibar zile *tonnage* yake inajulikana, kwa sababu inakuja na *bill of landing* na kila kitu kinajulikana. Kwa hivyo, tunajua tunaingiza mchele kiasi gani pamoja na mambo mengine. Lakini kuhusu mazao yanayotoka Tanzania Bara, mengi yanafikia *Dhow shed* na wala hakuna *tonnage*, isipokuwa watu wanapakia jahazini na kuondoka. Vile vile mazao yanayotoka shamba ambayo takwimu ni muhimu sana haijulikani ni *tonnage* yake.

Mhe. Spika, kwa mazao yanayotoka Pemba sijasikia humu kutajwa mezani za barabarani na sijui kwa kitaalamu zinaitwa vipi. Kwa kweli nchi zote duniani wanazo isipokuwa Zanzibar. Kwa hivyo, labda sio na ikiwa ndio basi watutajie mezani hizo, zitafika lini hapa kwa sababu ya kupata takwimu halisi ya bidhaa zinazoingia na kutoka kwa ajili ya usalama wa nchi nzima.

Suala la kilimo Mhe. Spika, kuna siku yake tutakuja kulizungumza. Lakini kwa ujumla serikali bado haijaonesha msisitizo mkubwa katika kukibadilisha kilimo kutoka hiki kinachoendelea cha mkono na kuelekea kilimo cha kitaalamu. Kwa hivyo, bado kuna haja kubwa ya kuongezeka kwa matrekta pamoja na mashine nyengine.

Nikiendelea na mchango wangu ni kuhusu suala la *Tariff Harmonazation*. Kwa sababu Sera ya Serikali ni Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, yaani sio kukuza uchumi tu na kama ni kukuza uchumi tu basi tungemalizia hapo, kama vile kwenye Kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu Qur-aan katika aya inayosema “Wameangamia wanaosali …” na wala hawakumalizia hapo tukaikata aya katikati. Kwa hivyo, tuwafikirie wale wananchi wa chini ikiwa sisi tutakweza hivi viwango vya kodi tukavifanya sawa na Bara, wakati wao masoko yao ni makubwa, yaani wanauza kwa wingi na sisi kwetu hapa ukesha muuzia mjomba, shangazi anakuja kukopa, sasa vipi tutaweza kuwaokoa wananchi wetu katika suala hili.

Mhe. Spika, tukiende kwenye Serikali ya Muungano kama ni serikali basi tuwe tukielezea *position* ya Zanzibar na hali hii ya kukweza kodi na wala tusichukulie kibiashara na kukuza uchumi, isipokuwa tuzingatie na mapato ya wananchi wetu.

Kama tulivyosema kwamba mishahara yetu ni midogo sana hata ukilinganisha na hapo Bara. Walimu tu wakienda wanapewa shilingi 300,000/- ama 400,000/- , hapa wanaambia *graduate* ni shilingi 120,000/- na kwa upande wa wataalamu wakubwa ndio mambo yao mazuri zaidi. Kwa hivyo, lazima tuwe na msimamo wa kuilinda hii Zanzibar *otherwise* tutamalizia hivyo.

Mwisho Mhe. Spika, nataka nizungumzie kuhusu suala la mafuta. Kwa kweli suala hili si la kulifanyia mas-hara na wala mchezo kwa sababu tatu Mhe. Spika. Kwanza ni amana, unapopewa amana utakwenda ulizwa amana ile ulivyoitumia, sasa sisi tusijekuulizwa na vijukuu pamoja na vitukuu kwamba hawa waliopita katika Baraza la mwaka huu ndio waliotuponza. Kwa sababu tumeshapitisha azimio humu ndani ya Baraza kwamba mafuta ni ya Zanzibar na wala sioni sababu ya kuyumba. Mhe. Spika, nilizungumza humu wakati nilipokuwa nikichangia kwamba ikiwa mtu anaogopa kufa basi kitanda alichokinunua shilingi milioni 1 anakufa juu yake.

Basi anaogopa nini na wala hakuna anayejijua atakufa vipi, yaani mwisho wa binadamu ni kufa. Lakini kile kitanda alichokinunua shilingi milioni 1 na nyumba aliyoijenga kwa shilingi bilioni 1 ndiyo atakayokufia mule na watu wakaja wakalia na halafu karithiwa mule. Sasa wewe unaogopa nini kutetea maslahi haya *(Makofi)*.

Mhe. Spika, sisi tunachokisubiri hivi sasa ni chombo chetu cha Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta ndicho tunachokisubiri. Ikiwa kwenye kikao hiki hakikuwezekana basi Inshaallah tukijaaliwa kikao kijacho tuje tupitishe sheria ya kuundwa chombo hicho ama si hivyo tutakuwa tunadanganyana. Ahsante sana *(Makofi)*.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza hapa. Vile vile sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa katika hali ya afya njema.

Kwa kuanza mchango wangu nitazungumzia kuhusu suala la elimu. Kwa kweli kwenye bajeti kuna vitabu vya sekondari ambavyo vimepangiwa kupewa wanafunzi wa sekondari. Lakini Skuli zetu za Sekondari lugha ya kufundishia ni Kiingereza na bajeti iliyopita sikuona vitabu vya Kiingereza na wala bajeti hii.

Kutokana na hali hii hatuwezi kumfunza mwanafunzi akaweza kufanya mitihani yake vizuri ya masomo yote ya sayansi, *geography* pamoja na mengine bila ya kujua Lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atupatie vitabu vya *dictionaries, class libraries and class readers*, tukivipata hivyo basi kidogo tuta-*improve* katika Lugha ya Kiingereza. Kwa kweli bila ya kujua lugha hii basi hata hiyo sayansi hatutaweza kufanikiwa kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa walimu kilio ni kile kile namuomba Mhe. Waziri kuhusu lile posho la walimu la asilimia 25 warejeshewe kwa moyo wa imani kabisa *(Makofi)*.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Sekta ya Mawasiliano. Tukiangalia mapato yetu au bajeti yetu tunategemea uingizaji au kasma kutoka Uwanja wa Ndege. Lakini uwanja wetu wa ndege uko katika hali mbaya, basi angalau ungetiwa kwenye bajeti na kuanza kufanya ujenzi wa ukuta wa uwanja na baadaye tukatengeneza zile njia ya kurukia na kutulia ndege na tukaweza kupumua, kwa sababu wafanyabiashara wanapata tabu sana kwani ndege kubwa haziwezi kutua kwenye uwanja wetu.

Kwa hivyo, ninadhani uingizaji wetu utakuwa mzuri kama tutaanzia hayo halafu tena tutazidi kujenga mambo mengine.

Vile vile kuna suala la *Cable* mpya zinazotaka kuletwa Zanzibar kwa ajili ya kuboresha huduma za umeme uwe mwingi na kuwa na nguvu zaidi kwa maslahi ya yetu pamoja na taifa kwa jumla. Kutokana na hali hiyo nyumba nyingi zinaweza kuingia kwenye suala la kubomolewa kwa lengo la kupitishwa line mpya ya umeme huo.

Lakini kutokana na hali ya sasa ya mazingira na pia namuomba Mhe. Waziri kuhusu tathmini itakayofanywa kwa ajili ya zile nyumba, basi wale walengwa au wanaohusika na kubomolewa kwa nyumba zao walipwe kwa thamani ya sasa pamoja na kupatiwa viwanja *(Makofi).*

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuna hizi barabara kama ile barabara ya Mkapa iliyotoka Amani hadi Mtoni hii imeshatiwa kwenye mpango wa ukamilishaji. Lakini mpaka leo bado haijamaliza tena barabara ile inasababisha ajali nyingi sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba ile barabara ingemalizwa na kuepukana na ajali zinazotokea siku hadi siku.

Vile vile kuna barabara kwenye Jimbo langu Magogoni ya Kinuni japo kwa kiwango cha kifusi pamoja na kufukiwa yale mashimo, ili wananchi waweze kupita vizuri.

Nikiondoka hapo nizungumzie kuhusu wastaafu na katika hili nimuombe Mhe. Waziri kwamba hawa watu kama wangekuwa wanapewa maslahi yao kwa muda maalum, yaani wakeshastaafu tu wanapewa basi wasingependa kurejea tena na kuomba kazi tena. Isipokuwa wangejipanga vizuri na kuweza kuanza maisha yao mapya na kutoa nafasi za ajira kwa wengine ambao ni wapya.

Mhe. Spika, ahsante sana na leo nimezungumza kidogo kwa vile ndio siku ya mwanzo.

Ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja *(Makofi).*

Mhe. Said Khelef Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi. Pia sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote.

Mchango wangu nitaanzia kwenye sehemu za barabara. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Haji Mkema Haji amezielezea barabara tofauti hapa, lakini barabara ya Bubwini sikuisikia kutajwa kwenye kitabu hiki, ingawaje ilitajwa mwaka juzi lakini mwaka huu hawakuitaja.

Sasa wananchi wa Jimbo la Bubwini wamenipa masikitiko yao nikuletee wewe Mhe. Waziri kwamba kwa nini hawakusikia barabara ya Bubwini kutajwa, kuna sababu gani, kwani umezitaja ulizozitaja pamoja na zile zilizomalizika. Lakini katika hizo zilizomalizika zilikuwa kwenye kundi hili. Kwa hivyo, salamu zao walizonipa kwamba leo nipige buti hapa au wapate jawabu iliyosahihi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa kusema kweli barabara ya Bubwini wanavyosema wananchi wa Bubwini ni kwamba barabara hii haijengwi, kwa sababu tokea mwaka 2000 mpaka hivi sasa 2009 na jawabu za kujibu kule hatuna. Kwa mfano, mtu akiniuliza barabara yetu itajengwa lini basi humwambia asiniulize, lakini iko siku utanisikia ndio akaniambia kama safari hii kama hatukusikia umepiga buti Baraza la Wawakilishi Bubwini hulali. Mhe. Spika, Bubwini unakujua kama hukujui uje utembee *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli ninaushukuru Mfuko wa Barabara angalau umetuona mara mbili. Lakini hivi juzi walipokuja wametia upande mmoja tu kuelekea Makoba na kwa upande wa barabara kuu huku bado hali si nzuri. Kwa hivyo, hata wakulima Mhe. Spika, bidhaa au mazao yao wanapopakia kwenye gari huwa yanaanguka chini kutokana na ubovu wa barabara, hivi kweli wakulima hawa wataendelea na shughuli zao, nadhani hatavunjika moyo.

Kutokana na hali hiyo naiomba serikali kwa kupitia Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupatie majibu mazuri, ili wananchi wangu wasikie *(Makofi)*.

Mhe. Spika, silizungumzi hii kwa wizara hii isipokuwa wizara husika nayo ikae tayari, kwa sababu wameshachoka kudanganywa. Tulishawahi kumwita Mhe. Waziri na kutuahidi kwamba kabla ya bajeti barabara yetu itajengwa, lakini tunazunguzwa huku na kule na utaratibu huu si mzuri, kama haiwezekani ni bora tuambiwe *(Makofi)*.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu suala la nyongeza za mishahara. Mhe. Spika, wafanyakazi wetu wameongezwa shilingi 20,000/- lakini kwa awamu mbili na hili tumeshalikubali, ingawa ni kidogo, isipokuwa tunaangalia hali ya serikali ilivyo. Kwa hivyo, wafanyakazi wana malalamiko yao kuhusiana na hizi nyongeza za mishahara.

Kwa mfano, wakati tayari mwezi fulani waanze kupata hizo nyongeza za mishahara, wanasema hawazipati, yaani hawatiliwe, kwa hiyo kuna sababu zipi. Sasa wafanyakazi wametutuma rasmi kwamba tulizungumze suala hili na Mhe. Waziri ufahamu kwamba mishahara inapoongezwa basi unapofika ule wakati wapewe na isiwe tunawadanganya *(Makofi)*.

Vile vile kuna suala la wastaafu wetu hapa tayari wameshalipa, lakini hawa wanawapa pencheni, pia na wao wameniagiza nilizungumzie kuhusu pencheni wanayoipata ni ndogo na kwenye hii nyongeza ya mshahara wao hawakujisikia. Je, wao watakuwa wapi? Watapata nyongeza au hawatopata. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati anapofanya majumuisho atupe majibu mazuri kuhusiana na suala hili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nimalizie na suala la kilimo. Kwa kusema kweli wananchi wa Jimbo la Bubwini ni hodari wa kulima, lakini hawana sehemu ya kulima na hasa kilimo cha mpunga. Vile vile kuna tatizo kuhusiana na hizi mbolea zinazotolewa wananchi wa Jimbo la Bubwini hawafaidiki. Kwa sababu mbolea inapelekwa Mahonda, kutoka Mahonda mpaka Bubwini ni masafa na hata hali ya barabara niliyoizungumza ndio inajulikana, kupitia njia za ndani kuna kuwa na tope nyingi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na humu amezungumzia kuhusu masuala ya mbolea, lakini tunaomba wananchi wa Bubwini kwamba wasogezewe ile mbolea pamoja na dawa za kuulia magugu.

Hivi sasa watu wameamka kwa kilimo na wala tusifikirie kwamba mbolea hii inatumika kwa mpunga tu, mpaka mananasi watu wanalima kwa kutumia mbolea. Mhe. Spika, naiomba serikali ituonee huruma kule Bubwini kwa barabara, mbolea na mengineyo. Mhe. Spika, ahsante sana baada ya hayo machache na atakaponijibu vizuri Mhe. Waziri basi sitapiga buti na wananchi watatusikia *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda uliobakia ni mdogo sana, kwa hivyo, tujitayarishe kwa jioni na ninategemea kuanza na Mhe. Haji Faki Shaali (Mnadhim wa Upande wa Upinzani).

(Saa 6:55 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa11:00 jioni)

(*Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa jioni hii ya leo, mimi moja kwa moja nitakwenda kwenye michango kwa sababu shukurani zimeshatolewa za kutosha na wenzangu. Mimi kwanza naanza mchango wangu kwa kupitia mapitio ya uchumi kwa mwaka 2008/2009, nataka nizungumze machache sana katika mapitio haya.

Kwanza nimefarijika kwa kusikia kwamba mchango wa sekta ya kilimo umepanda kwa asilimia kumi na mbili hiyo ni habari njema, lakini kilichonichanganya mimi kidogo hapa ni pamoja na kwamba mchango wa kilimo umepanda na kwa maana hiyo mchango wa sekta ya huduma umepungua kutokana na kupanda kwa kilimo, lakini kutokana na *inflation* sababu moja ni kupanda kwa bei ya vyakula, sasa kama katika nchi umezalisha chakula cha kutosha zaidi ndio kilimo kimepanda sasa vipi *inflation* itasababishwa na kilimo tena.

Sasa hapa kidogo inanichanganya maana sikutarajia kuona maendeleo ya kilimo kuwa mazuri kutokana na mbolea na mvua mpaka imefikia asilimia kumi na mbili, lakini hapo hapo tunaambiwa *inflation* pamoja na mambo mengine na bei za vyakula, sasa vitu tumezalisha zaidi halafu bei za vyakula zinasababishwa na kilimo, hapo Mhe. Waziri naomba nipate ufafanuzi kidogo.
Mhe. Spika, halafu la pili ni katika deni la taifa limetajwa kwamba ni shilingi bilioni. 137 milini 809.73 ambalo kama Wazanzibar ukipiga hisabu kama tuko milioni moja itakuwa kila mmoja anadaiwa 137,809/= hilo ndio deni tunalodaiwa mpaka mtoto mchanga anayenyonya. Sasa mimi kudaiwa kama alivyozungumza somu yangu Mhe. Haji Omar Kheir kwa nchi zinazoendelea si jambo la ajabu, lakini hili deni la taifa linalipwa kwa kodi za wananchi, sasa suala langu je hili deni la taifa ambalo Wazanzibar sote tunadaiwa kila mmoja 137,809/= hayo mambo yaliyokopwa yameleta faida na sisi tunaolipa, au tunadaiwa kiasi hichi lakini hawakunufaika watu wote na imenufaika watu wachache lakini kulipa tulipe sote. Kwa sababu hili deni litalipwa kwa kodi za wananchi sasa suala je, kila Mzanzibar atakayelipa deni hili kafaidika na mkopo huo hilo lilikuwa ni suala jengine.

Lakini sambamba na hilo nina suali nataka niulize siku moja hapa liliulizwa katika Baraza na Mhe. Waziri akalijibu, lakini nadhani alijibu kama ni joki, lakini mimi nauliza kikweli kweli. Mhe. Waziri katika serikali ya Muungano wenzetu kila mwaka wanakuwa wanaeleza akiba ya taifa na mara hii wameitaja kwa bahati mbaya sikuihifadhi katika kichwa changu na sina kile kitabu hapa, lakini wametaja wana akiba kiasi gani. Sasa suala langu je sisi Zanzibar tuna akiba kiasi gani, kwa sababu kumbu kumbu zangu zinanambia

wakati ule nasoma uhai wa Mzee Karume alikuwa akitaja majukwaani kwamba tuna akiba kiasi fulani.

Hata wakati wa utawala wa Mhe. Aboud Jumbe haikuwa siri kwa serikali ya Zanzibar kutaja akiba yake ya kigeni, lakini leo mimi Mwakilishi mzima sifahamu je mwananchi wa kawaida sijui kama atakuwa anafahamu, sasa nadhani kwa kuwa serikali ni yetu sote na hizi ni zama za uwazi ikiwa wazee wetu walithubutu kusema sisi tunaficha nini, kama hakuna pia serikali isione aibu hakuna aibu hapa tuseme tu kwamba hatuna.

Au kama tunazo lakini katika mfuko wa Muungano je hiyo akiba ya muungano iliyopo yetu sisi itakuwa ni kiasi gani au ndio ile ile 4.5. Sasa hili ni suala muhimu watu lazima waelewe masuala ya nchi yao nah ii bajeti ni ya wananchi, kama siku zote tunavyosema kwamba ni bajeti ya wananchi sasa tena isiwezekane kwamba kuna wananchi wanaelewa baadhi ya mambo lakini baadhi yam engine haelewi hii itakuwa sio bajeti ya wananchi.

Halafu jembo jengine ambalo linanichanganya zaidi katika hii bajeti ni kuhusu mapato, Makadirio yaliyokadiriwa ya makusanyo katika bajeti iliyopita tunaambiwa kwamba hata itakapofika mwezi wa Juni, mwaka huu wanakadiria kukusanya 99.9 mimi nasema hiyo ni 100%. Kwamba kile walichokikadiria mwaka jana kwa fedha za ndani basi wanakadiria hata kufika mwezi wa Juni watafikia asilimia hiyo, hapa nimpongeze Waziri wa fedha na watendaji wake wote, *ZRB* na Bodi ya Mapato kwa suala hili hii ni juhudi kubwa wamefanya. Kama kweli itawezekana kufikia analau asilimia 90 basi lazima tuwapongeze sana. Lakini sasa suala langu pesa hizi zimekwenda wapi kwa sababu ikiwa makusanyo tunayokadiria tumefikia 100% sisi ndio tunaopita katika makati, utakuta kuna idara nyengine wamepata *40% other charge*. Wengine wana 50% wengine 60% lakini huku tulichokikusudia chote tumekusanya, sasa hichi tulichokusana kimekwenda wapi au kuna matobo yanavuja. Sasa ikiwa tulichokusudia kukusana na kukitumia tumekipata chote ilikuwa na *other charges* zipatikane 100% kwa amount hii hii ambayo tumeikusanya. Lakini ukienda Utawala Bora Pemba utakuwa wamepata 40% wengine 60% wengine 70% lakini kukusanya tumekusanya 99% sasa imekwenda wapi.

Sasa hii inaashiria mambo mawili kwanza labda kwenye serikali kuna ufisadi na hizi fedha tunazoomba hapa na kuzitumia hazitumiwi kama ilivyokusudiwa, inaonekana kwamba ufisadi hatujaugundua. Au inawezekana kuna matumizi yasiyozingatia kanuni za matumizi na sheria za fedha, sasa jibu atanisaidia Mhe. Waziri itakuwaje fedha tunazokadiria tena za ndani halafu kule kunakuwa na 40%, 50% na 60% zinakwenda wapi, hili mimi linanitia mashaka na kwa sababu juzi juzi nimepata taarifa sijui kama sahihi au sio sahihi hata hivi

karibuni kulikuwa na walimu hewa katika Wilaya moja hapa Unguja, lakini serikali iko kimya kabisa.

Sasa mimi nina wasi wasi na mambo kama haya kwamba ufisadi uwakuta upo ndio kama hili moja la walimu hewa. Mhe. Spika, kuna taarifa kwamba hapa Unguja kuna Mkoa mmoja kuna suala la waajiriwa walimu hewa, sasa nadhani mambo kama haya pamoja na mambo mengi ambayo yatakuwa yapo serikalini lakini sisi hatujajipanga kupambana na ufisadi. Sasa kama hatujajipanga kupambambana na ufisadi nadhani mambo kama haya yatakuwa yanakuja.

Mhe. Spika, sasa nataka nizungumze suala ambalo Waziri Kivuli na Mhe. Rashid Seif wamelizungumza ambalo msingi wa hoja umo katika bajeti ya Mhe. Waziri, katika changamoto za maendeleo Mhe. Waziri kataja nyingi lakini moja wapo ni ongezeko la watu, kwa kweli hili suala tunapolizungumza linaleta kama taswira ya kisiasa lakimi mimi sizungumzii katika taswira ya kisiasa lakini nazungumzia katika taswira ya uchumi, kama alivyozungumza Mhe. Rashid Seif nah ii sio mara yangu ya kwanza kulizungumza hata baraza lililopita mimi nimelizungumza, kwamba haina maana kwa Wazanzibar kupanga uzazi. Kwa sababu ikiwa nyie mnajipangia uzazi kwamba muwe kiasi katika nchi ili uchumi wan chi uweze kutosheleza mahitaji yenu, lakini leo milango imefunguliwa watu wengi kupita kiasi serikali inashindwa kugharamia wananchi wake.

Mhe. Spika, pana kitu kimoja hapa hatujakigundua inawezekana wenzetu wa Bara wakaja na hoja kwamba na Wazanzibari huku wapo zaidi Wapemba wako wengi ni kweli, lakini Mhe. Spika, nataka nikupe habari moja pale Dar es Salaam wafanyabiashara wakubwa ni Wazanzibari kwa hivyo pale Dar es Salaam kama utasema Wazanzibari ondokeni serikali inaweza kupooza, kwa sababu walipa kodi wakubwa pale Dar es Salaam, lakini hawa wenzetu waliokuwepo hapa wanalipa nini.

Mimi na wenzangu tulimtembelea Mzanzibari mmoja pale ana viwanda nilikuwa na Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Hamza Hassan wakati huo hajawa waziri tulikuwa kamati ya fedha. Kuna Mzanzibari mmoja ana makampuni pale wanalipa bilioni nne serikalini kwa mwezi kodi yao, anatwambia analipa milioni mia tatu *TANESCO* sasa Mzanzibari kuweko Bara ni *products.* Kwa hivyo ukisema uwaondoe pale unaua uchumi wako, lakini jee sisi waliokuwepo hapa wanasaidia kukuza uchumi.

Kwa sababau zamani wenzetu wa kibara walikuwa wanasaidia kukuza uchumi hasa Pemba ndio waliokuwa wakitumikishwa kulima mikarafuu, Unguja minazi lakini leo hao hawafany kazi hizo waliokuwepo wengi kazi zao ni kutembeza vibomba vinavyopiga kelele nauza nini, lakini mali aliyokuwa nayo

haifiki hata shilingi mia tano anayotembeza lakini kila pahala vimeenea. Sasa utakuta wale hawazalishi kitu wala hawalipi kodi wale na hawa dada zetu wanaosambaa samba hivyo nadhani biashara wanayoifanya wale usiku haitozwi kodi, kwa sababu biashara yenyewe haramu ya siri.

Mhe. Spika: usije ukasema inafanywa kwa kificho. *(Kicheko)*

Mhe. Haji Faki Shaali: Lakini Mhe. Spika, nataka nije kwenye hoja ya msingi ya Mwalimu Nyerere wakati wa kuunganisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sababu ya kuibakisha Zanzibar ibakie na serikali yake ni kwamba itakuja kupotea, pamoja na yote aliyokuwa nayo lakini anasema Zanzibar itakuja kupotea kwa hivyo tuiachie na Serikali yake. Sasa hivi inatajwa kisiasa Zanzibar lakini ikishakufa kiuchumi halafu itapotea kwa kisiasa kwa hivyo nadhani hiyo ni changamoto lazima tuweke taratibu nzuri, lakini ukweli hali inatisha sana.

Mhe. Spika, jengine ni katika utekelezaji wa mpango sasa hapa napo nina masuala mengi ya kuelimishwa, katika mwaka uliomaliza wa fedha 2008/2009 serikali ilijipangia miradi 63 na program 20 utakuja jumla ni 84, fedha zilizopangwe zilikuwa ni bilioni 192, milioni 273.8 ambazo kati ya hizo SMZ ilikuwa itoe bilioni 18, 522 ambazo ni sawa na 9.6%. Sasa hapa pana mambo mawili kwanza ule utegemezi watu kama walivyozungumza wenzangu unajitokeza kwamba ni mkubwa, lakini hilo hasa sio shabaha yangu kuzungumza ninachotaka kuzungumza kwamba katika haya makadirio ya mwaka jana pesa iliyopatikana ni 32% tu ya makadirio. Kwa hivyo hii miradi 20 na program 23 pesa iliyopatikana ni 32%.

Mhe. Spika, mimi suala langu ni hapa ikiwa program 20 na miradi 63 ya mwaka jana haikupata pesa na pesa iliyopatikana ni 32%, lakini na leo tena tunakwenda kufanya program 20 na miradi 63 huoni kamba bajeti yetu itakuwa ni bajeti hewa isiyotekelezeka. Kwa sababu kama miradi yetu ya mwaka jana angalau tungeitekeleza kwa 6% halafu ukaja tena na miradi hii 63 na program 20 ingeingia akilini, lakini yale ya mwaka jana hujapata kitu halafu unakwenda kutekeleza program 20 na miradi 63 huoni kwamba hii bajeti siyo halisi ni bajeti ya kujidanganya. Sasa nadhani bora tupange mambo machache ambayo tunaweza kuyatekeleza kuliko kupanga mambo mengi tusiyoyatekeleza itakuwa tunajidanganya na mtu mzima hajidanganyi mwenyewe.

Mhe. Spika, jengine nizungumzie juu ya habari ya vichocheo vya ukuaji wa uchumi Mhe. Waziri kavitaja vingi, lakini kuna kimoja kakisahau sasa nashkuru Mhe. Waziri Kivuli yeye kakikumbuka na mimi nakikumbuka kwa sababu ni suala la tatu katika utawala bora ya MKUZA. Mhe. Spika, katika MKUZA kuna utawala bora kwa sababu nchi haiwezi kuendelea kiuchumi

kama hakuna utawala bora hii haiwezekani kwa hivyo utawala bora ndio msingi wa kujengea uchumi.

Leo Somalia huwezi kujenga uchumi kutokana na mashaka yaliyokuwepo, Sudan kuna mafuta na kila kitu lakini nchi inayumba kutokana na matatizo kwa hivyo utawala bora ni suala la msingi, kwa sababu utawala bora ndio unaoleta utulivu na amani, bila ya utulivu na amani huwezi kujenga uchumi hata huko kusali basi utasali kwa wasi wasi wachilia mbali kupanga uchumi. Sasa hili bahati mbaya Mhe. Waziri hakulizungumza lakini nadhani moja katika kichocheo cha ukuaji wa uchumi kwa kipindi hiki ilikuwa ni hali ya utulivu na amani uliopo nchini.

Sasa suala je huu utulivu na amani uliopo nchini tunataka uendelee au tunataka uondoke nadhani jibu kwa kila mtu atataka uwepo, je mambo gani ambayo yanaweza kuvuruga huu utulivu na amani uliopo sasa nadhani masuala kama haya lazima yaje kwa mtiririko. Sasa mimi nataka niungane na wenzangu walioonyesha hofu zao ili kuizindua serikali kwamba mimi nina wasi wasi kutokana na tunavyoelekea kwenye uchaguzi mwakani huu utulivu na amani unaweza kupotea, watalii wakakimbia na sisi badala ya kushughulikia uchumi tukashughulikia malumbano ya kisiasa, tukarejesha uadui nadhani ndiko tunakoendelea. Kuna mambo mtakuwa hamjui labda hamjaambiwa lakini sisi tutakwambieni.

Mhe. Spika, sisi jambo moja ambalo tunaona litatuondolea utulivu na amani katika nchi yetu ni hivi sasa kuna daftari linaaza Micheweni tunategemea mwezi wa saba litaanzia Micheweni, lakini huko Micheweni linakoanza daftari kuna Wazanzibari wengi hawana vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi ambavyo kwa mujibu wa katiba wala havina ulazima katiba ipo wazi kabisa, katiba ipo wazi na sifa za mpiga kura zote zimo kwenye katiba bora niliache nitakuja kuzungumza kwenye utawala bora.

Mhe. Spika, lakini watu sasa hivi hawana vitambulisho vya uzanzibari ukaazi wakienda huwa hawapewi wanazungurushwa, watu wakienda kwa Sheha anasema yeye fomu hana, ukienda kwa Mkuu wa Wilaya anakwambia mimi nimo kwenye kamati ya ushindi wa chama changu siwezi kuruhusu mambo haya.

Ukienda Afisi za Vitambulisho utaambiwa watu waambieni waje huku kweli mtu atoke Konde aje kwa Mkurugenzi kuomba vitambulisho, kwanza sheria ndio inavyosema hivyo kwamba mtu aje huku sasa yote utakuta kuna kuzungushwa zungushwa ili wananchi wazuiliwe haki yao ya kupiga kura. Sasa mwananchi raia ukimfanyia hivyo Mhe. Spika, unadhani ataipenda serikali na utulivu utakuja hapo.

Sasa mimi nawaomba watu wazima waliomo humu ndani, wasomi wanaojiheshimu na wanaoipenda Zanzibar yetu wasiruhusu mambo kama haya ya kitoto kwa ulimwengu wa leo kufanya, leo dunia nzima watu wako Dar es Salaam lakini wanapiga uchaguzi Marekani hata Msumbiji katika nchi za Afrika, yaani ile haki ya kupiga kura kwa raia inamtafuta hata akiwa nje ya nchi.

Sasa leo wewe wananchi waliomo ndani ya nchi yako unawanyima hapo utulivu utakuja kweli, mimi naona hapa kitakachokuja ni chuki, uhasama, uadui, watalii watukimbie tuache kuzalisha tushughulikie migogoro hivyo jamani aibu kama hizi mpaka lini tunaonekana Wazanzibari hatuna akili, hatufahamu mambo kwa nini.

Mhe. Spika, sasa mimi nadhani haya mambo serikali namuomba Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi, Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ wasimamie na wahakikishe Wazanzibari kila mmoja anapata haki yake kama tulivyokula kiapo kulinda katiba hii, kwa sababu hii ni haki yao kikatiba asitokee mtu mmoja akafanya mambo ya kihuni kama haya tukamuonea haya tukammezea mezea nafikiri inakuwa sio vizuri, kwa sababu itakayopakwa matope ni nchi yetu hilo nilikuwa niungane na wenzangu.

Halafu jengine kinachonisikitisha katika bajeti Mhe. Spika, ni mradi wa karafuu mradi huu umetengewa milioni sitini na karafuu bado nasema japokuwa sio mti wa mgongo tena lakini nasema ni uti wa mguu, kwa hivyo kwa vyovyote bado karafuu lazima tuzishughulikie lakini bajeti nzima kwa karafuu unaweka milioni sitini hapa inaonekana bado hatujakuwa makini.

Mhe. Spika, jengine ninaloomba kwa serikali kwa sababu lazima hiki kidogo unachopata katika nchi basi tukitumie vizuri, mimi naomba sana serikali itathmini sana ziara za nje za Mawaziri wetu ni *productive* maana ziara zimekuwa nyingi za nje, je hizi ziara wanazokwenda hao mawaziri zina tija kwetu.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri Kiongozi ziara ambazo hazina tija kwetu asiziruhusu au ambazo wanaweza kwenda maafsa wawili lazima na Waziri awemo, hata safari ya kwenda maafsa wawili watatu basi lazima na Waziri nay eye aingie. Sasa nadhani serikali iwe makini kubana matumizi kwa sababu wafadhili wanaotusaidia na wao wanajibana huko kwao ndio wakaweza kutusaidia ingekuwa wanatumia ovyo ovyo wasingeweza kutusaidia.

Mhe. Jengine pencheni nashukuru serikali ya Muungano imeweka kiwango cha chini cha pencheni ni shs. 50,000/= sasa nadhani na sisi Mhe. Waziri wa fedha namuomba au serikali kwa ujumla kuna wazee wetu waliotusomesha wanapata elfu kumi na tano, kwa kweli mimi naona haya kuna mwalingu wangu siku zote nikipita Changaraweni maalim Hassan ananiita na kunambia tupigieni kelele namwambia kweli lazima tupige kelele, leo eflu kumi na tano mtu katusomesha sisi na amefanya kazi zaidi ya miaka mingapi sijui analipwa elfu kumi na tano basi angalau pencheni tukaitoa katika kiwango cha chini tukafikia angalau shilingi elfu hamsini badala ya hali ya sasa.

Halafu jengine ambalo nataka nilizungumze kwa ufupi ni *suprimentary budget* mimi nina wasi wasi kwamba kuna baadhi ya pesa humu kwenye matumizi ukiziangalia kuna kitabu lakini sijui nimekiweka vipi, lakini kiufipi niseme nitaeleweka kuna baadhi ya miradi katika mapitio ya kiuchumi nimeiona kwamba imetumia fedha zaidi ya ilizokadiriwa, kuna mradi mmoja umetumia zaidi ya *for 100%* lakini sikumbuki hapa kuletewa *suprimentary budget.*

Mradi wa barabara ya Mshelishelini/Pwani Mchangani ambao ziliombwa milioni thamanini lakini zimetumiwa milioni mia nne na sitini na tisa na hili ni suala la kikatiba, kwa hivyo hatuwezi kuliepuka suala ka kikatiba sijui ni ibara ya ngapi ile. Lakini nashangazwa tokea nije katika Baraza hili haijatokea hata siku moja kuletewa *suprimentary budget* wakati hili ni suala la kikatiba kwa nini tuivunje katiba wakati tumeapa kuilinda katiba.

Nadhani iko katika 106 ibara ndogo ya 2(b). Mhe. Spika, sisi tumekula kiapo kwa kulinda katiba lakini katiba tunaivunja na wala hatushughuliki, sasa nadhani jambo hilo tupate maelezo ya kutosha ili tujiridhishe Mhe. Spika,.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nipate maelezo vile vile katika utekelezaji wa *program* zilizopita kuna *program* mbili za mawasiliano laba Mhe. Machano atamsaidia Mhe. Waziri aje kutueleza naona hazikuombwa pesa, kuna program ya ununuzi wa vifaa MDRI na program ya kuimarisha viwanja vya ndege naona hii haikuingizwa pesa kabisa, sasa nadhani labda Mhe. Waziri atakuja kutueleza akisaidiwa na mwenzake.

Nije haraka haraka jengine ni nchi na mashirika yaliyosaidia bajeti yetu nimepiga hisabu ni kama hamsini na saba kwa mujibu wa taarifa ya Mhe. Waziri ambayo wenzetu huwa mnapiga makofi, mimi nimehisabu hapa kwamba jumla ya nchi na mashirika yaliyotusaidia jumla ni hamsini na saba. Sauala langu nyie wenzetu wa upande huo vilevikitajwa mkipiga makofi huwa mnasherehekea kupewa ile misaada , ule utegemezi au mnasherehekea nini.

Mhe. Spika, halafu jengine nataka nitoe rai nimeangalia nyumba za Kengeja karibuni nilikwenda ziko katika hali mbaya sana, nilitegemea kwamba Mhe. Mansour mwenzangu kwa ajili ya kuzinusuru zile nyumba kule zisianguke, lakini nilivyoangalia katika hiki kitabu cha mpango nimeona kamboa pesa milini nne kwa ajili ya nyumba za Mpapa Unguja, sawa sawa Mpapa na Kengeja zote sawa sawa wote ni Wazanzibari wala sina wivu mimi kusaidiwa Mpapa lakini ushauri wangu ili kuzinusuru nyumba za Kengeja ambazo zimejenga na Marehemu Mzee Karume ili kumuenzi naomba zile nyumba tuzinusuru tena katika bajeti hii.

Sasa hapa naomba kidogo nimuombe radhi Mhe. Waziri Kivuli wangu katika ile bajeti yake mbadala nimuombe rani niongeze kitu, zile fedha za miradi ya UKIMWI katika Wizara naomba zikatwe katwe mpaka zipatikane kiasi cha milioni mia nne au mia tano zipelekwe ili zinusuru nyumba kwa sababu UKIMWI kila mmoja sasa hivi ameshaufahamu hapa, kila mmoja mfanyakazi wa serikali ni mtu mwenye elimu, redio zinaelimisha na TV zinaelimisha, vijarida vinaelimisha sifikirii kwamba tukikata programu ya UKIMWI kwa mwaka mmoja kwamba watu watakufa kwa UKIMWI.

Si hivyo watu watakula keki kwa pesa za ukimwi na huku majumba yataporomoka, sifikirii sasa hivi kama kuna faida yoyote ya kutumia pesa za serikali kwa mambo ya UKIMWI kila mmoja anaufahamu hizi ni pesa za watu kutumia tu.

Wala Mhe. Waziri usione kwamba hotuba yako itaharibika kwa kuchukua ushauri huu ambao unatokana na upinzani naomba uachane na mambo kama haya chukulia uzalendo tu, kwamba chukua pesa za UKIMWI tuzipeleke Kengeja tunusuru majengo na Inshaalaah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hakuna mtu atakayekufa UKIMWI mwaka huu.

Mhe. Spika, jengine la mwisho ni swali. Nimekiangalia hiki kitabu cha bajeti kwa umakini mkubwa na ustadi na najua kwamba Mhe. Waziri ana wataalamu wazuri sana. Nimeangalia ukurasa wa 59 Mfumo wa Bajeti kwa Mujibu wa Uwezo Halisi kwa Mwaka 2009/2010. Mimi nasema kwanza si kwa mujibu wa uwezo halisi kwa mujibu wa omba omba, kwa sababu sisi si uwezo wetu huu, lakini hilo silo ninalotaka kusahihisha.

Mhe. Spika, kitu kinachonikanganya Mhe. Waziri hapa anaomba shilingi bilioni mia nne na kumi na mbili, mia sita na tano milioni. Sasa pesa hizi anazoomba Mhe. Waziri ni pesa zetu za ndani na nje (misaada na mikopo), lakini sasa swali linakuja wakati zinapofika bajeti za Mawaziri wanapoomba pesa wao hawaombi pesa za nje wanaomba za ndani tu, ukiangalia mwisho

katika samari ya kile wanachokiomba huwa wanaomba zile za ndani tu hawaombi za nje.

Mhe. Spika, hii itakuwa ni mara yangu ya tatu kuja na hoja hii, lakini Mhe. Waziri bahati nzuri yeye kaomba zote mpaka za nje jumla zimekuja bilioni 412,605 milioni. Kwa hivyo, mimi nampongeza Mhe. Waziri kutuomba tumuidhinishie pesa zote makusanyo ya ndani na nje tunamshukuru, lakini sasa mbona mawaziri hawafanyi hivyo, mawaziti wengine wakifika katika wizara zao huwa wanaomba zile pesa za ndani tu za nje hawaombi.

Mhe. Spika, swali langu, yupi sahihi ni Mhe. Waziri anayeomba tumuidhinishie za ndani na nje au ni Mawaziri wanaoomba tuidhinishe pesa za ndani tu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutukutanisha hapa tukiwa na afya njema na uzima. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa pili kwa kipindi cha jioni kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wiki iliyopita na leo kuanza kujadili tokea asubuhi na kuendelea hadi hivi jioni.

Pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake wote walioandaa bajeti hii ambayo kwa kweli ni bajeti kwa hali yetu mimi nasema ni nzuri na ni bajeti ya wananchi, kwa sababu imejali wananchi wake tangu mwanzo mpaka mwisho. Kusema kwamba bajeti yetu tumeelemea sana kwenye tegemezi, mimi nadhani Waswahili husema, “Mtu hushona nguo kwa kitambaa alichonacho”, ukitaka kushona kanzu ndefu kitambaa kidogo utapata matatizo lazima ukadirie kwa mujibu wa uwezo wako ulionao, hapo utaweza kufanya shughuli zako kwa vizuri.

Mhe. Spika, nimpongeze Mheshimiwa mwenzetu Bi. Asha Moh’d Hilal kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na leo tunae hapa kuwakilisha wananchi wake wa Magogoni namuombea kila la heri na umri mrefu ili aweze kufanya kazi zake vizuri na arithi nyayo za Marehemu Mhe. Daoud Hassan Daud.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa nichangie bajeti yetu hii iliyowasilishwa hivi juzi. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini bajeti hii tunaipokea kwa mikono miwili na naomba wenzangu tuijadili na tuipitishe kwa sababu tukiipitisha bajeti hii ndio kazi zetu zote za mawizara zitaweza kufanya kazi kama ilivyopangiwa. Kwa hivyo, nawanasihi mwenye mawazo yake atoe lakini baadae tuipitishe kwa nguvu zote

ili fedha zilizoombwa zipatikane ziweze kutumiwa kwa kazi za kawaida na hata kwa kazi za miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, bajeti yetu nimesema ni bajeti ya maendeleo kwa sababu imegusa nyanja mbili muhimu sana, nyanja ya kwanza ni ya kilimo. Mhe. Spika, tukikataa tukikubali lakini kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu na sio sisi tu, lakini takriban nchi nyingi za kimasikini wanategemea sana kilimo.

Hapa petu ukifanya sensa ya kutafuta wakulima basi si chini ya asilimia 60 ni wakulima waliobakia asilimia 40 wapo wataokuwa wanafanya kazi serikalini, taasisi za watu binafsi na wanaojitegemea wenyewe kwa kujiajiri. Kwa hivyo, kilimo nimeona kwamba safari hii serikali imekipa kipaumbele na kwa kuweka azma nyingi za kuweza kusaidia.

Kwanza wamekusudia kilimo cha sasa hivi kilimwe kitaalamu tuondokane na kile kilimo cha kizamani, kitalimwa kitaalamu vipi? Wameeleza kwamba watasaidia nyezo ikiwemo matrekta. Matrekta yanasaidia sana ukulima, jembe la mkono na trekta ni tofauti sana. Kwa hivyo, serikali imeweka mkakati wa kuongeza matrekta kwa lengo la kusaidia wananchi wetu katika kulima.

Pili pia serikali imepunguza bei ya mbolea ama wengine wanaita pembejeo. Hii pia ni kuwasaidia hao hao wakulima waweze kulima eneo dogo lakini watumie mbolea ili waweze kupata mazao mengi. Pamoja na mbolea hiyo, lakini pia sasa hivi serikali ina kitengo cha kutafuta mbegu bora na tayari zimepatikana, ziko mbegu za muhogo si chini ya aina 100 moja tafauti na sasa hivi ziko za mpunga pia wanapewa wakulima wetu wanaweza kulima na wanapata mbegu bora basi atapata chakula kilichokuwa kizuri, aweze kulima aweze kupata chakula chake na kidogo auze. Hivi sasa kuna wataalamu wengi na mpaka mabwanashamba na bibishamba, hawa pia lengo la serikali ni kuwafikisha kwa wakulima ili waweze kusaidia kilimo hicho na wafakie yale malengo yaliyokusudiwa. Sasa kwa maelezo hayo mimi naunga mkono sana serikali ifanye jitihada hayo wanayoyazungumza basi wayatekeleze ili tuweze kufikia kwenye malengo.

Suala la pili pia limezungumziwa na kupewa umuhimu mkubwa ni suala la utalii. Utalii ni zao mbadala la zao la karafuu, nazi huko nyuma na mambo mengine. Hivi sasa utalii unapewa kipaumbele na serikali yetu kwa lengo la kuweza kusaidia uchumi baada ya kuona zao letu la karafuu linaanguka na sasa hivi limeingia ushindani, kwa sababu mwanzo ilikuwa karafuu zinalimwa Zanzibar tu peke yake Unguja na Pemba, lakini sasa hivi kuna nchi si chini ya nane mpaka kumi zinalima zao hilo na kwa ushindani mkubwa. Sasa serikali naiunga mkono kuweka umuhimu mkubwa katika utalii.

Nimeisoma bajeti wamesema malengo makubwa ya kuimarisha utalii moja watakiimarisha chuo, hilo tayari wameshapatikana watu wa kuweza kukiendeleza chuo kile kwa majengo lakini pia wanatoka kwenye ngazi ya cheti na sasa wanaingia kwenye ngazi ya *diploma* na ngazi ya *degree* ili wasiwe na zogo la kutafuta *PO* kutoka nje ya nchi yetu.

Nadhani wakishafika ngaiz ya *degree* basi *PO* watatoka hapa hapa na tutapata ajira kubwa ya wazalendo katika kuimarisha hilo. Pia mtalii hawezi kwenda kwa chuo tu cha utalii kuweza kupata wataalamu, lakini lazima kuna nyezo ambazo serikali imeziainisha kwenye bajeti hii zitekelezwe hizo ili ziweze kusaidia utalii kukua.

Moja kiwanja cha ndege. Kiwanja cha ndege hivi sasa kimewekewa mkakati wa kutengenezwa ili watalii wakifika pale waweze kujua tumeingia kwenye sehemu nzuri na tunaweza tukatembea bila ya tatizo lolote. Kwa upande wa barabara vile vile imewekwa mikakati kwamba barabara nyingi zitengenezwe ili watalii wakishashuka wende wanakotaka kwenda katika hali nzuri na waridhike na yale maandalizi na miundombinu tuliyonayo. Pamoja na hayo barabara na uwanja wa ndege, lakini pia imewekwa wazi hivi sasa kwamba tayari wenzetu wengi wanaowekeza hapa petu wanawekeza utalii wa daraja la kwanza kabisa.

Hapo mwanzo ilikuwa hoteli zetu nyingi ni madaraja madogo lakini sasa hivi tayari wenzetu wana hoteli nyingi za daraja la kwanza na tunapata wale watalii wenye sifa, vishuka wanakuja kwa upande wao lakini pia kutokana na maandalizi haya tunapata watalii waliokuwa wazuri na tunapata kipato kilichokuwa kizuri. Sasa naipongeza serikali kwa hilo kwa sababu mambo kama hayo yamekuwa mazuri na yanaweza kusaidia katika kuendeleza.

Jengine tatizo kubwa la nchi yetu ni suala la umeme. Kipindi cha nyuma muda wa miezi miwili mitatu tulipata tatizo la umeme, lakini bajeti pia imeeleza kwamba tuna mradi tayari umekamilika nap engine mwisho wa mwaka huu utakamilika wa kuleta *line* mpya katika Kisiwa chetu cha Unguja na *line* nyengine inayotoka Tanga inakwenda Pemba. Nadhani na Pemba nako ukishafika umeme hoteli nyingi wawekezaji watakwenda kuweka kwa sababu tatizo kubwa kule ni umeme. Kwa hivyo, zile hoteli mbili tatu zilizoko ukifika umeme zitaongezeka.

Kwa upande wa hapa Unguka nilikuwa namuomba Mhe. Waziri pamoja na kupongeza nina swali kidogo atapokuja anipe maelekezo. Umeme huu tayari wa kutoka Raskiromoni kuja hapa Unguja umeanza hatua ya kwanza kwa kupita kufanya *survey* wale watu wa mradi na tayari umepita kuangalia line sehemu utamopita. Sehemu moja imegusa eneo la Amani na pale Amani mimi

ninaishi na majirani wengi sana na tayari wametiliwa X watu wale kwa kuelezwa kwamba sehemu ile itapita *line* itabidi wahame watafute maeneo mengine na tathmini nadhani tayari inafanywa.

Nina swali dogo nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu hili nimetumwa nitataka nipeleke jibu sasa akinijibu itakuwa vizuri zaidi. Watu waliojenga pale walinunua viwanja na wakajenga nyumba, lakini sasa hivi thamani inayotiwa ya mtu nyumba anayoishi sio kiwanja. Sasa je, wale wataovunjiwa pale wakishalipwa fedha zao serikali itawasaidia viwanja? Ama katika makisio hayo vitakuwemo na viwanja kabisa kwa sababi hilo ni tatizo kubwa.

Vile vile fedha zitakazotolewa zitakidhi haja na ujenzi wa nyumba za hivi sasa kwa sababu tumebaini sana kwamba mashirika yakitia thamani huwa hayasikii ile thamani ya mtu aliyejenga ile nyumba. Sasa tunaomba na hili kama serikali itakuwa na wataalamu wao washirikiane na taasisi ile ili tuone wananchi wa eneo lile wanapata haki zao kamili na wanaweza kuishi kama hapo mwanzo.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye utangulizi huo nije kwenye ukurasa wa 15 kifungu 26, hapa panazungumzwa biashara za nje ambazo zinafanywa na nchi yetu na kuuza nje. Hivi sasa ni biashara mbili zilizotajwa katika kitabu hiki ikiwemo karafuu na mwani. Nataka nitoe maelezo kidogo ya mawazo yangu halafu kama yatakuwa yanafaa basi serikali itusaidie.

Kwanza nizungumze suala la mwani. Hivi sasa mwani unanunuliwa na kampuni za watu binafsi na hao ndio wanaotafuta masoko nje wakauza. Mwani ukianguka bei nje nay eye huku anaangusha bei nap engine wala haununui na unaharibika. Sasa ushauri wangu serikali ingefanya taratibu ikatafuta taasisi ama shirika ikaweza kununua huu mwani pale unapokuwepo ukawepo, likiweko soko ukawa unauzwa. Kwa mfano kama karafuu, sasa hivi karafuu kama itazaliwa na itachumwa basi itanunuliwa na itahifadhiwa likipatikana soko inauzwa nje. Sasa ningelishauri kwa kuwa sasa hivi kinamama wengi wamejitokeza katika kulima mwani kuendesha maisha yao basi ningeishauri serikali kutafuta utaratibu wa kuweza kutafuta taasisi ikanunua mwani huu na wakati kukiwa hakuna bei ukahifadhiwa na pale bei ikipatikana basi ukauzwa.

Kuhusu karafuu pia na mimi nishirikiane na wenzangu walioanza kuzungumza kwamba bado karafuu pamoja na kuwa zao hilo limeanguka lakini bado linatufaa na wananchi wengi hususan Pemba zao hilo ndilo wanalotegemea kufanyia shughuli zao kama ujenzi wa nyumba zao, maisha yao, ununuzi wa mifugo wakati wa msimu hasa wa karafuu pamoja na matatizo yote. Kwa hivyo, ningeliomba serikali ikaweka kipaumbele suala zima la karafuu kusaidia upalizi, kutoa miche mingine ili wananchi waweze kupanda na zao hili lisipotee, kwa sababu bado linatusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nikimaliza habari ya biashara za nje nije ukurasa wa 14 hapo wenzangu wamezungumza lakini na mimi nataka nitoe mawazo yangu. Kwanza niipongeze serikali juu ya suala zima la kuwalipa wastaafu wengi ambao sasa hivi waliobakia ni wachache mno. Lakini pamoja na hayo, nipongeze hapa hapa serikali kwa kuweza kuongeza mishahara ya wafanyakazi kutoka shilingi 80,000 kwenda 100,000.

Mhe. Spika, naomba hili serikali pia izidi kufanya jitihada ikiwa itawezekana japo haujafika mwisho wa mwaka basi kuna uwezo wa kuweza kuongeza mshahara wangefanya utaratibu wowote wakaongeza. Kwa sababu shilingi laki moja kwa kipindi hiki ni pesa ndogo sana, kwa hivyo kwanza tunapokea kilichotolewa lakini bado serikali isichoke kusaidia wananchi wake.

Kwa upande wa wastaafu kumezungumzwa kwamba sasa hivi pencheni ya mwisho mtu anapata shilingi elfu kumi na tano ni ndogo mno. Sasa huko nyuma nilisikia kwamba ziko nchi nyengine pencheni watu wanafanyiwa *package* moja analipwa kama milioni nane au tisa anakadiriwa tu kwamba huyu kastaafu mika sitini anaweza kufa kwenye miaka thamanini akapewa donge lake la milioni kumi na tano akafanyia shughuli zake.

Sasa nadhani pia nimuulize Mhe. Waziri labda hili lilifanyiwa utafiti likafeli kwa hapa kwetu au bado limo ndani ya utafiti ili wale wote wanaolipwa pencheni wasiwe wanakwenda kila mwezi, wafanyiwe utaratibu wakusanyiwe chao wapewe wajue mawili kama watarithiwa au watatumia mpaka kufa. Sasa hili nalo namuomba Mhe. Waziri kama tulilijaribu na likatushinda basi tupate jibu la kama limo kwenye process si vibaya pia akatwambia.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 19 kifungu cha 35 Makusanyo ya Mapato ya Serikali *ZRB* na *TRA.* Kwanza nishukuru kwamba wenzetu hivi sasa wanajitahidi sana katika kukusanya, imeoneshwa humu malengo waliyojiwekea na kima walichokusanya kwa kweli wamejitahidi sana. Sisi tuna wajibu wa kusaidia ukusanyaji wa mapato kwa sababu wengi tunaonunua vyakula madukani huwa hatuchukui risiti. Sasa ningeshauri na sisi pia tukasaidia serikali yetu kuwaelekeza kuwa sisi tukinunua kitu tuombe risiti pamoja na wananchi wetu kwa lengo la kulinda mapato yetu.

Lengo la kuzungumza hapa nilikusudia kwamba zaidi kuna mapato mengine yanapotea nadhani serikali pia ingeweka jitihada wakaweza kuyakusanya mapato hayo. Ziko kodi nyingi nyengine zinachangishwa na mawizara kusaidia katika mapato ya serikali. Nadhani mfumo ulioko sasa hivi tungeubadilisha tungepata fedha nyingi zaidi.

Kwa mfano Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira mimi napita kama kamati kufuatilia maendeleo yake. Sasa Wizara ya Kilimo utakuta wenyewe wanasema wanajiwekea lengo mfano mwaka huu watakusanya milioni kumi na mbili, lakini ukienda utaambiwa tumevuka lengo pengine mara mbili. Sasa mimi huwa nafanya wasiwasi.

Mimi nitakuwa na mtoto nyumbani tunakwenda kondeni namuuliza utalima matuta mangapi? Atanambia nitalima moja kwa sababu hataki kujisumbua, mimi niliyelima mengi nitakuwa najitahidi mwenyewe nitakuwa najisumbua. Sasa wizara kuiambia ijipangie lengo wenyewe atatafuta kima ambacho anaweza kukusanya kwa muda mfupi. Nadhani serikali ingeangalia utaratibu na kutafuta wataalamu kwa kila wizara ikatizamwa hasa kwa mapato haya wizara hii ikadiriwe kukusanya kiasi fulani kusaidia mfuko wa serikali.

Kwa mfano tulipokwenda machinjioni Kisakasaka, kule ng'ombe anawekwa karantini wiki nzima unalipa shilingi 300 wakati ng'ombe yule mtu anamnunua kwa shilingi laki tano, kuchinja shilingi 700 wakati shingo tu ya ng'ombe mtu anauza elfu 50. sasa nadhani mapato kama yale yangeangaliwa na sheria ya pale nafikiri ipo muda mrefu sana, ng'ombe yupo wiki nzima anakaa pale unamlipia shilingi 300, pale pana walinzi wanalipwa mshahara, akiibiwa mmoja mnalipa, kuna dawa zinatumika za serikali kuangaliwa afya zao mpaka inaonekana wako sahihi ndio wanauzwa. Sasa nadhani hiyo ni mifano michache ninayotoa ya kuweza kusaidia.

Hata *parking* za mjini hizi, *parking* hapo Darajani kwa mwezi unaweza kukusanya mabilioni ya pesa lakini hakuna utaratibu mzuri vile vile na maeneo mengi gari zinakaa inaweza ikaanzishwa mapato yakasaidia serikali. Naiomba wizara ingekaa na wataalamu wake ikazidi kufikiria njia mbali mbali za kuweza kuongeza mapato katika serikali yetu. Kwa hivyo, kwa upande wa mawizara ndio hilo nililolizungumza.

Halafu pia nashukuru kwamba katika hotuba hii kumezungumzwa kwamba kutaanzishwa kodi za majengo ambapo sheria tayari tumeshaipitisha nadhani na hii itasaidia ikisimamiwa vizuri katika kukuza mapato ya nchi yetu, lakini kama haikusimamiwa basi hatutofikia lengo tulilolikusudia.

Pia kunataka kuanzishwa kodi mpya za ardhi. Nadhani hivi sasa wawekezaji wengi wanakuja kwetu kuwekeza kwa kuwa wanaona wanapata bei ndogo sana katika uwekezaji. Sasa kwa kuwa serikali imebaini hilo naomba na hili lisimamiwe vizuri ili tuweze kufika kwenye lengo tulilokusudia, vyenginevyo litabaki kwenye maandishi lakini tulilokusudia haliwezi kupatikana. Kwa

hivyo, nashauri hili pamoja na majengo yasimamiwe ili tuweze kupata fedha za kutosha na kunyanyua mapato yetu.

Nikiendelea nije ukurasa wa 30 kifungu nambari 57 hapa inazungumziwa miradi midogo midogo ya wananchi. Kwanza niipongeze serikali kwa kuiunga mkono miradi hii na kila mwaka wanatenga fedha za kusaidia miradi hii. Tatizo lililojitokeza hapo mwanzo naona safari hii kidogo limerekebishika.

Mwanzo ilikuwa unaweza kupeleka mradi pengine wa milioni 6 lakini utakuta kwa mwaka mzima milioni sita zile unapata kidogo kidogo Januari milioni moja, Aprili milioni moja, Juni milioni moja mpaka Disemba unamalizia, sasa mradi unakuwa unachukua hatua ndogo ndogo kumalizika. Sasa tunashauri safari hii kwa kuwa fedha zimetiwa wizara ikae ipange majimbo yote yanajulikana 50 itizame kwa mwezi wa Januari mpaka Machi tupate majimbo mangapi ili mtu anapewa pesa anaweza kumalizia mradi wake.

Vile vile hapo itabidi ifanywe taratibu majimbo yote yaneemeke kwa sababu kuna majimbo unamalizika mwaka hawajapata kitu na miradi wanayo. Sasa ningelishauri hili kwa nia nzuri serikali imefanya basi pia walitekeleze kwa nia nzuri. Ufanywe utaratibu wa kugawa kila majimbo kuanzia Januari mpaka Machi mangapi yapewe pesa, Aprili/Mei mangapi mpaka tunamaliza ili ile azma ya miradi ya wenzetu ikisha basi na majimbo mengine imalizike na ule msaada wa serikali tuupate wakati uliokuwa ndiwo.

Mhe. Spika, baada hayo sasa nije ukurasa wa 44 kifungu 82 hapa pamezungumzwa kuhusu msukosuko wa kiuchumi katika dunia. Hivi sasa sote tunajua kwamba dunia nzima imepata msukosuko wa kiuchumi na bajeti yetu pia imeliona hili na kuweza kuweka mikakati maalum ili kuweza kujihami na tatizo hilo. Mikakati hiyo imekusudiwa zaidi kwa sababu sekta zilizoathirika hapa kwetu na msukosuko wa uchumi moja ni utalii.

Sasa serikali imeliona hilo na imefanya sasa hivi iweze kufanya na utalii wa ndani si lazima kutoka nje tu, kwa sababu utakuta sisi wenyewe humu ndani inawezekana kwamba mtu akaambiwa kuna historia fulani Nungwi mtu anaweza kuanza mwaka wa kwanza mpaka akafika miaka 50 hajaiona labda asome kwenye magazeti.

Sasa ni utaratibu mzuri kushawishi na kuelimisha wananchi wetu kwamba na sisi humu ndani tunaweza tukafanya kazi ya utalii sisi wenyewe binafsi, unaweza ukenda ukaangalia msitu wa ngezi nasikia kuna tumbili wa aina ya peke yake ambao hapa Unguja hawapo ukenda kama Mzanzibari basi utakuwa umeongeza kitu katika nchi yako.

Pia mtu anaweza kutoka Pemba akasema kwetu kuna tumbili akasema Unguja kuna kimapunju akasema niende Jozani kuangalia, sasa haya yakiendelezwa yatasaidia na utalii wa nje utakuja kuendelezwa. Nadhani huu ni mpango mzuri na naomba usimamiwe vizuri ili tuweze kufikia hatua iliyokusudiwa.

Nikiendelea hapa nina swali dogo kwa upande wa wizara nimuombe Mhe. Waziri pengine atapokuja kufanya majumuishoa basi anisaidia kunipa jibu kama lipo kama halipo itakuwa basi.

Mhe. Spika, kutokana na msukosuko huu wa kidunia nchi nyingi za dunia ya tatu kama sisi masikini wamepata midaada mbali mbali ya kifedha na wakati mwengine ya nyezo ili kusaidia na kujiweka sawa kwenye uchumi ulioathirika. Je, na sisi katika nchi yetu kupitia pengine Tanzania kwenye mwamvuli mkubwa tumepata chochote na sisi cha kusaidiwa juu ya suala hili? Kama jibu lipo naomba nije nipewe.

Pia hivi karibuni kwa bahati mbaya na masikitiko makubwa wenzetu Bara walipata maafa ya kuripuka mabomu, watu wengi wameathirika, makaazi, vifo, tunawapa pole, lakini na sisi tumepata maafa ya aina mbili, tumepata Pemba kwa kuungua Boti la MV Amana na hapa kwetu imezama boti ya MV Fatihi. Sasa vile vile wenzetu waliweza kupata misaada ya kuweza kusaidiwa pengine mali zilizopotea na kuweza kujikimu kwa wale waliopata misiba. Je, na sisi tumepata msaada wowote pengiine kutoka nje ama wenzetu kama wafanyabiashara? Kama kimepatikana chochote watu wa serikali wanasikia basi watueleze na sisi ili na wenzetu waliopata maafa hayo waweze kupata faraja kidogo.
Mhe. Spika, nikiendelea kwenye mchango wangu nije ukurasa wa 47 kifungu 88 nadhani nimalizie kwa sababu wenzangu wako wengi wanaotaka kuzungumza. Hapa pamezungumzwa mwelekeo wa mpango wa maendeleo wa 2009/2010, na hapa kazungumza Mhe. Waziri naomba ninukuu kidogo, “mpango huu bado unaendelea kuzingatia dira 2020 na mkakati wa MKUZA”, nadhani hii ndio dira yetu ya muda mrefu kwamba ikifika mwaka 2020 basi mengi tuliyoyapanga katika mikakati yetu yaweze kutekelezeka.

Hili nalipongeza na imeelezwa kwamba safari hii katika msimamo huo serikali imetenga shilingi 4.7 milioni kugharamia programu 22 na miradi 65 ya maendeleo kwa mwaka 2009/2010. Hii imeonesha ni ongezeko la asilimia 22.3 milioni sawa na asilimia 119, nadhani suala ni zuri na naomba serikali itekeleze mkakati huu iliyouweka kwa lengo la kufikia azma iliyowekwa.

Lakini pia imeelezwa mwisho na kukusanya shilingi 412.605 milioni na kutumia shilingi 172.692 milioni kwa kazi za kawaida, kazi za maendeleo

shilingi 239.914. nadhani hizi zote katika njia hii ya kupeleka mbele uchumi wetu kitaifa.

Mhe. Spika, mwisho katika hotuba yangu nisisitize kitu kimoja ambacho pia nimekiona kwangu mimi ni athari lakini sijui Mhe. Waziri atatwambiaje. Nimesoma katika taarifa iliyopita mwaka jana kulikuwa na misamaha mikubwa sana ya kodi katika vitu mbali mbali, nilipouliza niliambiwa vyengine vitu vya misikiti, vitu vya maendeleo, lakini si chini ya bilioni saba kwa mwaka mmoja zimesamehewa kwa mambo mbali mbali.

Sasa ningelishauri Mhe. Waziri angelitizama utaratibu mwengine ili mambo mengine tukayafumbia macho, kwa sababu nchi ndogo kama hii tunasamehe bilioni saba kwa mwaka ni pesa nyingi sana. Naomba na hili Mheshimiwa wakae na wataalamu wao yale mambo ambayo si muhimu basi watoe japo tumbaku ili iweze kusaidia katika kuendeleza nchi yetu.

Mwisho niipongeze Wizara ya Kilimo kwa kuunda kamati ya kuweza kusaidia maendeleo ya kilimo katika nchi yetu. Kwa kumalizia hayo mimi mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini baada ya hayo mawazo niliyotoa naiunga mkono bajeti hii ya serikali ya mwaka 2009/2010 kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kwa kuweza kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa kuongeza kima cha mshahara kuwa juu zaidi kutokana na kima chini cha shilingi 80,000/-. Mhe. Spika, hapa kidogo mimi nimeingiwa na wasi wasi kutokana na hiki kiwango kilichoongezwa na serikali. Tukiangalia na hii bajeti yetu ya leo tunayoendelea nayo kuichangia, Mhe. Waziri alitwambia kuwa ongezeko hili litafanya kazi katika kipindi cha mwezi wa Oktoba kwa ongezeko la shilingi 10,000/- na Januari kwa ongezeko la shilingi 10,000/-.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, ongezeko hili jipya kwenye bajeti hii limo? Kama halimo je, kuna uwezekano wa kufanywa bajeti ndogo? Kama hakuna suala hilo kwa nini Mhe. Waziri asitwambie ongezeko hili linafanyika Julai kuliko kufanyika mwezi wa Januari. Hapa ndipo penye wasi wasi wangu kwa hii shilingi 10,000/- ilivyoongezwa. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje kunifahamisha pengine ulimi hauna mfupa aliteleza kusema Oktoba labda Julai itaweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, nitachangia mambo ya jumla jumla. Mhe. Spika, Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia suala la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu malimbikizo ya watu wanaopeleka vyakula kule na akaeleza kwamba vyakula havitoshi. Lakini Mhe. Spika, hasa tukiangalia wizara hii naona hatujaitendea haki kutokana na wizara kuwa kubwa na ni muhimu sana.

Mhe. Spika, katika kipindi cha nyuma kulitokea tatizo la jiko la vitu vya kuchemshia vifaa vya operesheni liliungua na ilichukua muda mwingi sana na walihangaika kila baadhi ya pembe ili kupata fedha zile na walishindwa, wakawa na jiko dogo tu ambalo la dharura. Mhe. Spika, hili suala bado linasikitisha sana.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunasema kuwa ni mwokozi kwa binadamu kma tunavyoizungumza kilimo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zamani ilikuwa ina wagonjwa wachache na ilikuwa inakidhi haja kutokana na jengo lile wakati huo wa kikoloni maradhi yalikuwa kidogo kwa sababu vyakula vyao vilikuwa *standard*. Lakini sasa hivi kutokana na vyakula vibovu wagonjwa wameongezeka jengo lile ni dogo. Mhe. Spika, nilitegemea mimi kwenye bajeti hii ningeona suala hilo la kujengwa jengo jipya na ambalo linakwenda na wakati. Lakini sijaona kitu hiki kuzungumzwa kwa kina hasa.

Mhe. Spika, hivi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuna baadhi ya vitu kwa mfano *ultra sound*. Kuna *ultra sound* moja sasa hivi haina kioo haioneshi vizuri, utaikuta pale imefunikwa kitambaa mashine nzima lakini kioo tu ambacho kinagharimu shilingi milioni 6 leo tunaweka pale iharibike au spare ichukuliwe vitu itiwe kwengine. Kwa kweli Mhe. Spika, bado tutakuwa tunaiumiza wizara.
Mhe. Spika, ilivyokuwa ile wizara ina wataalam wengi sana mimi nilifikiria kutokana na hili ongezeko la mishahara na wao tungeona ile hali ambayo madaktari, wauguzi na watoa huduma jinsi gani ambavyo hii nyongeza na wao ingewasukuma vizuri. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna kilio kikubwa sana kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hususan hawa wafanyakazi wake ambao ni wenye taaluma.

Mhe. Spika, hivi karibuni mimi nilikuwepo hospitali ya Muhimbili nikajaribu kuwauliza wale ma-*orderly* jinsi gani mishahara yao inavyokwenda. Kwa bahati nzuri utakuta orderly mshahara wake ni sawa sawa na wauguzi wanaofanya kazi katika hospitali yetu. Mhe. Spika, ipo haja sasa hivi tuione Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kuweza kuisaidia kwa hali na mali ili angalaua twende na lile jina la rufaa kwa utaratibu wake.

Mhe. Spika, tunakuja kwenye kilimo tumekisema sana leo kuanzia asubuhi kuieleza hali halisi kilimo lakini narudia kusema kwamba hatujawa *serious*

katika kilimo. Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira bajeti yake ni ndogo tukitaka tusitake. Lakini humu kwenye kitabu sijaona ile misaada ya mikopo kwa wenzetu wa Tanzania Bara kupitia kilimo, sikuona chochote kinachoeleza kuwa na sisi angalau tunapata asilimia fulani na ongezeko la kuja kwetu sisi katika hii mikopo. Sasa nikajiuliza tutawezaje leo kilimo hiki kuweza kukiinua na likawa ndio pato kubwa la taifa letu.

Mhe. Spika, kilimo si kitu cha masihara. Mhe. Spika, sasa hivi wenzetu Bara wamejaribu kuunda mbinu na sisi lazima tukubali tuunde mbinu. Mhe. Spika, wenzetu Bara wameruhusu mashirika ambayo wenye uwezo wa kununua matrekta waje kuwakopesha wakulima. Mhe. Spika, sisi mpaka leo hapa Zanzibar bado tuna kile kijembe kongoroka alichosema Mhe. Ali Suleiman Ali cha mwinamo. Kweli kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu kinatuumiza mgongo lazima uiname unapotaka kulima. Mhe. Spika, kwa kweli hatujawa tayari kwa sababu tungekuwa na programu nzuri ya kilimo na tumekusudia hasa kutaka kukiinua kilimo na ziko taratibu nyingi ambazo tuna uwezo wa kuweza kukiinua kilimo.

Kwa sababu jambo la kwanza lazima tuwe na mashirika ambayo yana uwezo wa kuwakopesha wananchi wetu matrekta kwa mkopo nafuu. Hapa mimi ningesema kwamba tayari kilimo tunakiweza. Lakini ikiwa tunasema tu kilimo, kilimo, kilimo, kitatuua. Ukiangalia ukurasa wa 11 kuna usambazaji suala la mbolea. Mhe. Spika, mbolea wanapata watu wachache kilimo hicho kimefaidika wapi. Madawa ya magugu wanapata watu wachache kilimo hicho tumekisaidia wapi. Tungekuwa na utaratibu wa wilaya na mikoa.

Mhe. Spika, kwanza katika hizi shehia tayari kuna kamati za kilimo lakini utakuta hazishirikishwi katika huu uendeshaji wa suala la kutoa mbolea, masuala ya kupewa dawa za magugu hawashirikishwi. Kwa mfano kule kwetu wanaambiwa nendeni Sakafuni ambapo kwa wengine inakuwa ni masafa marefu, hata wanapoamua kwenda wanakuta kule mbolea imekwisha na dawa ya magugu imekwisha.

Sasa hivi dawa ya magugu utakuta huko nje zinauzwa kwa ulanguzi kwa sababu watu wa Bara wanakuja kuzinunua ni ghali, sisi tunauziana kwa bei ya chini lakini baadae inauzwa kwa njia ya mlango wa nyuma ni ghali. Sasa leo tunakisema kilimo itakuwa tunaimba kwenye mdomo tu lakini kwenye kutekeleza tunashindwa, tunakieleza vizuri halafu katika utekelezaji tunakwama. Huo ni ukweli.

Kwa sababu sisi wengine tumeshakuwa na ujuzi wa masuala ya kilimo kutwa tunaingia kwenye mabonde kuangalia na uwezo tunao hapa Zanzibar wa kupanda mpunga bila ya kununua pahali popote kama tutakuwa *serious*.

Mabonde tunayo lakini ukosefu wetu sisi ni vitendea kazi hili lazima tulikubali, bado tuna system ya zamani tu ya jembe, japo tunayatoa lakini tutafanya nini. Hebu tuambiwe leo kuna sehemu ya kukopa matrekta kama hatukugeuka waheshimiwa tukenda kukopa matrekta tukawapa wananchi wetu. Mhe. Spika, nalo hili ni lazima sasa tujipange vizuri kabisa, tuache mzaha ili twende kuwaelimisha wananchi wetu na utaratibu wa kuleta hivi vitu vifike na kwa wakati.

Mhe. Spika, leo serikali ndio inayoagiza matrekta lakini hayakidhi haja. Mhe. Spika, sasa wakati wa ulimaji wa kunde umefika lakini wananchi hawajui walimie nini kwa sababu matrekta hakuna tunaambiwa ndio kwanza yako karakana yanafanyiwa *service,* karakana hawajatiliwa fedha ya kufanyiwa *service*. Mhe. Spika, kweli tutaweza kuinua kilimo katika hali kama hii.

Maana yake nikisema hiyo fedha yenyewe gharama yake sio kubwa, labda kuchukulia hii *maximum* ya hapa na pale kama shilingi milioni 8 tuseme labda ndio *service* kubwa, basi mpaka leo yako pale na yatakaa pale pale kipindi kinaondoka hiki cha kulima kunde. Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo yanakifanya sasa hivi kilimo chetu kirudi nyuma kabisa.

Mhe. Spika, nisifu tu kuhusu suala la uvuvi niseme *Alhamdulillah* idara hii inafanya kazi vizuri sana na imekusanya vizuri sana. Lakini si vibaya kusema idara hii Mhe. Spika, ikafanywa wizara kwa sababu ina malengo mazuri na makusanyo yake mazuri, ukiangalia hili eneo lote Unguja na Pemba Idara ya Uvuvi imeenea. Sasa nawapongeza wahusika kutokana na udhibiti wao mzuri na wametumia fedha za wafadhili vizuri sana lazima sifa yake ipewe. Si vibaya Mhe. Spika, nikakusifu wewe kutokana na utaratibu mzuri wa kuendesha vikao kwa vizuri, unapanga wajumbe wako kwenda kwa mpango kwenye safari japo mimi hujanichagua. Lakini ni lazima umsifu mtu kutokana na utendaji wake wa kazi, hiyo ndio hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nakuja katika kero la wafanyabiashara ambalo limekuwa kubwa na kila siku tunaambiwa inaundwa kamati. Mhe. Spika, Mhe. Rais Ali Hassan Mwinyi alitangaza “Zanzibar njema atakae aje” lakini dhana hiyo imepotea sasa hivi haipo kwa sababu biashara yetu haipo. Mhe. Spika, biashara hivi sasa iko Bara, tunaambiwa kuna *minimum* na kuna *maximum*, sasa mimi nashangaa kwa Bara *minimum* na kwa Unguja *maximum,* lakini hiyo *minimum* utakuta wenzetu wanaitumia vizuri sisi tunawekewa vile vile jina la *maximum*. Mhe. Spika, hiki kitu mimi kinanishangaza, ukitoa gari hapa ukipeleka Bara unalipa tena. Kero hili ni la kila siku, tunatangaza uchumi umepanda wafanyabiashara watukimbie uchumi huo utapanda vipi.

Wafanyabiashara hawapo leo Unguja lakini nenda mtaa wa Congo Dar es Salaam utakuta katika duka moja wanaingia watu 10 mpaka 20, leo wetu wako pale wanang'ong'wa na nzi hakuna biashara. Hili tukitaka tusitake lazima tuliseme linaumiza ndani ya roho kwa sababu ni njia za kuangushwa uchumi Zanzibar. Mhe. Spika, hili ni lazima tulikubali na kila siku linakuwa kero hilo hilo tu halipati jibu. Wafanyabiashara wanaumia wanatukimbia tukubali, kila siku wananung'unika. Wakipeleka basi kule, hii kwa kwetu tunaambiwa ndio kiwango kimoja ni shilingi milioni 2 kwa kuwa hili linafanya kazi, likenda kule unaambiwa ongeza tofauti yake shilingi laki tisa. Mhe. Spika, tunakwenda wapi?

Mhe. Spika, uchumi wetu utapanda kweli hali kama hii, tunakuja kutoa ripoti tunasema uchumi umepanda, lakini tutazame uchumi huo umepanda kwa njia nyengine. Mhe. Spika, hili suala tungeomba serikali iliangalie upya, yako mambo tuna uwezo sisi wenyewe tukaamua.

Mhe. Spika, kwa mfano juzi mimi nilimsikia Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi hapa alisema neno la mafuta, waliamua bila ya woga kwa nini sisi tushindwe kuamua suala hili tukasema sasa kiwango ni hiki. Kwa nini tushindwe? Ni kujiamini.

Mhe. Spika, mimi nasema Mwenyezi Mungu asinijaalie kunipa cheo nikawa Mshauri wa Rais, kila siku ningekuwa sitoki kwa Mhe. Rais na ninamwambia moja, mbili, tatu. Kwa sababu tunayaona yale mambo ambayo yanatuathiri, woga wetu ndio unaotufanya tuwe masikini. Hili lazima tuliseme.

Mhe. Spika, naomba hili suala tulishughulikie si kitu cha mchezo kwa sababu kuna biashara kwa upande wa maji ya uhai yatazameni yanavyoingia hapa. Mhe. Spika, hapa kwetu tuna maji yako ya *drop* lakini hayaendi kule Bara sasa hii biashara itakwendaje. Ikiamuliwa kwenda kule sasa watahodhi wao kila kitu. Watawachukua wao sawa sawa na *Zantel*, mmeipigia debe hapa nyinyi wakati sisi tuko nje leo *Zantel* iko wapi, Makao Makuu yako Dar es Salaam na ilikuwa yetu wenyewe ilikuwepo hapa.

Sasa hatupati pato kwa sababu Makao Makuu yako kule. Mhe. Spika, ni lazima viongozi tujikaze kuwatetea wananchi wetu, pengine tutawakamua wananchi wetu maziwa yenyewe hawana. Tutawakamua damu sawa sawa na ng'ombe, maana ng'ombe ukimkamua sana mwisho wa habari utamkamua damu. Tutatoa kodi nyingi humu za kuwabana wananchi wetu mwisho tutawaumiza.

Mhe. Spika, kuna miradi mingi sana tukisema serikali hebu sasa tuamue hapa tuchimbe gesi asilia tufanye mafuta yetu na mambo mengine, *wallahi* hatufi masikini sisi hapa hata siku moja na kila siku bajeti itapita vizuri labda

itatolewa kasoro ndogo ndogo tu. Mhe. Spika, hayo ni mambo ambayo nakuomba kupitia kwa Mhe. Waziri hebu tukae tuweze kulisaidia hili suala kwa nguvu zetu zote, biashara ya Zanzibar sasa inapotea.

Mhe. Spika, wenzangu leo walizungumzia masuala ya halmashauri. Mhe. Spika, halmashauri hivi sasa zinafanya kazi sawa sawa na serikali kuu, zinatusaidia katika shehia zetu kwa kujenga mambo yaliyokuwa muhimu sana. Halmashauri zinatengeneza *dispensary*, zinasaidia maji safi, zinasaidia masuala mengine madogo madogo ya jamii lakini utakuta mapato mengine wananyang'anywa na *ZRB* hawayapati hayo.

Sasa tunategemea halmashauri ifanye kazi gani. Hebu tuwapeni fursa. Hii miradi midogo midogo ya *ZRB* waondoke hapa watiwe wale. Leo utakuta eneo linauzwa halmashauri haipati asilimia 10 yake sijui kwa sababu gani, inaruka inakwenda kwengine. Lakini kama halmashauri ingepewa asilimia ile basi mimi naamini serikali kuu isingekuwa na kazi. Mhe. Spika, tunafika pahala tunadharau mambo mengi sana, tumewanyang'anya, leseni za utalii zote.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri alione hili kuwa halmashauri inamsaidia yeye katika utendaji kuinua serikali na kusaidia yale masuala mengine. Kwa sababu serikali si lazima mambo mengine itie mkono wao, hizi halmashauri zina uwezo na zimefanya kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, jengine ni suala la utalii. Serikali imeamuru vizuri tu kuleta suala hili lakini kuna tetesi wengine wanasema kuwa wanalipa huko huku inakuja hesabu ya watu. Mhe. Spika, tutajuaje hili suala mimi naona tunapotoshwa na idadi haziwi vizuri, makusanyo yetu japo tunasema kuwa asilimia kubwa ni nzuri wakati asilimia ile ukiitazama kama tungekuwa na uwezo wale wangelipa hapa basi ingekuwa nzuri zaidi.

Mhe. Spika, utalii tumesema ni moja katika pato kubwa la serikali na ndilo tumelitilia nguvu hivi sasa. Lakini wananchi wale waliokuwa karibu na utalii bado asilimia ya manufaiko ya pale yangali madogo sana. Ukifanya sensa ya wale wafanyakazi waliokuwa *zone* ya kile kijiji chenyewe kwa sababu serikali ilikwenda ikawashauri wananchi na wakakubali kwa manufaa ya kuona wao watatajirika katika zile shughuli ambazo zinazofanywa pale kwenye hoteli. Lakini kinyume chake wamekuwa wao wanadhalilishwa na ule utalii.

Mhe. Spika, tunajipanga vipi hapo. Kama tunajipanga katika ukusanyaji wa mapato basi tujipange jinsi na wale wananchi wetu kwa kuweza kunufaika na ule utalii wenyewe uliokuwepo pale katika shehia yao. Lakini kinyume chake hawanufaiki wananufaika watu wa Tanzania Bara sio wao, ni asilimia ndogo wanayofaidika wao. Mhe. Spika, sasa sisi tunakaa tunajiuliza jamani hii faida

ya nani na wakati serikali tayari imeshatangaza. Isitoshe Mhe. Spika, kuna hoteli moja Blue Bay Mhe. Ali Abdalla Ali alisema sasa tuna uwezo kuwa ma-*PO* sisi wenyewe lakini inanishangaza sana mpaka leo katika hoteli hiyo sioni Wakenya wameshaichukua nafasi yetu.

Sasa ukifuatilia utakatazwa huko juu. Mhe. Spika, mimi nasema siogopi huko hapa ndio pa kusema. Mhe. Spika, yuko mzee pale mhusika ambaye tayari ana uzoefu lakini anawekwa kando tu. Kwenye kikao cha ma-*PO* akiitwa Mkuu wa Mkoa anapelekwa yule mzee, nimeuliza nimeambiwa kazi yake ni Afisa wa Usalama. Mhe. Spika, kwa kweli hili suala linaniuma sana hatutaki nafasi zetu. Ndio maana waheshimiwa wengine wamesema kuwa sisi tunaambiwa tuzae kwa mpango wenzetu wanakuja kuchukua nafasi zetu ndio hiyo sasa hatari yake.

Mhe. Spika, au utaambiwa mtu msimamizi wa *dishwasher* anatoka nje, kwani sisi hatujui kukosha masufuria mpaka kwa usimamizi. Mhe. Spika, haya ni matatizo zile post ambazo zinawajibika wenyewe Wazanzibari tuweze kusimamia basi tunashindwa kupewa. Sasa Mhe. Spika, tunasema kuwa utalii Zanzibar ndio kitega uchumi cha serikali lakini sasa hivi hatari yake ni hiyo.

Halafu Mhe. Spika, ukiangalia kuna masuala mengine katika hizi post za ajira kama sasa hivi kuna wakati ambao tayari ajira. Lakini hebu tufanye uchunguzi sasa hivi inafanywa huko ya hizi ajira ambazo zinazofanyika. Kama nilivyosema asilimia ya wale ndugu zetu wa mitaa ile ukenda pale utaambiwa wako kumi tu. Kwa nini tusifanye mikakati ya kutosha ili wale wananchi wetu wakaweza kunufaika.
Mhe. Spika, kwa kumalizia suala la misitu kule kwetu Kiwengwa kuna msitu wa hifadhi kwa kweli sasa hivi humu tunamofanya katika *zone* za utalii na ningesema kuwa tuweke heshima ili msitu ule wa kitaifa uheshimiwe. Kwa sababu sasa hivi watu wanakata msitu ovyo tu bila ya kuangalia nini hasara zake.

Mhe. Spika, nalo hili tulione kuwa misitu sasa hivi imo katika ongezeko la kutafuta pato la serikali kuu lakini utakuta watu sasa hawaoni hiyo faida yake wanakata kiholela misitu na tumesema sasa hivi kuwa kilimo tutakipa nguvu, tutapeleka mijiti ambayo inahusika kule kwenda kupanda mingine lakini utakuta bado utaratibu ambao watu kuufahamu zaidi kama huu msitu huwa ni mali yetu na unaweza ukatupa faida aidha wale *NGO's* za pale au kikundi chochote kitakachopewa dhamana na serikali inaweza kupata pato na wewe kupata ajira, lakini bado wananchi wetu hili suala hawajauona umuhimu wake. Kwa sababu wanasema kuwa ni eneo ambalo tayari liko wazi na sisi tunakubalika basi nyinyi kaeni. Lakini eneo ambalo lina msitu na umekubalika umeingia basi tusiweze kukata.

Mhe. Spika, ningeomba hilo nalo tulione kuwa wananchi wathamini msitu na hizi mbegu tulizosema kilimo cha iliki ambayo sasa hivi imepotea, mivanila sasa hivi ipo sehemu chache tu. Sasa nalo hili tulitilie nguvu kupeleka miti. Mhe. Spika, utakuta wananchi wengi wanataka sasa hivi kulima vanila, iliki, tangawizi, kungumanga, pilipilimanga, hivyo ndio vilimo ambavyo sasa hivi kama vitalu vyetu viko tayari ambavyo vimeshaotesha vitu hivyo kwa kuwafikisha wananchi haraka sana kwa sababu ni moja katika zao ambalo linaloleta tija katika serikali yetu. Ni vitu ambavyo tuna uwezo wa kusafirisha nje na kuweza kupata faida kubwa sana.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nakushukuru kuwa hujanambia nimalize nizungumzie ukurasa wa 16 mwenendo mzuri wa hali ya biashara umejitokeza pia kwa upande wa biashara Tanzania Bara usafirishaji. Mhe. Spika, hapa mimi kidogo naomba Mhe. Waziri akija anisaidie.

Mhe. Spika, tunapopeleka sisi biashara hizi nyengine ndogo ndogo kule Dar es Salaam bado lingali tatizo tunalipa kwa mfano kupeleka friji, TV na vitu vyenginevyo. Sasa imekuwa kule kwa wenzetu tukipeleka vyetu sisi imekuwa biashara imepungua chini. Lakini ukichukua kule halafu mimi kitu ambacho kinazidi kunishangaza, ukichukua kule vitu kuleta Zanzibar bado unabakia ulipe bandarini kule halafu isitoshe ukija huku kwetu unakuwa hulipi.

Mhe. Spika, ukinunua mipira ya maji ukifika pale bandarini unatakiwa ulipe sasa mimi nikajiuliza. Lakini ukiingia hapa nchi yenye huruma naambiwa nisilipe ni kitu ambacho kinanishangaza. Halafu Mhe. Spika, kwa nini na sisi biashara zetu hapa kuna mambo mengi kwa mfano kule wenzetu shokishoki hawana lakini hazifanyiwi kasi kupelekwa kule, madoriani hawana hayapelekwi kule, hebu tuangalie kuna nini?

Mhe. Spika, la mwisho la kusikitisha maji ya *drop* mimi Dar es Salaam miaka yote nakwenda sijayaona, naona mimi hapa *Zanzibar Kool*, wenzetu Uhai, Dasani yapo hapa. Mhe. Spika, siku moja Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikwenda mikoani huko alikuta maji ya Kenya katika hoteli akasema kuanzia leo yasiuzwe pale kwa sababu anataka biashara yetu iuzike ndio mantiki yake.

Lakini sisi maji yetu hayavuki tunaambiwa yametiwa sumu ya uaghai ya kuambiwa yana chumvi ndio maana hayaendi kule, lakini nikinywa yao naona machungu. Sasa mimi nikawa najiuliza hapa yale yenye chumvi na haya machungu tofauti zake ziko vipi. Mhe. Spika, namwomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwa kina maana sina haja ya kupita buti leo, isipokuwa nataka nimpongeze tu.

Lakini suala hili Mhe. Waziri na mimi ninamwamini kwamba atalifuatilia kwa kina, kwa sababu ya yeye ni Mzanzibari na anataka kuwaokowa Wazanzibari. Kwa hivyo, hata na magazeti yetu ya Zanzibar hayapo kule, lakini magazeti yote yanayotoka kule hapa yapo. Hivi sisi hatujui biashara na wala hatuna uwezo wa kupeleka bidhaa zetu kule, ninadhani tunao uwezo.

Kwa sababu kuna muda fulani tuliwahi kupeleka maziwa sisi, lakini yalifanyiwa mambo mpaka leo maziwa hatujapeleka tena kule. Vile vile sigara tulikuwa tukipeleka, yaani unapewa sehemu ndogo ya kuuzia sigara kweli utapata pato, kwa kweli hakuna kabisa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Lakini ajue kwamba kwenye pongezi hizo na kasoro lazima zitakuwemo. Kwa mfano, sawa na mtu kuvaa *tie* akasahau kuvaa buti.

Vile vile wanashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kitope pamoja na mimi mwenyewe binafsi kwamba tunaiunga mkono bajeti hii ya serikali kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Ahsante sana.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kwa kutoa shukurani kwa kunipatia nafasi hii na mimi nizungumzie kidogo kuhusu Bajeti ya Serikali.

Pili ingawa hili limeshazungumzwa sana, lakini kwa sababu ya kipekee naomba nitoe pole pamoja na majonzi ya dhati kwa wenzetu waliotutoka Mhe. Daud Hassan Daud pamoja na Mhe. Soud Yussuf Mgeni, hasa kwa sababu Mhe. Soud Yussuf Mgeni alikuwa ni msaidizi wangu mkuu, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, Amin.

Tatu nimpongeze Mhe. Asha Mohd' Hilal kwa kujiunga na sisi kwenye Baraza letu namtakia kila la kheri *(Makofi)*.

Mhe. Spika, jengine naomba nichukue nafasi hii maalum kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwamba nimpe nafasi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa ungangari wake bora ajiunge na kambi yetu *(Kicheko/Makofi)*.

Sasa nizungumzie kuhusu Bajeti ya Serikali. Kwa kweli bajeti hii ina uzuri mmoja na uzuri wake ni kwamba alisema kwenye bajeti hii zaidi ya asilimia 50 imewekwa kwa masuala ya maendeleo. Hii ni bajeti nzuri hata ukilinganisha na Bara haijawahi kutokea na hapa napenda nimpongeze Mhe. Waziri.

Lakini wasi wasi wangu kwamba hayo maendeleo ni kweli tuliyoyaweka tutayapata na tuta-*inject funds* hizo kwenye *development*. Kama tutapata *funds* hizo na tuka-*inject* katika *development* ambayo ni zaidi ya asilimia 50 kwa hivyo, inastahiki pongezi.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka kuzungumza ambalo Mhe. Waziri katika kitabu chake kwenye ukurasa wa 7 na 8 kuhusiana na mtikisiko wa uchumi. Ninadhani bajeti nzuri inayozungumzia mtikisiko wa uchumi ingelisema hasa hasara ambayo Serikali ya Zanzibar imepata kutokana na mtikisiko huu pamoja na kutuonesha sisi Wazanzibari ile *Rescue Plan*.

Mpango gani ambao serikali ilikuwa inao au imeuandaa, ili mtikisiko huo uweze kupungua. Lakini bajeti hii imekwenda tu *just passing* na wala haikutuelezea hasa, nafikiri hii ni kasoro. Kasoro hii naomba irekebishwe kwa sababu tukijua hasara ambayo tumeipata kutokana na mtikisiko huu na *plan* zetu za ku-*rescue* tatizo hili.

Ninadhani hapo sote Wazanzibari tungekuwa kidete au tungeweza kujifunga mkaja kama wanavyosema wenzetu, ili suala hili la mtikisiko wa uchumi tukaweza kulishughulikia ipasavyo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 44 na 45 Mhe. Waziri amezungumzia masuala mawili kuhusu suala la utalii na karafuu. Kwa upande wa utalii utashuka kwa asilimia 10 na hii ndio *projection* ya wizara au serikali kwa watalii.

Ninafikiri hii haitoshi na bajeti hapa itakuwa na matatizo kwa sababu hajasema. Kwa mfano, angelisema Mhe. Waziri kwamba watalii walioingia mwaka 2008 walikuwa 100,000 na watalii hawa waliingiza shilingi bilioni 2. Lakini kutokana na mtikisiko huu watalii safari hii tunakisia wataingia 80,000 na kutokana na kushukuka kwa asilimia 10 zile bilioni 2, sasa tutapata angalau bilioni 1 na nukta kadhaa.

Kwa hivyo, *at least* tukajua ni kiasi gani ambacho tutakosa kutokana na kupungua kwa watalii. Hali hiyo ingelisaidia sana katika kujua hasa bajeti yetu iko namna gani na kitu gani ambacho kimeanguka au kimetuangusha na tufanye nini, ili tuweze kuinyanyua bajeti yetu kwa njia nyengine.

Mhe. Spika, kuhusu suala la karafuu na vile vile kama utalii. Kwa sababu alisema kwamba bei ya zao la karafuu itashuka, lakini hakutuelezea mwaka jana ilikuwa kiasi gani na mwaka huu inatarajiwa kuwa kiasi gani, ingawa amesema itashuka kwa kiasi gani.

Lakini ninadhani bei hii ya karafuu napenda nisikubaliane na Mhe. Waziri, na hapa kwa sababu bado hatujawa *serious* katika kutafuta Soko la Karafuu pamoja na kuhamasisha watu wetu.

Ndio maana Mhe. Spika, katika kitabu cha pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa 2009/2010 kwenye ukurasa wa 21 na 86 tutaona kwamba Mradi wa Kuimarisha Mikarafuu ni shilingi milioni 60. Sasa mimi nasema ikiwa serikali inasema zao la karafuu ndio zao kubwa na wanaweka shilingi milioni 60, kwa ajili ya kuimarisha zao hili kwa kweli hawako *serious*.

Kutokana na hali hii siku zote zao hili litakuwa liko nyuma, wachumaji wa karafuu watakuwa nyuma na wala hawatoridhika kabisa kwa bei ambazo zinatolewa. Kwa sababu hakuna *seriousness* ya kutafuta Soko la Karafuu na wala kuwahamasisha wachumaji wa karafuu katika kuzalisha karafuu nyingi zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mara nyingi Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji utasikia amesafiri, sijui kwa ajili ya kutafuta soko la nini. Naomba kutoa mfano kama tutaufuata basi nina amini karafuu tunaweza tukapata bei kubwa sana na hali hii inaweza kusaidia katika kuongeza bajeti yetu.

Kwa mfano, Uganda wao walikuwa na tatizo la soko la kahawa, sasa walichofanya waliamua tu serikali wakasema kwamba hoteli zote kila chumba iwekwe nusu kilo au kilo moja ya kahawa. Sasa anapokwenda mtalii na hata Mganda akenda kulala mle, anachukua kahawa ile kama. ni *souvenir*, lakini kimantiki ni kwamba kilo moja ile ya kahawa tayari ameshailipia kwenye malipo yake ya hoteli. Kwa hivyo, kama tayari ameshailipia, basi serikali inakwenda hoteli na kusema kwamba tulikupa idadi fulani ya kahawa na tunahitaji utupe fedha zetu. Sasa kutokana na utaratibu kama huo inakuwa soko halina tabu tena kwa bei nzuri.

Kwa mfano, hapa nimefanya hesabu tunazo karibu hoteli 300, sasa wale watalii pamoja na watu wengine wanaokwenda hoteli kupata huduma mbali mbali. Vile vile mtu yeyote akiamua siku moja kwenda na familia yake Kiwengwa na kukaa kwa muda wa siku mbili, basi atakapoondoka anaondoka na kilo moja au nusu kilo ya kama tutakuwa na *policy* hiyo.

Kwa hiyo, nusu kilo ya karafuu anachukua kama ni *souvenir*. Lakini tuwe tayari tumeshasema kwamba mwenye hoteli nusu kilo ya karafuu ile aongeze shilingi 10,000/- na mtu haioni. Isipokuwa inaingia mle na ikesha kuingia basi tunakwenda hoteli na kuwaambia watupe fedha zetu idadi ya kilo ambazo tulimpa kwa kipindi fulani.

Kutokana na hali hiyo, tunaweza kuuza hapa karibu tani 5,000/- kwenye hoteli na wala mtu hajui na bila ya kusema chochote na bei itakuwa ni kubwa. Kwa sababu ukimwambia kwa mfano, nusu kilo ya karafuu ni shilingi 10,000/- aongeze kwenye kodi ya chumba hakuna mtu atakayepiga kelele. Kwa hivyo, hiyo ni njia moja ya kupata mapato.

Mhe. Spika, naiomba serikali ikaifikiria kwa makini, ili karafuu zetu ziwe na soko, pili hawa watu angalau wanapokuja akipewa *souvenir* karafuu na kudhani anachukua bure, kumbe si bure na itaenea ulimwengu mzima. Kwa kweli ukienda Zanzibar unapata *cloves* bure kwenye mahoteli, kumbe sisi tunafanya biashara.

Ninadhani tuwe wabunifu kama hivyo tena nafikiri hiyo itakuwa ni biashara nzuri sana, tutauza karafuu zetu kwa bei nzuri pamoja na kuwasaidia wakulima wetu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la uvuvi. Nasikitika kwamba humu halikuzungumzwa hasa, yaani limepitishwa tu na wala sioni kama lilipewa kipaumbele na tukasema kwamba wavuvi wetu tutawasaidia namna gani, wanaweza kuingiza kiasi gani na fedha hizo zinaweza kuisaidia bajeti ya kwa kiasi gani.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Spika, kwamba bajeti hii haikubuni vianzio ambavyo tunaweza kupata fedha, kwa ajili ya kuisaidia serikali pamoja na wananchi wetu kwa jumla.

Katika kitabu hiki Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 51 unasema kwamba mapato ya ndani anakusudia kukusanya kiasi ya shilingi 159,697 milioni kutokana na vianzio vyake ambazo kati ya hizo shilingi 148,932 milioni zinatokana na kodi na shilingi 10,765 milioni zinatokana na vianzio visivyo vya kodi. Vianzio vya kodi hapa imetolewa *ZRB* ambayo ni shilingi 85,773 milioni na *TRA* shilingi 63,159 milioni na vyengine havikutajwa.

Mhe. Spika, hapa kuna makosa matatu muhimu na bajeti hii sioni kama imetilimia kutokana na kasoro hizi zilizopo hapa. Mhe. Spika, kwa mfano sisi tunao uwanja wa ndege, huu siku hizi tunamshukuru Mwenyezi Mungu umekuwa ni mkubwa ndege nyingi zinakuja, eneo au sehemu ya uwanja wa ndege ni miongoni mwa vyanzo vya mapato.

Ndege zinazokuja zinatoa mapato ya namna nne au tano. Kwa mfano, kwanza tujue ni ndege ngapi, pili kuna *Landing Fees*, tatu kuna *Parking Fees*, *Handling Fees*, kuna suala la *Refueling* katika uwanja pale, zote hizi ni kodi ambazo ni

kubwa sana, tukiacha *Airport Tax*. Kwa hivyo, nilifikiria kwamba bajeti hii ingelisema kwa mwaka huu tunatarajia zitatua ndege 70 kwa mfano kubwa, ndege 300 ndogo ndogo hizi *Landing Fees* tutapata dola laki 2, *Parking Fees* tutapata dola hizi na kiasi fulani.

Sasa mchanganuo huu ndio ungelituwezesha kujua kwamba je, sekta hii eneo hili tunapata kiasi gani na tufanye nini, ili kuboresha na kupata *funds* zaidi kutokana na huduma hizi, lakini haikusema. Kwa maana hiyo, hapa bajeti ina kasoro, kwa sababu haikuwa wazi na wala hatujui kwenye eneo hili tutapata kiasi gani.

Mhe. Spika, vile vile Bandarini kama ilivyo kwenye uwanja wa ndege na bandari nayo ni muhimu miongoni mwa vyanzo vya mapato, lakini hatukuambiwa. Kwa hivyo, hatujui bandari yetu meli ngapi zinakuja au zilikuja mwaka uliopita na tunatarajia meli ngapi zitakuja, tunatarajia tani ngapi zitateremshwa pamoja na makontena mangapi yatateremshwa na hayo yataingiza dola kiasi gani.

Bandarini pia kuna *fees* nyingi. Kwa mfano, kuna *Port Fees*, *Handling Fees*, *In anchorage*, *Out anchorage*, *Long side anchorage*, vile vile kuna masuala ya meli zinapofika nje anaagizwa *pilot* kwa malipo. Kwa kweli hizi Wizara ya Fedha hamkutueleza au tuseme Zanzibar hakuna meli hata moja inayokuja na kwa nini mkawa kimya hivi katika vyanzo vya mapato.

Kwa sababu bajeti inatakiwa haya yote yaonekane, lakini Mhe. Spika yote haya hayapo, yaani hayakuzungumzwa na yako kimya kabisa kama Zanzibar ndio kwanza tunaanza hatuna uwanja ndege au hatuna bandari ama huduma hizi hatutoi, kitu ambacho si kweli.

Mhe. Spika, ninafikiri kwamba bajeti kuwa nzuri lazima mambo haya yawepo, vyenginevyo tutajiuliza kwa nini hamtwambii kuna matatizo gani hapa, kwa nini mkatuficha na wala haiwezekani. Kwa maana hiyo, lazima tuambiwe na yaonekane, ili tuweze kushauri baadhi ya mambo ama kuongezwa au kupunguzwa.

Kwa mfano, kama tungelijua kwamba *out anchorage* ya meli inayozidi tani 70 ni dola 3,000 basi tunaweza kusema, ili kuongeza fedha sasa ni dola 4,000, lakini hatujui. Tuseme *Handling Fees* ya ndege kubwa 767 kama ni dola 2,000 sasa iwe 2,500 ndio tutapata fedha. Lakini kila kitu kimebanwa na Wizara ya Fedha kwa Katibu Mkuu pamoja na Waziri basi, kwa hivyo hatuwezi kwenda isipokuwa lazima mtwambie na sisi kwa ajili ya kuwapa ushauri na wala msifanye mambo peke yenu *(Makofi)*.

Sasa mkituambia hivyo, ndio tutaweza kushauri pamoja na njia mbali mbali na kusema vianzio hivi viongezwe au vipunguzwe kwa kiasi fulani, hapo ndipo itakapokuwa bajeti nzuri ambayo ni ya watu.

Mhe. Spika, mafuta pia ni kianzio chengine nacho ni kimya hakuna taarifa yoyote hukusu *Depot* zile na wala zinatozwa kodi kiasi gani, meli zile zinalipa kiasi gani pamoja na ushuru wa aina gani na hiki ni kianzio kikubwa, kwa nini hatuambiwi.

Ninachosema ni kwamba bajeti hii ina kasoro kwa sababu vianzio vya mapato vyote havina *data*, yaani *statistics* za kujua kwamba tuongeze au tupunguze na vianzio vya mapato ikiwa havina data. Kwa hivyo, sisi unatufanya tuwe bubu na hatuwezi kupendekeza wala kushauri kwamba kianzio hiki kiongezwe ua kupunguzwe. Mhe. Spika, ninadhani uzuri wa bajeti tungeliainisha vianzio vya mapato katika maeneo haya kwa mfano, bajeti yetu ingelikuwa ni nzuri na tungeliweza sisi Wawakilishi wako kushauri kianzio hiki kiongezwe au kipunguzwe.

Kwa mfano, tunaweza kusema Mhe. Spika, kwamba *Handling Fees* za ndege ndogo ndogo za *Zanair* pengine dola 500 ni kubwa, tufanye dola 400 na tukifanya hivi tutanufaika sisi wasafiri tunaokwenda Dar-es-Salaam, Unguja, Pemba na sehemu nyengine na hayo ndiyo mambo ya bajeti yanayotakiwa, lakini yote yako kimya. Kwa hivyo, hii ndio kasoro ambayo napenda Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anielezee tutafanya nini.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu Serikali ya Mungano wa Tanzania dhidi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli ni bahati mbaya na maelezo haya Mhe. Spika, mara nyingi tunayasema, lakini bado serikali haijasikia na haya ndiyo yanayaowaua au kuwaumiza Wazanzibari.

Kwa mfano, kuna suala la *Co-operate Tax*. Nafahamu kwamba kuna yale mashirika ya Muungano ambayo yana sehemu zake hapa Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu wa sheria fedha zile za *co-operate tax* yale mashirika yaliopo hapa zinatakiwa zilipwe hapa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hilo halifanyiki.

Kwa kweli hiki ni kianzio kikubwa cha fedha kwa nini tunawaachia na zile tumekubaliana kwamba hizo zilipwe Zanzibar. Lakini zote wanasema wanalipa makao makuu ambapo ni kinyume na utaratibu. Sasa kama unakwenda kinyume na utaratibu tuliokubaliana na bado serikali inakaa kimya, ina maana inawakaribisha hawa makusudi wafanye wanavyotaka.

Kwa hivyo, suala moja la kupata fedha zaidi kwa serikali ni kuhusu *co-operate tax*, ambalo bado mashirika ya muungano yanazichukua fedha hizi na kuzipeleka Makao Makuu ya Mashirika yalioko Bara.

Suala la pili kuhusu mambo ya uhamiaji, *Tanzania Civil Aviation, Tanzania Communication Regulator Authority* yote hayo.

Jambo jengine ambalo Serikali ya Muungano imeua kwa makusudi mapato ya Serikali ya Zanzibar ni mengi. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alielezea kuhusu sigireti. Kwa kweli sigireti za Raha na za Kuchuja Mhe. Spika, kama uliwahi kwenda Mwanza sigireti zile zilikuwa zikitakiwa kama ni bidhaa zenye thamani sana na siku ile ile wafanyabiashara wanarudi.

Lakini wenzetu walipoona kwamba sisi tunafaidika, basi sigireti zile zikatozwa ushuru mkubwa, yaani hata yule mfanyabiashara anapofika kule anapolinganisha bei anayouzia na kununulia haiwezekani, hatima yake kiwanda kimekufa, ndio lengo lao na wao wanafurahi.

Mhe. Spika, Kampuni ya *ZANTEL* ilikuwepo hapa na hizi *vouchers* za simu tunazonunua za shilingi 5,000/- 10,000/- zile zinakuja *in bulk* na halafu kila boski linatozwa *fee* ya dola 10. Sasa wenzetu hawa ambao hawana imani na Zanzibar inatozwa hapa dola 10, lakini boski ile inapofika Dar-es-Salaam kwa sababu kampuni imeshakwenda kule wanatozwa tena dola 10 tena na kufanya jumla ya dola 20.

Kwa hivyo, *ZANTEL* wakasema kwa nini tufanye hivyo, wakati tunapopeleka yale maboski tunatozwa zile dola 10 na baadaye tunaposafirisha kutoka Dar-es-Salaam kwenda Zanzibar hatutozwi. Sasa ni mfanyabiashara gani ambaye atakuwa hana akili ya kutozwa kodi ya aina moja kwa sehemu, yaani Zanzibar na Tanzania Bara. Ndio maana wafanyabiashara wote hivi sasa wanakwenda Bara.

Kutokana na hali hiyo, ushuru wote unalipwa kule na hapa tunabakia hatuna kitu. Sasa huu ndio urafiki pamoja na udugu wa aina gani, serikali imefanya nini kama haya, imeua viwanda vyetu na leo hatuna kiwanda hata kimoja. Kwa mfano, hayo maji aliyozungumza Mhe. Mjumbe, huthubutu kwenda na *Drop of Zanzibar* Dar-es-Salaam ushuru utakaoambiwa utafikiri ni maji ya Zamzam. Kwa hali kama hiyo, hatuwezi kufika hapala kwa sababu wenzetu hawana huruma na wanatumiza kwa makusudi *(Makofi)*.

Sasa serikali kama hatujakaa na kuyaamua haya kidhati kabisa na badala yake kila siku kuyaweka kwenye Orodha ya Kero za Muungano, tunapokwenda kule tunazungumza siku mbili na baadaye tunakaa miezi mitatu. Kwa kweli

tutaendelea kupata matatizo Wazanzibari wataendelea kuumia na wao wataendelea kunufaika.

Mhe. Spika, huu si Muungano wa dhati kwa pande hizi mbili, lazima kuwe na mazungumzo ya mambo kama haya. Kwa sababu nchi kama hii ni lazima tuwe na vyanzo vya mapato, lakini vyanzo vyote vimekamatwa na wala hatutofika na nchi yetu itakufa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hayo ni mambo ambayo wizara ingeliweza kutwambia inafanya nini na imepanga kufanya nini. *(Makofi).*

Mhe. Spika, suala la mwisho nizungumzie kuhusu uchumi pamoja na ongezeko la watu. Jambo hili nalo ni tatizo, lakini hapa naomba nitoe wasia kwa serikali tena kwa mfano hai kwa kisiwa kinachoitwa Fiji. Fiji kulikuwa na kiongozi akiitwa Rabeca yeye alikuwa na uchu wa madaraka, sasa aliona kwamba Fiji wale wazaliwa au wenyeji wanaomuunga mkono ni kidogo, basi aliona wachukue watu kutoka nchi za jirani.

Kwa bahati zao lao kubwa ni miwa, wale wanapokwenda kule wanapanda miwa pamoja na kupewa kila kitu mpaka vitambulisho vya Fiji kwamba wao ni Wafiji. *as a result* ya *inject* ya watu ambao sio Wafiji baada ya muda watu wale ndio walioshika serikali, ni wageni kutoka nje ndio walioshika serikali. Sasa mimi wasia wangu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuja kupinduliwa kwa mpango huu hao wanaoletwa tunawaachia bila ya kuwa- *control na passport* na mambo mengine, lazima visiwa viwe na *control* hebu tutizameni UK na Ireland, wewe nenda na uwe na *passport* ipigwe *visa* halafu usema unakwenda Ireland huwezi kwenda kuna utaratibu wake kwa sababu hawataki watu waende tu.

Mhe. Spika, sasa nasema ni lazima kwa sababu hapa ni visiwa tuwe na *control* ya watu hawa, tujue nani anaingia na nani anatoka, lakini tukiwacha holela tu tutafeli na mwisho hao ndio watakaokuwa mabwana zetu sisi tutakuwa wadogo, hayo yatakuja kutuumiza baadae, hivi sasa hatuyaoni au kama tunayaona tunayachezea, lakini yatakuja kutuumiza baadae.

Mhe. Spika, tuchukue mifano kwa Hong Kong, China na mwenginemo, lazima *control* ya watu katika visiwa ni muhimu sana, vyenginevyo sisi tutaathirika na watakaokuja kutuuliza ni wajukuu zetu kesho na keshokutwa. Hata katika suala la uchumi huwezi kupanga ikiwa hujui watu wako ni wangapi, kila siku watu wanaingia hawatoki, kama r*ed sea* hii ina- *inlet* tu yale maji yanaingia tu, lakini hayatoki sasa tusiwe kama red sea, haina *outlet* ya kutokea yakishaingia maji ndio basi. Sasa Mhe. Spika, tukifanya hivyo tunaweza kupata hasara na hatuwezi kupanga na upangaji wetu wote wa bajeti unaweza kufeli kwa njia hii.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa muda huu na namwomba Mhe. Waziri azingatie hayo kwa nia safi ili bajeti yetu iwe nzuri. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuweza angalau kuchangia, kwa hivyo Mwenyezi Mungu akubariki na akupe kila kheri na akuondoshee kila la shari.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kumshukuru Allah Subhana wataala kutujaalia jioni hii ya leo kuweza kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya fedha na uchumi, bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, lakini kabla ya kuanza kufanya kazi hiyo nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magomeni kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Magogoni kwa kumchagua Mhe. Asha Moh'd Hilal, kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni, nawapongeza sana. Lakini pili Mhe. Spika, nichukue nafasi hii vile vile kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuongoza vyema kwa utulivu na amani, lakini pia kwa kusimamia ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi hiki na sasa hivi serikali imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo na sote tunajivunia.

Mhe. Spika, pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wake kwa kutayarisha mipango mizuri iliyopangika, iliyokuwa na kasoro kidogo sio nyingi. Mipango ambayo kama itatekelezwa vizuri, basi visiwa vyetu hivi huenda vikabadilika na tumwombe Mwenyezi Mungu mipango hii iende kadri ya vile ilivyokuwa imepangwa.

Lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti Mhe. Haji Omar Kheir kwa hotuba yake nzuri na inakubaliana na yale yote aliyoyasema juu ya utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli za serikali na mambo mengine mengine ili tuone inakwenda vyema.

Mhe. Spika, tunapozungumzia suala la bajeti ya serikali tunazungumzia mambo makubwa matatu, kwanza tunazungumzia mapato ya serikali, lakini pia tunazungumzia matumizi ya serikali, lakini hatimae tunazungumzia juu ya mipango ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu.

Lakini haya mambo mawili ambayo tumeyazungumzia masuala ya matumizi pamoja na mipango ya maendeleo, hayawezi kufanikiwa au kutekelezeka kama serikali haikuweza kupata mapato ya kutosha, tutakapopata mapato ya kutosha

maana yake mipango yetu ya matumizi pamoja na mipango ya maendeleo tunaweza kutekeleza ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu ambazo Mhe. Waziri ametuletea katika hotuba yake makadirio ya mapato ya ndani kwa mwaka huu wa fedha ni 38.7% ya mapato yote ya serikali, ambapo ruzuku na mikopo inakadiriwa kuwa ni 48.3% na ile misaada ya kibajeti pamoja na hati fungate inakadiriwa kuwa ni 13% ya bajeti nzima. Kutokana na hesabu hizo ambazo Mhe. Waziri ametuwasilishia ni dhahiri kwamba mapato ya ndani katika bajeti yetu hii hayazidi 40%, kwa maana hiyo bajeti yetu ya mwaka huu zaidi ya 60% inategemea fedha kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, tukiangalia upande wa pili wa bajeti ya maendeleo matumizi ya kazi za maendeleo katika bajeti hii ni 58.1% ya bajeti nzima ya Serikali, kwa kweli ukiangalia ni kiwango kizuri, ni kiwango kikubwa na ambacho cha kupigiwa mfano kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Lakini katika fedha hizo za maendeleo 48.3% ni mchango wa wahisani na 6.9% ni mchango wa serikali, lakini ukiangalia fedha halisi za maendeleo ambazo ni bilioni 239.91 serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kutoa asilimia 17 na zilizobakia 83% ni fedha za wahisani.

Sasa katika hali kama hii na katika bajeti kama hii ni sura ambayo inatisha, wahisani watakapositisha tu fedha zao kwa ajili ya maendeleo na asilimia kubwa ambayo ipo, ni dhahiri kwamba katika kipindi hiki basi maendeleo ya wananchi wetu yatakuwa mashakani.

Lakini Mhe. Spika, tukija kwenye matumizi ya kawaida ambayo fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya kuendesha mawizara yetu ni 9.4% ya mapato ya serikali, fedha hizi ni muhimu sana na kwa sababu fedha hizi zinaiwezesha serikali kupitia mawizara kufanya shughuli zake mbali mbali, kuweza kusimamia na mipango yake mbali mbali, ukiangalia ni kiwango kidogo mno, lakini ndio hali halisi ya mapato yetu na uwezo wetu ni kiwango kidogo.

Mhe. Spika, kwa ujumla bajeti yetu ya mwaka huu pamoja na mipango mizuri ambayo nimeieleza ambayo Mhe. Waziri ametuwasilishia ni bajeti ambayo inategemea kwa asilimia kubwa sana wahisani, jambo hili linafaa kukaa na kulitafakari sana pamoja na kwamba hatuwezi kuliepuka kwa sababu ya hali halisi ilivyo, lakini utegemezi huu umekuwa mkubwa mno ambapo tunahitaji kukaa na kutafakari kuona namna gani tunaweza kupunguza hili pengo la utegemezi kwa sababu utegemezi huu umekuwa mkubwa mno.

Mhe. Spika, ndugu zetu wa Pemba mara nyingi wanasema kwamba mno yoyote ni mbaya, maana yake hata chai ile ikizidi sukari maana yake inakuwa mbaya na ikikosa sukari inakuwa si nzuri, lakini ikizidi inakuwa mbaya, hali kadhalika chumvi katika chakula ikiwa haimo inakuwa mbaya, lakini ikizidi inakuwa mbaya zaidi kwa hivyo mno yoyote ni mbaya. Sasa bajeti yetu imekuwa tegemezi mno kwa sababu bajeti inayotegemea wahisani wa nje kwa zaidi ya 60% ni tegemezi mno, tungetegemea kwamba tutegemee watu wa nje, lakini iwe kwa angalau 20% kwa yale mambo mengine mengine. Lakini tegemezi hii imekuwa mno.

Mhe. Spika, nadhani hii ni changamoto kwa wachumi wetu wa Zanzibar kwa sababu hatuwezi kuendelea na hali kama hii katika siku zijazo, hao wakubwa ambao tunawetegemea watusaidie na wao wenyewe wako katika hali mbaya wapo taaban, leo nchi kubwa kama Marekani inadaiwa matrillioni ya fedha na Wamarekani hao hao tunategemea watusaidie, sasa hali hii ni lazima tukae tuitafakati tujipange vizuri katika siku zijazo, lakini tutakuja kushindwa hata kutengeneza ile barabara moja.

Mhe. Spika, lakini nasema tujiulize hivi tutaendelea na hali kama hii hadi lini ndio tutakuwa tunakwenda hivi hivi tu hatuwezi tukakaa tukauma bongo letu, lakini pia Mhe. Spika, tujiulize tutaendelea kuzikodolea macho taasisi zetu hizi za ukusanyaji wa mapato *ZRB* na *TRA* wawakamue wananchi wetu halafu tufanye mipango ya matumizi, hivi tujiulize hakuna njia nyengine mbadala ya kutuondosha hapa tulipo na kwenda katika eneo jengine. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba majibu yapo kuondoka hapa tulipo kwenda katika eneo jengine majibu yapo, pamoja na kwamba sisi ni wanasiasa sio wachumi.

Mhe. Spika, majibu ya mambo haya ni mengi, lakini nitajaribu kuzungumza baadhi tu, kwanza serikali ihakikishe inasimamia ipasavyo suala zima la uwajibikaji kwa kila mtu katika sehemu yake ya kazi, tutakapohakikisha kwamba kila moja anafanya kazi na anawajibika katika sehemu ya kazi, basi itakuwa ni moja kati ya njia ya kutuondosha hapa tulipo kwenda katika sehemu nyengine hii ikizingatia kwamba wafanyakazi wafanye kazi kwa muda wao wa kazi kadiri ya sheria ilivyo sio kama ilivyo sasa hivi.

Mhe. Spika, lakini hata wale waliopangwa kukusanya mapato hayo tunayoyazungumza, basi wafanye hivyo kwa uadilifu mkubwa na waachane na tabia ya udokozi dokozi ule wa mali ya umma.

Jengine hata wale waliopangwa kutoa huduma kwa ajili ya wananchi kwa mfano madaktari, wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wao wawajibike ipasavyo katika maeneo yao lakini hata waalimu na wao wanahitaji kuwajibika katika maeneo yao ya kazi, wale watoaji wa haki Mahakimu, basi

wapunguze muda wa kusikiliza kesi kwa sababu wananchi wanatumia muda mrefu kwenda Mahakamani kwenda na kurudi na masuala yao yanakuwa bado hayajapatiwa ufumbuzi. Kama nilivyosema kwamba hayo ni baadhi ya maeneo tu ambayo kama serikali itasimamia ipasavyo, basi suala la utegemezi wa wahisani na kutegemea zaidi fedha za mapato kutoka nje basi yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, lakini jengine ni suala la kutumia rasilimali zetu, visiwa vyetu Mwenyezi Mungu ametujaalia vimezungurukwa na rasilimali nyingi, kisiwa chetu kimezunguukwa na bahari, ni eneo ambalo lina utajiri mkubwa na kama tutalitumia vizuri na kuitumia vyema bahari yetu, basi tunaweza kupata mapato mengi na Mwenyezi Mungu anafanya kila kitu kwa uwezo wake, sisi hatuna madini, hatuna dhahabu, hatuna almasi.

Lakini ametujaalia kutupa bahari ambayo ina rasilimali kubwa kupita kiasi hebu tujitizame au tujiangalie rasilimali hii ya bahari iliyotuzunguuka tunaitumia ipasavyo, ndani ya bahari yetu kuna samaki wa kutosha bahari ya chini na bahari ya juu, bahari kuu zote zina samaki wa kutosha tunazitumia ipasavyo.

Mhe. Spika, baharini tunaweza kuzalisha umeme wa kutosha tulipokwenda Dubai mwaka jana tulielezwa kwamba umeme wote unaotumika pale Dubai basi unatumia mawimbi ya bahari, umeme uliokuwa haukatiki ni wakawaida, lakini ukiangalia sisi tumezunguukwa na bahari umeme wetu tunautoa Tanzania Bara wakati mwengine unakatika, wakati mwengine mitihani mikubwa mikubwa na tunalipa fedha nyingi wakati tuna rasilimali ya kutosha juu ya bahari iliyotuzunguuka ambapo tungeweza kutumia mawimbi ya bahari yakatuzalishia umeme.

Mhe. Spika, ndani ya bahari hiyo hiyo kuna rasilimali ya mafuta, mafuta ambayo tungetegemea kwenye bajeti yetu angetueleza mipango ya serikali juu ya uchimbaji wa mafuta yaliyokuwepo baharini, lakini Mhe. Waziri kaamua kunyamaza kimya pamoja na kwamba suala hili lilichukua nafasi kubwa na mijadala katika kikao kilichopita tungetegemea angetudokeza kidogo kwamba serikali ina mpango huu na huu hata sera angetueleza au ile kampuni tuliyopendekeza. Lakini ukweli ni kwamba Mhe. Waziri kabakia kimya kabisa pamoja na kwamba kamuachia waziri mwenyewe, lakini na yeye angetudokeza kidogo, kwamba serikali katika kipindi hiki cha mwaka 2009/2010 tunategemea kufanya moja, mbili, tatu kuhakikisha mafuta yanachimbwa, lakini kabakia kimya, rasilimali hizi zote ziko baharini.

Mhe. Spika, Kisiwa chetu kipo katika eneo zuri la kiulimwengu na kama nafasi hiyo tuliyokuwepo tukiitumia vizuri, basi tutakuwa matajiri wa kutosha na hatutoweza kutumia au kutegemea misaada kutoka nje.

Mhe. Spika, kiwanja cha ndege tungeweza kukitumia, tukakiboresha vizuri kikawa cha kisasa zaidi, mimi naamini ndege nyingi ambazo zinakwenda katika ukanda huu wa kusini mwa Afrika na Afrika ya Mashariki basi kituo chake kikubwa kingekuwepo hapa na serikali ingeweza kukusanya mapato mengi sana, lakini hata haya maeneo huru ya uchumi kama tungeyatumia vizuri, basi mimi naamini matatizo haya ya ukusanyaji wa mapato yangekuwa kwetu ni ndoto na wenzetu wanaitumia sana fursa hii. Kule Dubai kuna maeneo wanaita *jabal aly* ni maeneo makubwa ambayo yanaiingizia serikali ya Dubai mapesa mengi.

Lakini hata bandari tuna maeneo mazuri sana ya kutengeneza bandari kubwa za kisasa, tuna eneo la Mpigaduri ambalo kama tungelitumia vizuri kujenga bandari ya kisasa meli nyingi na mizigo mingi ingeweza kuletwa hapa na kuteremshiwa hapa, lakini pamoja na kuwa na vitendea kazi vizuri basi nchi yetu hii ingebadilika na ikawa peponi.

Haya Mhe. Spika, tunayoyazungumza jibu lake tunasema kwamba hatuna uwezo wa kuyafanyia haya, lakini kama tutafungua milango na kuachana na urasimu kama tulivyozoea, basi mambo haya yote yanawezekana na kwa sababu tayari kuwa watu wana fedha zinatafuta wapi wakawekeze.

Lakini bado milango yetu tumeifunga, bado tuna mipango ile ile ya kizamani, bado tunataka tuchume leo na tutumie leo itawezekana wapi, lazima tujenge mazingira ya baadae, tutafute wawekezaji waje wawekeze katika maeneo ya uchumi ili na sisi tufaidike, sio lazima kufaidika leo lakini hata zaidi ya miaka kumi au ishirini ijayo, lakini hatimae nchi yetu iweze kubadilika na tutaachana kabisa na utegemezi huu ambao sasa hivi unaonekana ni mkubwa.

Mhe. Spika, lazima tukubaliane kwamba hata serikali imeshindwa kusimamia ipasavyo haki zetu zilizoko katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lazima hili tulikubali, baadhi ya wajumbe wamelizungumza hili lakini ndio hali halisi ilivyo tuna haki zetu nyingi zilizokuwepo katika serikali ya Jamhuri ya Muungano tunashindwa kuzisimamia ipasavyo, sijui kama alivyozungumza mwenzangu Mhe. Makame Mshimba kama ni woga au kitu gani. Lakini kama hatutosimamia haki zetu ipasavyo, basi tutaendelea kuimba kila siku na tutakuwa tegemezi wenzetu wanaendelea mbele.

Mhe. Spika, suala la mgao wa fedha za *BOT* faida inayoapatikana ya 4.5 hili nalo linatupunguzia kiwango kikubwa sana cha mapato, lakini kila siku

tunaimba 4.5 wakati shea yetu katika serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya *BOT* ni 11% kwa nini tuwe tunapewa 5% ya faida inayotokana na *BOT*. Lakini kwa kuwa hatujawa makini katika kudai haki yetu katika sehemu hii, basi matokeo yake siku zinakwenda sisi tunalalamika utupu tu, tulalamika hatuna kitu.

Mhe. Spika, kama alivyozungumza Mhe. Abubakar Khamis Bakary kuna mapato ambayo yanatokana na taasisi na mashirika mbali mbali ya Muungano ambayo yanajikusanyia pesa chungu nzima hapa, lakini sisi tuko kimya tumelala, wanatumia maeneo yetu na ardhi zetu lakini sisi hatupati hata senti moja, wanatumia anga wanakusanya kodi za anga zetu pesa chungu nzima hatupati haki yetu. Sasa haya yote yanahitaji kusimamia ipasavyo ili bajeti yetu ipungue katika masuala ya utegemezi.

Mhe. Spika, suala la tume ya pamoja na fedha *JFC* nayo tunashindwa kuisimamia hii imeundwa muda mrefu, lakini kupitia tume hii ndio tungeweza sisi basi angalau kujikwamua kutoka hapa tulipo kwa kujua tumepata au tumekosa, lakini matokeo yake suala la *JFC* limekuwa kama ndoto. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 nitanukuu kuna kipengele kimoja hapa cha Katiba kwa ruhusa yako Mhe. Spika.

Sehemu ya pili ibara ya 115 ya Katiba hii ya Zanzibar inasema hivi naomba kunukuu:-

Kifungu Nam. 115

> "Hakuna fedha itayotumiwa katika sehemu hii hadi:
> (a) Tume ya pamoja ya fedha inayohusu mambo ya Muungano kama ilivyoainishwa na Katiba ya Muungano imechambua mapato na matumizi ya shughuli za Muungano na kutoa mapendekezo yake kwa vyombo vinavyohusika juu ya mgawanyo wa matumizi hayo; na
>
> (b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuyakubali mapendekezo hayo na mgawanyo wake.

Mhe. Spika, kama hatutosimamia vizuri suala hili la *GFC* tutawezaje kujua hizi taasisi za Muungano zinazozungumziwa hapa. Ni maeneo gani ya Muungano, tunastahiki nini sisi katika Muungano juu ya fedha hizi, lakini hadi leo imekuwa ni hadhithi. Tumezungumza toka tulipokuja hapa kesho na keshokutwa tunaondoka lakini bado suala la *GFC* itakuwa hadithi.

Mhe. Spika, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi zaidi ya mara tatu tumeomba kukutana na hii Tume ya Pamoja ya Fedha lakini hadi leo imeshindikana. Mwisho kamati ya juzi tulimuomba Mhe. Waziri wa Fedha tukamwambia kamati yetu tunataka utukutanishe na hii kamati, lengo letu la kukutanishwa na kamati Mhe.Waziri tunataka tuiambie ijuuzulu mara moja, kwa sababu imeshindwa kusimamia wajibu wake, hilo ndio lengo letu kubwa. Tunawaambia tunataka mjiuzulu hapa kwa sababu kazi mliopewa na serikali imewashinda. (*Makofi*)

Wakati tulipotembelea sekretarieti ya tume Kamati ya Fedha na Uchumi wametueleza matatizo mbali mbali ambayo hata tume haina habari, kazi yao ni kujikusanyia maposho na vikao wakaondoka. Kwa hivyo, lengo na madhumuni ya kukutana nao ni kuwataka wajiuzulu mara moja, lakini hadi leo tumeomba mara tatu kukutana nao imeshindikana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba tume hii ya *GFC* wajumbe wake utukutanishe na Kamati ya Fedha na Uchumi.

Jengine kila wakati tumekuwa tukizungumzia juu ya mapato ya *income tax* ambayo yanatakiwa yatolewe na wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambao wanafanya kazi hapa, lakini hadi leo imekuwa *silence*. Kwa hivyo, ni maeneo ambayo kwa kweli kama ingeweza kushughulikiwa ipasavyo basi mapato ya nchi yangeweza kukua na tukaondokana na utegemezi.

Mhe. Spika, haya yako mengi tu, lakini katika suala la hatua ya kuimarisha mapato ya serikali, serikali imesema kwamba itatayarisha sera ya ukusanyaji na kusimamia mapato ya nchi, lakini nilikuwa najiuliza Mhe. Spika, hivi kumbe sera ya kusimamia ukusanyaji wa mapato hadi leo haipo? Lakini sera hii lengo lake nini? Sera lengo lake maana yake ni kuongeza mapato ya serikali lakini pia kuwashajihisha wananchi wetu waweze kukusanya au kulipa kodi kwa hiari bila ya kusimamiwa. Lakini pia ni kuziba mianya ile ambayo wananchi wanaitumia ya ulipaji wa kodi za serikali. Kwa hivyo, haya yote Mhe. Spika, kama yatatekelezwa basi hii sera tayari ipo na mipango yetu ya kodi itakuwa ipo na maendeleo yatapatikana.

Mhe. Spika, namalizia juu ya suala la serikali kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT)* kutoka asilimia 20 hadi asilimia 18. Naipongeza, lakini imewasahau wale wanaolipa kodi ya *Hotel Levy* ambayo kodi ile inafanana na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Eneo hili halikuweza kuangaliwa.
Mhe. Spika, kwa kuwa muda umemalizika kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magomeni tunaikubali hotuba hii na tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mkongwe Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake (SAW) aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa tuko katika hali ya uzima na salama.

Mhe. Spika, pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu mdogo.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi alivyoitoa hotuba ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, hotuba hii imeeleza mengi, lakini mimi nakwenda kwenye wanawake wakulima wa mwani vijijini. Wanawake wa vijijini ni wakulima wakubwa wa zao la mwani, mwani unazalishwa ndani ya maji ya bahari na maji hayo sio ya magotini ni kuanzia tumboni mpaka kifuani na wanawake hao wengine hupoteza roho zao. Kwa hivyo, ninaiomba serikali pamoja na mwenyewe Mhe. Waziri wanawake hawa wawatizame kwa kipaumbele ili wazidishe kilimo chao na kilimo kile wazidishiwe mapato, kama mwani unauzwa kilo shilingi 1000 basi mimi nawaombea iwe kilo shilingi 2000.

Mhe. Spika, pia nampongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoelezea kwamba kilimo kakipa kipaumbele hasa kilimo cha umwagiliaji pamoja na kilimo cha juu. Mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri azidishe kilimo cha juu kukipa kipaumbele kwa sababu wakati wa kilimo unapofika kusema kweli wananchi wanahangaika kwa sababu majembe yanakuwa hakuna, mbolea na madawa.

Mhe. Spika, kipindi hiki cha mwaka huu ingelikuwa kuna majembe, mbolea na madawa basi wananchi hata hayo mapembe wasingeyajua. Kwa sababu wananchi wameitikia wito mkubwa sana mwaka huu haijapata kutokea, wananchi wamelima kweli kweli lakini kipato chao ni kidogo kwa sababu hawana madawa, mbolea hawana chochote, hata hao mabwanashamba pia hawawapitii.

Mhe. Spika, unaweza kwenda kwenye bonde ukaona mwitu ukafikiria labda mpunga ule uliochanua kumbe ni chicha, kuna jani kule kwetu linaitwa chicha linachanua mauwa linakuwa jekundu, sasa ukiliona utafikiria labda ni huo mpunga kumbe ni gugu. Sababu ya gugu hilo halina mbolea, halina dawa wala chochote na watu hawakulima kwa mpango. Kama ukifikia muongo majembe yakasambazwa katika mabonde basi ingekuwa nafuu, lakini hakuna hilo, katika Mkoa mzima kuna jembe moja au mawili. Mhe. Spika, majembe yamekaa kama binadamu mara yanahoma, mafua na halafu huku mwananchi kaganda anangojea kulimiwa mpaka miongo inapita analima pantosha, panvuna, pankwisha. Tunamuomba Mhe. Waziri kama kweli kapania safari hii kulima

kwa majembe basi atangulize majembe mapema katika mabonde ili wananchi wasipate tabu.

Mhe. Spika, wananchi wanapata tabu sana kwa kulima, watu wanataka kulima lakini zana hakuna. Hapa utasikia tunaambiwa kilimo uti wa mgongo kweli ni uti wa mgongo ukiutekeleza, lakini kama huutekelezi utakuwa kilimo ni uti wa kifua. Kwa sababu badala ya kulima kwa uti wa mgongo unalimwa kwa kifua. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri akipe kipaumbele hicho kilimo.

Vile vile nampongeza Mhe. Waziri kwa kuwaongezea mishahara wafanyakazi wa kima cha chini. Sihaba, watu wanasema, "Ingawa kidogo cha ng'ara". Hicho ni kidogo lakini kinang'ara sihaba tunamshukuru, lakini tutapopata lile donge nono basi tuwaongeze zaidi kutokana na maisha haya tuliyonayo.

Mhe. Spika, shilingi laki moja tusiwafurahie kuwa wameongezwa wee, wameongezwa, kwa sababu toka juzi watu waliposikia wamefurahia. Kuna watu wengine hawajui basi waliposikia wafanyakazi wameongezwa mishahara sasa hivi lile fungu la muhogo badala ya kulipata kwa shilingi 1000 basi linauzwa shilingi 2000, kwa sababu wanaona mishahara imeongezwa kumbe hawajui kuongezwa kule wameongezwa kiasi gani na hawajui kwamba laki moja hiyo ukienda nayo hapo Darajani mkoba haujai. Sasa tungemuomba Mhe. Waziri donge likiwa nono awaongeze zaidi wafanyakazi.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri kama wenzangu waliotangulia walivyoizungumza barabara ya Bumbwini na mimi nimetumwa na wanawake wa Bumbwini niizungumze. Mimi ni mmoja wapo wa wanawake wa Bumbwini na nataka niulize huku Bumbwini kumekosa nini? Kama liko jambo tulilokosa watu wa Bumbwini basi bora tuambiwe kuliko kufichwa tukaachwa tukateseka. Kwa sababu mtu unastahamili mpaka stahamala inakifikia dakika ya mwisho. Mhe. Spika, mtu hata akikunyooshea mdomo au kidole ujue hilo jambo limeshamtosha na watu wanasema, "Siri ya Mtungi iulize kata". Sasa siri ya barabara ya Bumbwini tunaijua sisi tunaokuja asubuhi na jioni tuko hapa.

Mhe. Spika, mimi labda niwaombe wajumbe wako kama barabara ya Bumbwini hawaijui wachukua hii *week end* inayokuja ya wiki hii tunayokwenda nayo, chakula cha kuwalisha nitawapikia mimi waje waiangalie barabara ya Bumbwini. Kwa sababu kama uliiona mwaka jana 2008 basi imebovuka hivi sasa haifai. Mtu mwenye raha yake na kuupenda mwili wake Bumbwini haji kutokana na barabara yake ilivyo na watu wote wanajua hapa.

Mhe. Spika, kulikuwa na kamati ilitembelea barabara ya Bumbwini, basi badala ya kuanza huku tunakotokea Mfenesini ilikwenda kuanza Bumbwini

Makoba kutia kile kifusi, tukatia kifusi mpaka skuli ya Bumbwini ndio walipomalizia.

Mhe. Said Khelef Ali husema kila siku wamerashia, wamerashia, akitaja kurashia hapa watu sijui hufikiri karashia nini wanacheka, kumbe karashia lile dongo hakuna chengine alichorashia, lakini akitaja nimerashiwa basi watu hapa husema aa kabiga brashi wanafikiria labda brashi ya kitu chengine. Mheshimiwa anakusudia brashi ya lile dongo lililofikia pale. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, mvua ya juzi hiyo brashi haipo tena, tunataka tujue kosa la watu wa Bumbwini ni nini?

Mhe. Spika, Bumbwini kuna wanawake wanakuja Mjini wanapata rufaa ya kuja kujifungua, fikiria mzazi anaumwa na uchungu, Mhe. Spika, uchungu hujawahi kuuona lakini umewahi kumuona mama anapoumwa anavyokunja uso, mtu akikunja uso ujue anaumwa basi mtu anaumwa na uchungu analetwa Mjini kweli Mheshimiwa ile si dhambi jamani tunayoipata? Jamani wakubwa tuoneeni huruma watu wa Bumbwini tunaumia. Kuna maradhi mengine ya siri jamani wanaume wanaugua na wanawake wanaugua, lakini inabidi lazima tujitise mle tujitikise. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, nakuomba pamoja na Mhe. Waziri humu kwenye kitabu kama alivyosema Mhe. Said Khelef Ali hakuna lolote alilolitaja Mhe. Waziri, kwa sababu angalau angetaja kwamba barabara zilizojengwa na hii itajengwa angetudanganya na sisi moyo wetu ungekuwa mzuri tukenda tukawadanganya wenzetu, lakini sasa hivi hata hatuna la kuwaambia kwa sababu vitabu wameshaviona na bajeti imeshasomwa na wao wameisikia, tutawadanganya vipi watu wa Bumbwini? Tumeonewa kwa kiasi gani?

Mhe. Spika, mimi naona bora niishie hapa. Kwa hayo machache mimi naunga mkono hotuba hii mia kwa mia, sipigi buti ninamwachia tu Mhe. Waziri kwa sababu ni mtu mzima na akili yake huyo, kama nikisema hivyo hivyo iko siku atanionea huruma wala sipigi buti atanionea huruma mwenyewe. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Kicheko)*

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 23/06/2009 saa 3:00 asubuhi)